# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA TATU

**Kikao cha Tano – Tarehe 3 Aprili, 2006**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D UA**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge napenda kutangaza kwamba bado kuna nafasi ya kuchangia kwenye Muswada wa Benki Kuu. Ninao wachangiaji kumi, lakini tulikuwa tunadhani ni vizuri Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Kamati ya Bunge nzima tuweze kuifanya kesho asubuhi. Kwa hiyo, tunaomba sana wale ambao pengine walikatishwa tamaa wajue kwamba nafasi bado ipo na niko tayari kupokea majina.

La pili, kuhusu maswali ya nyongeza nimepata malalamiko kutoka upande huu wa kushoto na pia upande wa kulia. Kwa hiyo, naona niko sawa tu kwa sababu kama pande zote wanalalamika basi Spika anafanya haki. *(Makofi)*

Waheshimiwa wabunge nawakumbusha tu kwa sababu leo tuna maswali 17, kwa hiyo itanibidi nijitahidi twende haraka ili tuweze kukidhi mahitaji ya hao waliouliza maswali na wengine wapate nafasi ya kuuliza maswali kesho. Kwa hiyo, natanguliza kuwaomba radhi tutakwenda haraka kidogo na pengine maswali ya nyongeza hayatakuwa mengi kama ambavyo mlivyotarajia. Katibu tuendelee na *Order Paper.*

### MASWALI NA MAJIBU

**Na. 58**

**Kodi za Majengo katika Miji na Manispaa Nchini**

**MHE. JOB Y. NDUGAI (k.n.y. MHE. HERBERT J. MNTANGI)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Ofisi ya Waziri wa Nchi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa iliyo chini ya Waziri Mkuu, ndiyo yenye dhamana ya kusimamia Halmashauri zote na kuidhinisha Sheria ndogo ndogo za kodi na ushuru:-

(a) Je, kwa nini kodi za majengo katika Miji, Manispaa na baadhi ya Miji midogo ni kubwa kufikia zaidi ya Shs.150,000/ kwa mwaka, nje kabisa na kodi za viwanja zinazotozwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi hata kama nyumba hizo sio za barabara?

(b) Je, Serikali haioni kuna haja ya kuondoa kodi hizo kwa nyumba zinazomilikiwa na wazee wastaafu na wajane ambao hutumia nyumba hizo kwa maisha yao binafsi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mbunge wa Muheza, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Halmashauri za Miji na Manispaa hutoza kodi ya majengo kutokana na kifungu namba 13(1) cha Sheria Namba 9 ya mwaka 1982. Halmashauri hizi hutoza kodi hii, pamoja na kodi zingine, kwa sababu kwa mujibu wa kifungu cha 14 cha Sheria Namba 9 ya mwaka 1982 Halmashauri zinatakiwa kuwa na fedha za kutosha kutekeleza majukumu na shughuli ambayo wananchi wanawategemea watekelezewe kwenye maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kodi ya majengo inaweza ikafikia hadi Sh.150,000/= au zaidi kwenye Miji na Manispaa, kwani hii inatokana na thamani ya jengo. Halmashauri kupitia Sheria ndogo ndogo ilikubaliwa kuwa majengo yote mazuri ambayo ni ya kisasa na yaliyokwishathaminiwa yatatozwa kodi za majengo kwa asilimia moja ya thamani ya jengo.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ambazo hazijathamini majengo yake zinaweza kuamua kutumia njia nyingine kutoza kodi ya majengo. Kiwango cha kodi kinachotozwa ni kile ambacho Halmashauri inaona kuwa wakazi wa eneo husika wanaweza kulipa kodi hiyo (*affordable economical area*). Nyumba zinazotozwa ni zile ambazo ni imara. Majengo ambayo hayatumiki, majengo ya tope, na majengo yaliyosamehewa kodi chini ya kifungu Namba 7 cha Sheria ya Kodi ya majengo namba 2 ya mwaka 1983, pia kifungu 4(b) cha jedwali la Sheria ya Fedha namba 15 ya mwaka 2003 inayorekebisha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Namba 9 ya mwaka 1982, majengo hayo hayatozwi kodi.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali haioni sababu ya kuondoa kodi hizo kwa wazee wastaafu na wajane kwa sababu majengo ya thamani kama hayo yanahitaji kupatiwa huduma za msingi na Halmashauri kama vile barabara, mfumo wa maji machafu,

usombaji taka ngumu na kadhalika. Aidha, wanaomiliki majengo hayo ni watu wanaojiweza, na baadhi yao wanayatumia kwa biashara. Hata hivyo, kwa maeneo ambayo Halmashauri haijafanyia tathmini majengo yake taratibu zinaruhusu jambo hilo kupelekwa kwenye Halmashauri ili lijadiliwe na kutolewa uamuzi ulio muafaka.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza na ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake. Kwa kuwa, imedhihirika na amekubali kwamba kwa kweli baadhi ya viwango vya kodi vinafikia sh. 150,000/= na hata kuzidi. Lakini suala nzima hapa ni kuhusiana na nyumba za kuishi ambazo wala si za biashara. Je, atakubaliana nami kwamba ipo haja ya kutoa maelekezo maalum kwa kodi hii ya majengo iwe *stream lined* vizuri na isiwe kama ilivyo sasa ambapo ni vurugu tupu kiasi kwamba katika maeneo mengine ya Miji midogo kama kule Kibaigwa, Mlali, Kongwa na kwenye Halmashauri nyingine hata nyumba za miti na tope bado zinadaiwa kodi ya nyumba anasemaje kuhusu hilo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, Halmashauri zote zimepewa madaraka ya kutunga sheria ndogo ndogo kama kuna Halmashauri inaona kwamba kuna tatizo la utozaji wa kodi za majengo naomba lianzie kule kule kwenye Halmashauri kutunga hiyo sheria ya *exemption* kwa ajili ya majengo ya aina hiyo, kwa ajili ya wajane na kwa ajili ya wastaafu likiletwa kwetu sisi tutaliangalia na kulishughulikia. Lakini sheria zote ndogo ndogo zinaanzia kwenye Halmashauri husika. Kwa hiyo, namshauri Mheshimiwa Mbunge arudi kwenye Halmashauri yake kushirikiana katika vikao mbalimbali ili kutunga sheria kwa ajili ya *exemption* ya majengo hayo. *(Makofi)*

**Na. 59**

**Kupandishwa Hadhi Kituo cha Afya *Mbambabay***

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipofanya ziara Wilayani Mbinga aliahidi kupandisha hadhi ya Kituo cha Afya cha *Mbambabay* kuwa Hospitali kamili na kuongeza Madaktari katika Hospitali ya Liuli na kupeleka gari la wagonjwa. Pia kupandisha hadhi ya kituo cha Afya cha Lituhi kuwa Hospitali:-

(a) Je, ni lini ahadi hizo zitatekelezwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Capt. John Komba, Mbunge wa Mbinga Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba viongozi wetu wa Kitaifa wanapofanya ziara za kikazi ndani ya nchi mara nyingi wanatoa ahadi mbalimbali kwa wananchi. Hili linawezekana katika mikutano ya hadhara au mikutano ya ndani au katika mazungumzo. Ahadi hizo huwa zinalenga kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi na kuwaondolea kero. Aidha, ili kutekeleza ahadi hizo Mikoa na Halmashauri husika inatakiwa kuweka ahadi hizo katika mpango na Bajeti za kila mwaka na zinatekelezwa kulingana na uwezo ulioko. Hivyo, juhudi zinafanywa na Ofisi yangu ili tupate ahadi zote hizo ambazo Mheshimiwa Rais alizitoa wakati alipotembelea Wilaya ya Mbinga wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu wa mwaka 2005 ziweze kutekelezwa kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, kulingana na Sera ya Afya Hospitali za Mashirika ya dini zinao utaratibu wao wa kupata watumishi ikiwa ni pamoja na madaktari. Aidha, suala la Serikali kupeleka gari la wagonjwa katika hospitali ya Liulil Ofisi yangu itawasiliana na Wizara ya Afya kama inaweza kusaidia suala hilo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kupandisha hadhi vituo vya Afya vya Lituhi na *Mbambabay,* Kituo cha Afya cha Lituhi kinamilikiwa na Kanisa la *Roman Catholic* – Lituhi na kile cha *Mbambabay* kinamilikiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga. Kwa Kituo cha Afya cha *Mbambabay* cha Halmashauri inawezekana kupandishwa hadhi kwa kufuata vigezo vilivyopo na utaratibu wake ni kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga inatakiwa kuwasilisha maombi hayo Mkoani na Mkoa kuwasilisha maombi hayo Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, na kuhusu kituo cha Afya cha Lituhi kinachomilikiwa na *Roman Catholic*, Ofisi yangu itawasiliana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ili kuona jinsi gani linawezekana kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba vigezo vinavyotakiwa ili Kituo cha Afya kiweze kupandishwa hadhi kuwa hospitali ni kama vifuatavyo:-

(i) Idadi ya watu itakayohudumiwa na Hospitali ifikie watu kati ya 150,000 hadi 250,000. Kituo cha Afya cha *Mambabay* sasa hivi kinahudumia eneo lenye wakazi wapatao 31,700.

(ii) Idadi ya watumishi wa kada mbalimbali kwa hospitali ni watumishi 103. Kituo cha Afya cha *Mbambabay* kwa sasa kina watumishi 18 tu. *(Makofi)*

(iii) Kuwepo kwa majengo na eneo la kutosha kwa ajili ya upanuzi.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema ahadi hizo zikiwasilishwa tutawasiliana na vyombo mbalimbali ili kuona ni jinsi gani ahadi hizo zinaweza kutekelezwa.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kituo cha Lituhi kilihamishwa na Serikali mwaka 1976 kikiwa hospitali. Wananchi walihamishwa kupelekwa kwenye maeneo mengine kwa madai ya mafuriko ya maji; na kwa kuwa mwaka 1986 Serikali iliwarudisha

wananchi wale kule na watu wa missionari kukataa kuiendesha hospitali ile tena na Serikali kulazimika kuwajibika kuanzisha kituo cha Afya; na kwa kuwa kituo cha Lituhi kiko kilomita 160 kando kando ya Ziwa Nyasi mpaka Makao Makuu ya Wilaya.

Je, hayo mazungumzo kati ya Wizara husika na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii yatakwenda haraka ili watu wale wasaidiwe Kituo chao cha Afya kiwe hospitali? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema mwanzoni kwenye jibu langu la msingi ni kwamba Kituo cha Afya cha Lituhi kinamilikiwa na madhehebu ya dini na mpaka sasa hivi hatujapewa taarifa rasmi kwamba kimehamishiwa Serikalini. Pindi tutakapopewa taarifa rasmi kwamba kituo hicho cha afya kinamilikiwa na Serikali sisi tutachukua hatua mbalimbali katika kukiinua au kukisaidia hicho kituo cha Afya cha Lituhi.

Kuhusu hospitali ya Liuli kadhalika pia inahudumiwa au ni mali ya mashirika ya dini na mashirika ya dini yana sheria zao za kuwasaidia wananchi na pia kuwapata madaktari au vifaa mbalimbali. Lakini pamoja na hayo ni kwamba vituo vyote vya Afya na hospitali za madhehebu ya dini vinavyomilikiwa na watu binafsi au mashirika ya dini vinapata ruzuku kutoka Serikalini kwa ajili ya watoto na akinamama wajawazito. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya ziada Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa maelezo ya ziada zaidi ya maelezo mazuri aliyotoa Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Rais alipopita katika maeneo mengi alitoa ahadi na ahadi nyingi zipo katika Ilani ya Uchaguzi.

Lakini kulikuwa na ahadi vilevile ambazo zilikuwa za papo kwa papo, hapa nashangaa kwamba alitoa ahadi mbili katika vituo viwili vidogo vipandishwe hadhi lakini hilo tutaliangalia.

Kwa hospitali ya Liuli Serikali imekuwa ikitoa *bed grant* na mishahara. Mwaka jana tulitoa shilingi milioni 67 na mwaka huu tumetoa shilingi milioni 89. Lakini hivi sasa tuko katika mchakato wa kuchambua ahadi zote ili tuzipangie muda wa utekelezaji na hizi ahadi ni za miaka mitano. Kwa hiyo, tusipotekeleza leo, tutaiweka kwenye mipango ili ifikapo miaka mitano tuwe tumekamilisha. *(Makofi)*

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Hospitali ya Amana katika Jimbo la Ilala, imeshatimiza masharti yote na ina hadhi kubwa sana. Lakini mpaka leo hospitali hii bado haijapewa hadhi ya kimkoa. Je, Serikali haioni sasa ni muda muafaka hospitali ya Amana kupewa hadhi ya Hospitali ya Mkoa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Nadhani ni Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii sasa.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, hospitali ya Wilaya inaitwa hospitali ya Wilaya. Mpaka sasa katika utoaji wetu wa huduma Ilala imekuwa ikitambulika kama Wilaya kwa hiyo hii hospitali ni ya Wilaya. Ahsante.

**Na. 60**

**Suala la Kupambana na Rushwa**

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA** aliuliza:-

Kwa kuwa, rushwa ni adui wa haki na maendeleo; kwa kuwa rushwa hiyo imekithiri katika nchi yetu:-

Je, Serikali ya Awamu ya Nne imejizatiti vipi kukabiliana na tatizo hilo sugu katika nchi yetu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mbunge wa Micheweni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, wakati akilihutubia Bunge kwa mara ya kwanza alisema naomba nimnukuu: "Tutaongeza kasi ya kupambana na rushwa kisayansi kwa kushambulia kiini chake na kuziba mianya yake." Mwisho wa kunukuu.

Aidha, Mheshimiwa Spika, juzi juzi tarehe 31 Machi, 2006 alipokuwa akilihutubia Taifa kutoka hapa Dodoma kuhusu mafanikio ya Serikali hii katika siku 100 za kwanza, Mheshimiwa Rais alisema naomba pia kumnukuu: "Tuliahidi kwamba tutapambana na rushwa kwa nguvu zetu zote. Nina furaha kuwaarifu wananchi kwamba tumeshaanza kuchukua hatua kwenye vita hii. Nilikaa na uongozi wa Taasisi ya Kuzuia Rushwa, tukabadilishana mawazo kwa kirefu na wao wakaahidi kwamba baada ya miaka 10 ya kujipanga na kujijenga kitaaasisi, sasa tutaona kasi na makali yao katika kupambana na vita hivi vya rushwa. Ninaomba waendelee na vita hii bila kuogopa wala kumwonea haya mtu yeyote. Naomba wananchi tuwape ushirikiano wetu. Na yule ambaye wanadhani hawamwezi wamlete kwangu." Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya ni matamshi mazito sana kutoka kwa Mkuu wa Nchi na hakuna wasiwasi wa kuyatilia mashaka. Serikali itaangalia upya taratibu za kuingia katika mikataba zinazotumiwa na Serikali, Mashirika ya Umma na Idara zinazojitegemea kwa lengo la kuongeza uwazi na uwajibikaji. Serikali pia itahakikisha kuwa watendaji wake wanakuwa na uadilifu wa hali ya juu na wenye kuzingatia misingi ya uwajibikaji na maadili ya kazi na kutoa huduma bora kwa umma. Vilevile, Serikali itaongeza uwazi

katika maamuzi yake na kuimarisha uwezo wa kifedha na kiutendaji wa taasisi zilizo mstari wa mbele kwenye vita dhidi ya rushwa hususan Taasisi ya Kuzuia Rushwa, Jeshi letu la Polisi na pia Mahakama. Serikali inawaomba wananchi kutoa ushirikiano kwa vyombo hivyo ili kufanikisha mapambano dhidi ya rushwa. *(Makofi)*

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Tatu ilikuwa ikishughulikia zaidi rushwa ndogo ndogo kama vile za Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo, Askari Polisi na kadhalika. Sasa je, Serikali ya Awamu ya Nne imejizatiti vipi kupambana na rushwa kubwa kubwa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu naomba nimtambue Mheshimiwa Shoka Khamis Juma kama Msemaji Mkuu wa Upinzani wa eneo la Utawala Bora. Kazi yetu mimi na yeye na viongozi kwa ujumla ni nyeti, ni kazi ngumu na ina wigo mpana sana ikiwa ni pamoja na kupambana na ujambazi pia. Sasa baada ya kusema hayo, naomba nimjibu kama ifuatavyo: Taasisi ya kuzuia rushwa siku za karibuni imeonyesha waziwazi kwamba sasa iko tayari kupambana na rushwa za aina zote ndogo na kubwa. *Inshallah* ni yale tunayosoma kila siku katika magazeti yetu. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, lakini kabla ya hapo sina hakika kama ni busara kwa Waziri kumshambulia mtu kwa tatizo lake la binafsi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hilo, naomba kuuliza swali lifuatalo. Kwa kuwa Awamu ya Tatu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, kwa sababu ulilolisema lilikuwa linastahili kama lingekuwa halisi Spika achukue hatua. Napenda kukuhakikishia kwamba Mheshimiwa Waziri hakukosea lolote. Kwa sababu alichosema ni kwamba mambo kama rushwa, ujambazi kwa kweli yote ni maovu na siyo wajibu wa Waziri na mwenzake Waziri Kivuli kupambana nayo ni sisi sote Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa ufafanuzi huo. Naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Tatu iliunda Tume ya kuchunguza mianya rushwa na vilevile kutoa mapendekezo kwa Serikali na Taarifa hiyo ya Tume ya Jaji Joseph Warioba mbali na kupendekeza mianya ya kuziba rushwa pia ilitoa orodha watu mbalimbali ambao walituhumiwa kuhusika na rushwa na kuitegemea Serikali kuchukua hatua. Aidha, hivi karibuni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Taifa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete aliwambia Watanzania kwamba anayo orodha ya watuhumiwa wa rushwa. Je, Serikali ina sababu gani za msingi za kutowafikisha mahakamani wale watu ambao tayari walipendekezwa na Jaji Joseph

Warioba na juzi Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, alithibitisha kwamba wanayo orodha yao? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali ya Awamu ya Tatu iliundwa Tume inayojulikana na kama Tume ya Joseph Warioba na Serikali iliifanyia kazi ripoti ya Tume hiyo kikamilifu na ndiyo maana leo tunaongea kuhusu miaka 10 ya jinsi ambavyo Tume ya Kuzuia rushwa imejipanga vizuri. Taarifa ya Tume ile imetumika katika kuongeza mtandao wa Taasisi ya Kuzuia Rushwa hadi Wilayani, imeongeza uwezo wake wa kufanya kazi, mapendekezo ya kuongezewa fedha yametekelezwa na Serikali. Orodha ya waliokuwa wakishukiwa ni wapokea rushwa wakubwa ilipokewa na hata sasa bado kuna orodha kama hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini ni kitu kimoja kuwa na orodha na kutia mashaka watu wanaopokea rushwa. Lakini ni kitu kingine kabisa kujenga hoja ya kufungua kesi Mahakamani, kesi ambayo una hakika utashinda. Utaratibu wetu wa kisheria ni kwamba anayeshitaki lazima athibitishe kweli kweli ili kumtia mtu hatiani na masuala haya ya rushwa mnavyofahamu siyo rahisi kuthibitisha kabisa kabisa kwamba mtu ana hatia. Ndiyo maana pamoja na kuwa orodha inaonekana ni vigumu kuwapeleka Mahakamani watu kama hao. Kwa wale ambao Serikali ina uwezo nao huwa inachukua hatua za kinidhamu kama vile kuwastaafisha kwa manufaa ya umma na kadhalika. *(Makofi)*

**Na. 61**

**Ukosefu wa Maji Jimbo la Ubungo**

**MHE. CHARLES N. KEENJA** aliuliza:-

Kwa kuwa, kwa muda mrefu sana maeneo mengi ya Jimbo la Ubungo lenye Kata kumi na moja yanakabiliwa na tatizo kubwa la ukosefu wa maji; na kwa kuwa tatizo hilo limesababisha maisha ya wakazi wengi wa Jimbo hilo hususan wanawake kuwa magumu sana:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kulitatua tatizo hilo katika maeneo ya Jimbo hilo?

(b) Je, utekelezaji wa mipango hiyo utachukua muda gani, hadi wananchi wapate maji, Serikali haioni kwamba ni vyema kutafuta vyanzo vya maji vinavyoaminika badala ya kutegemea maji kutoka mto unaotembea kama ilivyo sasa?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Charles Keenja, Mbunge wa Jimbo la Ubungo, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Jiji la Dar es Salaam na baadhi ya maeneo ya Kibaha na Bagamoyo hupata majisafi ya bomba kwa matumizi mbalimbali kutokana na Mfumo wa Majisafi toka Mto Ruvu Juu. Shirika la Umma la *DAWASA* ni mmiliki wa Miundombinu. Mfumo huo ambao *DAWASCO* ni mwendeshaji wa maji. Mfumo huo ambao baadhi ya miundombinu yake imejengwa miaka ya 1950 na 1970 ni mdogo na chakavu. Aidha, mfumo huo unakabiliwa na matatizo yafuatayo:-

(i) Uwezo mdogo wa mitambo kuzalisha maji usiolingana na mahitaji. Kiasi cha maji kinachozalishwa ni mita za ujazo 270,000 kwa siku ambacho ni asilimia 60 tu ya mahitaji yanayofikia mita za ujazo 450,000 kwa siku.

(ii) Upotevu mkubwa wa maji unaofikia asilimia 55 unaotokana na uvujaji wa mabomba, uendeshaji wa chujio na maji yasiyolipiwa.

(iii) Upungufu wa maji wa mara kwa mara kwenye mto Ruvu unaosababishwa na uharibifu wa mazingira na ukame.

(iv) Mitambo ya kusukuma maji kuharibika mara kwa mara kutokana na uchakavu wa mashine.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa napenda kujibu swali la Mhesimiwa Mbunge lenye vipengele (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili kutatua matatizo ya maji Jijini Dar es Salaam Jimbo la Ubungo likiwemo, Serikali kupitia *DAWASA* inatekeleza Mradi wa Uboreshaji huduma ya majisafi na majitaka kwa gharama ya dola za Kimarekani milioni 164.6, mradi huo ulianza kutekelezwa mwaka 2003 na umepangwa kukamilika mwishoni mwa mwaka 2007. Taasisi zinazogharamia mradi huo ni pamoja, Benki ya Dunia Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Rasilimali ya Nchi za Ulaya, *DAWASA* yenyewe na *DAWASCO.*

Mheshimiwa Spika, kazi zinazofanyika chini ya mradi huu ni pamoja na ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya maji safi na majitaka, progarmu ya miradi ya kijamii ya huduma ya maji na usafi wa mazingira, uimarishaji wa *DAWASA* ili iweze kuhudumia sawa sawa. Matayarisho ya upanuzi wa miundombinu ya majisafi, uondoaji wa majitaka na usafi wa mazingira pia yanatumia fedha hizo hizo..

Mheshimiwa Spika, ni matarajio ya Serikali kuwa baada ya mradi huo kukamilika maeneo mengi ya Jiji la Dar es Salaam likiwemo Jimbo la Ubungo yatapata majisafi na salama ya kuaminika zaidi, badala ya kupata kwa mgao kama ilivyo hivi sasa. Hivyo namwomba Mheshimiwa Mbunge Charles Keenja, Mbunge wa Jimbo la Ubungo pamoja na wananchi wake wa Ubungo wavute subira kwa jambo hilo..

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi hizo, upembuzi yakinifu wa mradi wa uendelezaji wa chanzo kipya cha maji unafanyika. Vyanzo vipya vinavyochunguzwa ni pamoja na visima virefu katika Mto Mpiji, Kizinga, Kigamboni. Aidha, usanifu wa

bwawa linalotarajiwa kujengwa kwenye Mto Ruvu katika eneo la Kidunda mkoani Morogoro umeshaanza. *(Makofi)*

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana na yanayotia matumaini. Lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

La kwanza Mheshimiwa Waziri alipotembelea mitambo ya Ruvu Juu aliwaagiza wahusika wahakikishe kwamba mitambo iliyoagizwa India inawasili nchini kabla ya mwezi Aprili sasa tuko katika mwezi wa Aprili tayari ningeomba kujua mafanikio yaliyopatikana mpaka sasa.

Lakini la pili kuna habari kwamba kuna maji mengi sana chini ya ardhi Kaskazini mwa Kawe na Kusini mwa Bandari ya Dar es Salaam Serikali inachukua hatua gani kuthibitisha ubora wa maji hayo na kuyachimba ili yasambazwe katika Jiji la Dar es Salaam. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba ni kweli Waziri wa Maji alitoa agizo pampu ziagizwe na pampu hizo zimeshaagizwa kutoka Australia na gharama ya pampu hizo ni jumla ya dola 22,346,000.

Mheshimiwa Spika, swali la pili ni kwamba Jiji la Dar es Salaam limeshaanza kufanya uchunguzi kama nilivyosema na sasa hivi tuna uchunguzi wa Bwawa la Kidunda na pia tuna uchunguzi wa mito mitatu ambapo kuna Mpiji na Kigamboni. Hiyo ya Kigamboni ni kwamba ndiyo maji ambayo tunasema yako mengi chini ya ardhi na ndiyo hicho sasa hivi uchunguzi utafanyika mara ambapo fedha zitakapopatikana. *(Makofi)*

**Na. 62**

**Ujenzi wa Bwawa la Manchira**

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI (k.n.y. MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne alipotembelea Mji wa Mugumu mwezi Septemba, 2005 aliahidi kuwa Bwawa la Manchira litakamilika mwaka huu (2006) na kwamba, yeye mwenyewe atakwenda kulifungua:-

(a) Je, ni lini Serikali itaanza kazi ya kutengeneza tuta la Bwawa hilo na kulaza mabomba hadi Mugumu Mjini, na kazi hiyo itakamilika lini?

(b) Je, ni lini Mheshimiwa Rais atakwenda Mugumu kulifungua Bwawa hilo kama alivyoahidi?

(c) Je, ni lini wananchi watakaohamishwa kutoka kandokando ya bwawa hilo watahamishwa na watalipwa fidia kiasi gani na fidia hiyo itaanza kutolewa lini?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, Mbunge wa Serengeti, swali lake lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ujenzi wa bwawa la Manchira umeanza na hadi sasa upasuaji wa mawe na uchimbaji wa mtaro umekamilika. Hatua inayofuatia ni ujenzi wa tuta la bwawa ambao utaanza baada ya kupata fedha kutoka HAZINA za kukamilisha ujenzi wa tuta hilo.

Ni matarajio yetu kuwa ujenzi wa bwawa hilo utakamilika katika kipindi cha mwaka 2006/2007 kama fedha zitapatikana kama jinsi tulivyoziomba. Aidha, ulazaji wa mabomba kutoka kwenye bwawa hadi Mugumu Mjini utaanza baada ya ujenzi wa bwawa kukamilika.

(b) Mheshimiwa Spika, baada ya ujenzi wa bwawa la Manchira kukamilika Wizara yangu kwa kushirikiana na uongozi wa Mkoa wa Mara na Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti itamwalika Mheshimiwa Rais ashiriki katika ufunguzi wa bwawa hilo.

(c) Mheshimiwa Spika, mnamo mwezi Aprili, 2006 Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti itaanza kazi ya kuweka mipaka ya eneo la bwawa ikiwa ni pamoja na kutathmini mali za wananchi watakaohamishwa. Hivyo, gharama za kuwafidia wananchi zitafahamika baada ya tathmini hiyo kukamilika.

**Na. 63**

**Upatikanaji wa Mbolea**

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE** aliuliza:-

Kwa kuwa, upatikanaji wa mbolea mara nyingi umekuwa ni tatizo kuwafikia Wakulima kabla ya msimu, hasa Wakulima wa Mkoa wa Kigoma, ambao hali ya hewa ni nzuri na mvua zinanyesha, pia ina rutuba tele:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuhakikisha mbolea inawafikia Wakulima mapema iwezekanavyo?

(b) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwekeza katika kilimo kwa Mkoa wa Kigoma?

(c) Je, Serikali itawasaidiaje Wakulima ambao hawana uwezo wa kupata mbolea?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE.HEZEKIAH N. CHIBULUNJE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula, Ushirika napenda kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Johnson Gezabuke, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula, Ushirika napenda kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Johnson Gezabuke, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kwamba wakulima wanapata mbolea kwa wingi na mapema kabla ya msimu kuanza, Serikali itachukua hatua zifuatazo:-

- Kuyahamasisha Makampuni makubwa ya Kimataifa kuleta mbolea nchini kwa wingi na kuifikisha kwenye maeneo husika ili kuwauzia wakulima mapema. Tayari, Kampuni ya YARA ya Norway ambayo ni muuzaji mkuu wa mbolea katika Soko la Dunia imefungua Ofisi yake Dar es Salaam na imekubali kuleta mbolea kukidhi mahitaji ya Tanzania na nchi jirani.

- Kuzielekeza Kampuni zinazosambaza mbolea nchini kuanza kusafirisha mbolea kwenda mikoani kuanzia mwezi wa Julai kila mwaka kwa lengo la kuzifikisha mbolea hizo kwenye maeneo husika mapema.

- Kutoa mafunzo kwa Mawakala wa Mbolea wa Vijiji juu ya uendeshaji wa biashara ya mbolea pamoja na kuwaelewesha uwezekano wa kutumia huduma za *SACCOS* na Benki zilizopo katika maeneo yao.

(b) Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa Mkoa wa Kigoma unapata mvua za kutosha karibu kila msimu na unayo ardhi ya kutosha inayofaa kwa kilimo. Kwa kutambua hivyo, Serikali imejumuisha Mkoa huo katika Mradi wa Uwekezaji katika Sekta ya Kilimo Wilayani *(District Agricultural Sector Investment Project (DASIP)* utakaoanza kutekelezwa na Serikali kuanzia mwezi Aprili, 2006 kwa ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB).* Mradi ambao utaghamimu shilingi 94.2 bilioni na utatekelezwa katika Mikoa ya Kigoma, Kagera, Mara, Mwanza na Shinyanga. Programu hiyo itasaidia wakulima kuwekeza katika kilimo. Aidha, Serikali itaendelea kutuma fedha kwa Halmashauri Mkoani Kigoma kwa ajili ya mipango ya kuendeleza kilimo ya Wilaya *(District Agricultural Development Plan (DADP).* Ili kutekeleza mipango hiyo.

Katika mwaka 2005/06 Halmashauri katika Mkoa wa Kigoma zimepewa fedha na Serikali Kuu kama ifuatavyo:- Kigoma shilingi 60,277,787, Kasulu shilingi 74,304,106, Kibondo shilingi 55,391,290 na Ujiji shilingi 11,409,091. Aidha, Wizara yangu imetekeleza miradi ya umwagiliaji maji kwa mwaka 2005/2006 iliyogharimu shilingi 4,000,000 kwa Kigoma/Ujiji na shilingi 30,122,000 kwa Kasulu.(c)Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ikishirikiana na Halmashauri za Wilaya itahamasisha kuundwa, kuimarisha na kuvitumia Vyama vya Ushirika na Vyama vya Akiba na Mikopo *(SACCOS)* ili vijiingize katika kutafuta mitaji mikubwa itakayowezesha kununua mbolea nyingi na kisha kuikopesha au kuiuza kwa wanachama wake. (*Makofi)*

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika nina swali moja la nyongeza.

Hivi ni kwa nini Serikali ina kigugumizi gani kuweza kuwakopesha wakulima kama vile inavyowakopesha wafanyabiashara ili wakulima nao waweze kupata maisha bora kutokana na mikopo inayotokana na Serikali?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE):** Mheshimiwa Spika, Serikali haina kigugumizi chochote juu ya kuwakopesha wakulima kama ambavyo wanawakopesha wafanyabiashara.

Nimejibu katika swali la msingi hapa kwamba kazi mojawapo ambayo Serikali inaifanya ni kuelimisha na kuhamasisha wakulima na wanavijiji kwa ujumla ili kuweza kuanzisha Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo ili iwe rahisi wakulima hawa nao kukopesheka kama wafanyabiashara nao wanavyokopesheka. *(Makofi)*

**Na. 64**

**Sensa ya Kilimo na Mifugo**

**MHE. VITA R. KAWAWA** aliuliza:-

Kwa kuwa, mwaka 2003/2004 Tanzania ilifanya sensa ya Kilimo na Mifugo nchi nzima:-

(a) Je, ni lini matokeo ya sensa hiyo yatakamilika?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kucheleweshwa kwa taarifa ya sensa hiyo kwa namna moja au nyingine ni kupoteza fedha nyingi za Serikali?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa,Mbunge wa Namtumbo, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Wizara za sekta ya kilimo ziliipa Ofisi ya Taifa ya Takwimu jukumu la kufanya Sensa ya Kilimo na Mifugo nchini.

Kazi ya Sensa hiyo ilihusisha ukusanyaji wa takwimu za kilimo na mifugo katika Vijiji na mashamba makubwa kutoka kwa wakulima wadogo kwa kutumia sampuli ya Vijiji 3,231 ambavyo vilichaguliwa kutoka kila Wilaya ya Tanzania Bara na sampuli ya maeneo 317 yaliyochaguliwa kutoka Tanzania Zanzibar, ambapo kazi hiyo ilikamilika mwezi Juni 2004. Baada ya kukamilika kwa ukusanyaji wa takwimu, uchambuzi wa Takwimu za Sensa hiyo ulipangwa kufanyika katika awamu mbili kama ifuatavyo:-

- Awamu ya Kwanza iliyohusisha uingizaji wa takwimu katika kompyuta na kutoa majedwali kulingana na mahitaji ya wadau wa sekta ya kilimo ambao ulianza mwezi Julai 2004. Kazi hiyo ilikamilika mwezi Juni, 2005 na takwimu hizo zimeanza kutumiwa na baadhi ya Wadau na Wizara mbalimbali.

- Awamu ya Pili iliyoanza Julai, 2005 inahusisha kazi ya kuandika mihtasari (*Agriculature Sample Census Reports*) inayotokana na Sensa hiyo. Utoaji wa Mihtasari hiyo umekwishaanza ambapo hadi sasa Ofisi ya Taifa ya Takwimu ikishirikiana na Wizara yangu imekwishatoa mhutasari wa Kitaifa kuhusu idadi ya mifugo pamoja na huduma katika Sekta ya Mifugo.

Mihtasari mingine inayotarajiwa kutolewa itahusu kilimo cha mazao pamoja na huduma zake, shughuli za wakulima wadogo katika kaya, upatikanaji wa maliasili na kilimo cha mashamba makubwa. Mihtasari hiyo iko katika hatua mbalimbali za kuandaliwa na inategemewa kuwa ifikapo mwezi Agosti 2006, mihtasari yote itakuwa imekamilika.

Mheshimiwa Spika, kulingana na kumbukumbu za sensa kama hii miaka ya nyuma na hata kwa viwango vya Nchi za Ukanda wa Kusini mwa Jangwa la Sahara, muda uliotumika kati ya ukusanyaji na mwanzo wa takwimu kutumika ni wa kuridhisha; na kwa hiyo taarifa za sensa ya kilimo na mifugo ya 2003/2004 haijacheleweshwa.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyoyatoa. Lakini kwa kuwa amekiri kwamba mihtasari ya kilimo haijatoka swali langu ni je Serikali haioni kucheleweshwa kwa mihtasari hiyo matokeo hayo wakati yanapotoka yatakuwa yamepitwa na wakati?

Pili, kwa kuwa Wilaya ya Namtumbo ni moja ya eneo lililopata mvua nyingi mwaka huu na wananchi wake wamelima mazao mchanganyiko ya chakula na yamekubali. Je, Serikali ina mpango wowote wa kuja kutambua ni kiasi gani ya chakula

kitakachozalishwa ili Idara ya Hifadhi ya Chakula ije kukinunua na kukiuza sehemu zitakazoathirika na chakula mwaka huu?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE):** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza juu ya kuchelewa kwa mihtasari kwamba iwe imepitwa na wakati. Nataka tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika majibu ya msingi nimesema kwamba takwimu zilishakusanywa na sasa hivi kinachoendelea na ile tunayoita *preparation* ni kuandaa takwimu ziwe tayari kwa kutumia.

Mheshimiwa Spika, kwa kawaida takwimu hizi zinazokusanywa kwa njia ya sensa makusudi yake kuweza kutumika kwa muda mrefu na ndiyo maana kutoka kipindi kimoja cha sensa na kingine kutakuwepo na muda hapo katikati ambao unatumia takwimu za sensa iliyotangulia. Kwa hiyo takwimu hizo zitakuwa hazijapitwa na wakati.

Lakini la pili, kuhusu kutambua chakula pamoja na mazao yaliyozalishwa katika Wilaya ya Namtumbo. Nataka nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge ya kwamba hiyo ndiyo kazi ambayo Serikali inaifanya na kazi hii hufanyika karibu kila mwaka. Kipindi kile kabla ya mazao hayajaiva huwa inapitishwa tathmini ya kuangalia hali ya mazao mashambani kuweza kutambua kiasi au kuweza kuleta makadirio ya kiasi cha mazao yatakayozalishwa na hivyo kuweza kutambua mazao yatakayopatikana kwa ajili ya chakula na vile vile yatakayouzwa katika masoko mbalimbali. *(Makofi)*

**Na. 65**

**Ardhi ya Ranchi ya Kalambo**

**MHE. PONSIANO D. NYAMI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Menejimenti ya ranchi ya Kalambo ipo tayari kuwagawia wananchi sehemu ya ardhi wanayodai kabla ya ranchi hiyo haijabinafsishwa. Je, isingekuwa vyema Serikali ikaagiza maeneo hayo yanayomilikiwa na ranchi yagawiwe kwa wananchi, wa Sintali, Nkana na Nkoanchindo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Nyami, Mbunge wa Nkasi naomba nitoe maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mkakati wa kumilikishwa kwa Watanzania baadhi ya maeneo ya Ranchi zilizo chini ya Kampuni ya Ranchi za Taifa (KARATA) umetekelezwa kwa kuzingatia maamuzi ya Serikali kupitia Waraka wa Baraza la Mawaziri Na. 2 wa mwaka 2002. Katika mpango huo lengo la Serikali ilikuwa kuwawezesha Watanzania wenye nia, ari na uwezo wa kuendesha ufugaji wa kibiashara kupata maeneo ya kati ya hekta 1,000 hadi

4,000. Jumla ya hekta 200,275 zilitengwa kwa ajili ya kugawanywa kwenye maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, katika Ranchi zilizogawanywa za Mkata, Dakawa (Morogoro), Mzeri (Tanga), Kalambo (Rukwa), Misenyi, Kikulula, Kagoma, Mabale (Kagera) na Uvinza (Kigoma) hadi sasa jumla ya Ranchi ndogo 124 zimepatikana na kupewa wananchi kwa utaratibu wa matangazo ya zabuni. Ranchi hizo zitakuwa na uwezo wa kuzalisha ng'ombe wapatao 100,000 kwa mwaka. Mpango huu umezihusisha Ranchi zote za *NARCO* kwa Kiingereza au KARATA kwa Kiswahili isipokuwa Ranchi za Kongwa na Ruvu ambazo zitaendelezwa na Serikali kama maeneo mahsusi ya kufuga ng'ombe wa nyama. Ranchi ya West Kilimanjaro haitagawanywa kwa wakati huu kwa vile ina kesi Mahakamani. Baada ya maelezo haya naomba sasa nijibu swali la Mheshimiwa Nyami, Mbunge wa Nkasi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, umilikishwaji wa maeneo ya Ranchi ndogo ndogo katika Ranchi ya Kalambo, ulikamilika tarehe 20 Oktoba, 2004. Zoezi hilo lilitekelezwa kwa kushauriana na Viongozi wa Mkoa wa Rukwa ambapo wananchi walihamasishwa ili waweze kushiriki kikamilifu katika kuomba maeneo ya kuwekeza mara baada ya zoezi la kupima kukamilika. Jumla ya Ranchi ndogo ndogo 13 zilipatikana na zilitangazwa kwenye magazeti ili zibinafsishwe kwa njia ya zabuni.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa taarifa kwamba Ranchi ndogo hizo tayari zimepata wawekezaji baada ya kutuma maombi na kuwasilisha mipango mizuri ya uwekezaji. Aidha, wakati wa utekelezaji wa zoezi hili maombi ya vijiji na vikundi vya wananchi vilipewa nafasi maalum na kipaumbele ili waweze kushiriki katika uzalishaji wa ng'ombe bora kupitia ufugaji wa Ranchi. Kwa hali hiyo, vijiji vya Mbuluma, Sintali na Lolesha vilipewa maeneo katika Ranchi ya Kalambo kama ifuatavyo:-

(i) Kijiji cha Mbuluma walipewa *Block* Na. 55/5 yenye hekta 3,167.40;
(ii) Kijiji cha Sintali walipewa *Block* Na. 55/3 yenye hekta 3,157.71; na
(iii) Kijiji cha Lolesha walipewa *Block* Na. 55/7 yenye hekta 2,562.40.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa maeneo haya ni makubwa vijiji vya jirani kama vile Nkana na Nkoanchindo vinaweza kushirikiana na wenzao katika kuendeleza maeneo haya. Utaratibu huu unaweza kusimamiwa na uongozi wa Mkoa wa Rukwa maadam maeneo haya yaendelezwe kama ilivyokusudiwa yaani kuwawezesha wananchi kutumia maeneo haya kwa kuendeleza ufugaji wa ng'ombe wa nyama kwa kuzingatia ufugaji bora, wa kisasa na wa kibiashara.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi niulize maswali ya nyongeza.

Kwa kuwa mheshimiwa Waziri inaonekana haelewi Jiografia ya shamba hilo la Kalambo na majibu anayoyajibu hapa hata wananchi wanaosikiliza wa vijiji vya Nkana na Nkoanchindo kwanza wanamshangaa anaposema ashirikiane na wananchi wa vijiji vya Mbuluma, Lolesha na Sintali. Na wao waliomba maombi haya mapema na

kutekeleza hayo na mimi mwenyewe nilikuwa nafuatilia. Hamuoni kwamba Serikali imewanyanyasa katika maeneo yao kwa kutokuwapatia eneo hilo na kuanza kuwapa wafanyabiashara wengine?

La pili kwa kuwa tunajua wazi kwamba katika ufugaji mara nyingi wanyama wanaharibu mazingira. Wananchi wanalima kilimo ambacho tunasema ni uti wa mgongo ama ni sekta kiongozi. Kwa nini mmeamua kuwajali wafanyabiashara na kuwaacha wananchi wa Nkana na Nkoanchindo solemba bila kuwapa eneo la kulima?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa anasema Jiografia ya eneo husika silifahamu wakati kusema kweli nalifahamu basi namwomba Mheshimiwa Mbunge Wizara iko tayari kushirikiana naye ili kuweza kuielewa sahihi Jiografia hiyo na kuweza kuishughulikia suala la vijiji alivyovisema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, si kweli kwamba wanyama kama alivyosema Mheshimiwa Nyami akimaanisha mifugo wanaharibu mazingira. Mifugo inaharibu mazingira pale ambapo tu inakuwa imezidi kiwango ambacho mazingira ya eneo lile hayawezi yakabeba idadi ile. Na kwa hali ilivyo kwa sasa katika eneo la Kalambo na vijiji vinavyozunguka hakuna takwimu zinazoonyesha kwamba kuna idadi kubwa ya mifugo ambayo inasababisha uharibifu wa mazingira. *(Makofi)*

**Na. 66**

**Uhitaji wa Elimu ya Watu Wazima**

**MHE. AMINA C. MPAKANJIA** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika kipindi cha miaka ya 1970 hadi 1980 Serikali ilitilia mkazo Elimu ya Watu Wazima, lakini sasa suala hilo halitiliwi mkazo wowote licha ya kwamba, bado elimu hiyo inahitajika sana katika Taifa letu. Je, Serikali ya Awamu ya Nne ina mpango gani madhubuti wa kuifufua elimu hiyo ambayo inahitajika sana kwa jamii ya Watanzania?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa, kipindi cha miaka ya 1970 hadi 1980 Serikali ilitilia mkazo mkubwa Elimu ya Watu Wazima (EWW) wenye lengo la kufuta ujinga wa kutojua Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK). Kiwango cha kujua Kusoma, Kuandika na Kuhesabu kilifikia asilimia 90 mwaka 1986. Kutokana na matatizo mbalimbali yakiwemo ya kiuchumi na kujitoa kwa wafadhili wa mpango huu, kiwango hiki kilishuka hadi asilimia 71 mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekusudia kufufua na kuendeleza EWW kwa kutekeleza Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Walioikosa (MEMKWA) na Mpango wa Uwiano Kati ya Elimu ya Wazima na Jamii (MUKEJA). MEMKWA unawahudumia watoto wa miaka 11 – 14 na vijana wa miaka 15 – 18 ambao walikosa Elimu ya Msingi katika Mfumo rasmi. Utaratibu huu unakusudia kupunguza idadi ya watu wazima wasiojua Kusoma, Kuandika na Kuhesabu. MUKEJA unawahudumia watu wazima wa miaka 19 na zaidi. Aidha, mpango huu unatoa fursa kwa wananchi kujua Kusoma, Kuandika na Kuhesabu na pia kuwaongezea ujuzi na uwezo wa kuendesha kwa ufanisi shughuli zao mbalimbali za kiuchumi. MUKEJA ulianza kwa majaribio mwaka 1996 katika Halmashauri nne (4) ambazo ni Sengerema, Moshi Vijijini, Morogoro Vijijini na Lushoto. Hivi sasa mpango huo upo katika hatua ya kusambazwa katika Halmashauri zote baada ya kuonyesha mafanikio. Mpango huu umefanikiwa kwa kuwa ni shirikishi, unakubalika.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa MEMKWA na MUKEJA utaongeza idadi ya watu wanaojua Kusoma, Kuandika na Kuhesabu. Mipango hii pia itasaidia juhudi za kuondoa umaskini, kufuta ujinga na kujenga mwelekeo sahihi kwa wananchi kuendelea kujielimisha maisha yote (*life long education*).

Mheshimiwa Spika, tunaomba ushirikiano na wadau wote wa elimu wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, Halmashauri, Mashirika yasiyo ya Kiserikali na watu binafsi katika kuifikia azma hii. *(Makofi)*

**MHE. AMINA C. MPAKANJIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri tu, ambayo amenijibu lakini pamoja na hivyo nilikuwa na maswali madogo ya nyongeza. Swali la kwanza, linahusiana na hii elimu ya watu wazima aliyoisema wanaitoa sasa hivi inaitwa MUKEJA, kuanzia watu wenye umri wa miaka 19 na kuendelea lakini ametaja Halmashauri nne tu ambazo mpango huu ulianza mwaka 1996 na amesema kwamba sasa hivi wanatarajia kwenda katika Halamsahauri nyingine.

Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kulihakikishia Bunge lako Tukufu ni lini mpango huu utaanza rasmi ukizingatia katika maeneo mengi sana ya vijijini watu wengi hawajui kusoma na kuandika? Hata mawasiliano tu kwa lugha ya Kiswahili cha kwetu wenyewe imekuwa ni tatizo nadhani hilo mliliona wakati wa kampeni watu wengine ilikuwa inabidi watafsiriwe kwa lugha yao. Tunaomba ufafanunuzi.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni kwamba elimu hii pia imekuwa ikitolewa kidogo sana lakini wamekuwa wakitumia madarasa ya shule za msingi. Sasa Serikali haioni kwamba ni wakati muafaka sasa hivi wa kujenga vituo maalum ama shule maalum za elimu ya watu wazima ili kuepuka ile wazazi kuona aibu kuwa darasa ama shule moja na mtoto ama mjukuu wake?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)**: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba mpango wa MUKEJA umeshaanza na unaendelea na kwamba kwa kuwa orodha ya Halmashauri ambazo zimehusishwa ni ndefu naomba baada ya Bunge hili nimpatie takwimu sahihi Mheshimiwa Mbunge na kwa Mbunge yoyote ambaye atahitaji.

Mheshimiwa Spika, suala la umri wa vijana hawa na kwamba wataona haya kwenda kusoma na hivyo vijengwe vituo, naomba niseme kwamba kwa hivi sasa Serikali ipo katika mpango mkubwa wa kuhakikisha shule zinajengwa; na kwa kuwa baadhi ya shule wanatumia asubuhi na mchana zina nafasi basi watu wazima watatumia. Hata hivyo mpango wa MUKEJA unalenga zaidi vijana na kuwawezesha. Kwa hiyo, mara nyingi haufanyiki mashuleni bali unakwenda kwenye vituo ambavyo wanakuwa pia na shughuli rasmi. Kwa mfano, uchongaji, ufinyazi, ushonaji na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa kusisitiza hilo kwa kuwa Wizara yangu inaongozwa na Ilani Elimu ya watu wazima ni moja ya vitu ilivyopewa kipaumbele naahidi tutatekeleza. (*Makofi*)

**Na. 67**

**Kupanua Elimu ya Sekondari**

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA** aliuliza:-

Je, ni kwa namna gani Serikali inanuia kutimiza lengo lake la kupanua elimu ya sekondari kwa kuongeza nafasi bila kuathiri ubora wa elimu hiyo nchini hasa kutokana na uhaba wa Walimu na vifaa mbalimbali vya kufundushia?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jackson M. Makwetta, Mbunge wa Njombe Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondori MMES mwaka 2004 hadi 2009 inalenga kuongeza nafasi na kuboresha elimu katika shule zote za sekondari za Serikali kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kutoa ruzuku ya maendeleo ili kuchangia nguvu za wananchi kujenga shule za sekondari za kutwa na kuzipatia shule za sekondari za Serikali ruzuku ya uendeshaji kwa ajili ya kununua vitabu na vifaa vingine vya kufundishia na kujifunzia. Pia kuimarisha

usimamizi na uendesheji wa shule hizo. Hapa napenda kuchukua nafasi hii kuishukuru Mamlaka ya Elimu Tanzania kwa kuzipatia shule za sekondari zipatazo 65 vifaa vya maabara kwa kufundisha masomo ya sayansi.

(ii) - Kuongeza ajira ya Walimu kwa kuajiri Walimu waliohitimu katikaVyuo vya Ualimu na Vyuo Vikuu mara wanapomaliza mafunzo.

- Kuongeza nafasi za Stashahada katika Vyuo vya Ualimu vilivyopo ili kuchukua idadi kubwa ya wanachuo.

- Kuajiri wahitimu wa kidato cha sita na Chuo Kikuu wasiyo na taaluma ya Ualimu kama hatua za muda mfupi za kukabalilina na upungufu wa Walimu katika kipindi hiki cha mpito na baadaye kuwapatia mafunzo rasmi ya Ualimu. Kuangalia pia uwezekeno wa namna ya kuwatumia Walimu wastaafu kufundisha katika shule za Sekondari.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hatua nilizozitaja za kuhakikisha kuwa ubora wa elimu hauathiriki Wizara inagharamia mafunzo ya Ualimu kwa kiwango cha Stashahada ya Uzamili na Shahada ya Ualimu katika Vyuo Vikuu vya Dar es Salaam na Tumaini kama mkakati wa muda mrefu.

Vile vile Wizara ina makubaliano na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kuwapa mafunzo ya Ualimu ngazi ya Shahada wanaofundisha kwa kutumia leseni. Wizara pia imekamilisha hatua za awali za mikakati ya kutoa mafunzo endelevu kwa Walimu kazini. Aidha Serikali inaangalia uwezekano wa kuboresha muundo wa utumishi pamoja na ajira ya Walimu kwa kushirikiana na wadau wengine ili Walimu wabakie katika ajira.

Mheshimiwa Spika, kufuatia juhudi hizi zinazochukuliwa na Serikali ni dhahiri kuwa lengo siyo kuongeza nafasi tu bali pia kuinua kiwango cha elimu inayotolewa.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Spika ningependa kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri na jitihada zinazofanywa na Serikali kuboresha elimu.

(a) Kutokana na uhaba wa Walimu suala ambalo ni tatizo la kweli. Je, isingekuwa vizuri Wizara ya Elimu kwa kushirikiana na Wizara ya Utumishi wafanye uchambuzi wa Walimu bora ambao wanakaribia kufastaafu ili wawawekee mikataba ya kuendelea na kazi baada ya kustaafu ili kutatua tatizo hili?

(b) Kwa kuwa lengo la Serikali ni kuwa na shule ya sekondari katika kila kata na kata hizi ni za kiutawala mahali pengine unakuwa na vijiji viwili kwa kata moja. Je, isingekuwa vizuri kwa Wizara ya Elimu kuwa na kata za kielimu ili kuoanisha mipango hii ya ujenzi wa kila kata ya kielimu ambayo itauwiana na kiwango cha wanafunzi

wanaomaliza darasa la saba na kwa sababu Wizara inaweza ikajua hata miaka kumi ijayo ili mipango hii iwe ya kisayansi zaidi?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri aliyoyatoa Naibu Waziri ningependa kumjibu Mheshimiwa Jackson Makwetta kama ifuatavyo:-

Suala la kwanza alitaka kujua kama kuna uwezekano wakuongea na Utumishi ili tuweze kuwaajiri Walimu ambao wako katika umri wa kustaafu ili kukabili uhaba wa Walimu. Ni kweli ushauri wake ni mzuri kwa sababu tayari tumeshaanza kuongea ili kuona uwezekano wa namna ambavyo tunaweza kupata Walimu ambao hasa kwenye shule za *A level*, wale ambao wapo karibu kustaafu ili waweze kuongezewa muda kwa utaratibu wa mkataba. Lakini kama nilivyosema tuko katika hatua ya mazungumzo, lakini ushauri tumeupokea.

Kuhusu suala la pili, pia ni wazo ambalo linahitaji kufanyiwa kazi kwa sababu mpaka sasa hivi wananchi wameshahamasishwa wanajenga shule kwa kadri iwezekanavyo na pia kupata msaada kutoka Serikalini lakini kwa kuwa ni wazo jipya ambalo ametupa yeye, nadhani lina haja ya kufanyiwa kazi. Ahsante sana.*(Makofi)*

## Na. 68

## Uwanja wa Ndege wa Songwe

**MHE. RICHARD SAID NYAULAWA** aliuliza:-

Kwa kuwa, ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Songwe unatarajiwa kukamilika ifikapo 2008 na kwa kuwa uwanja huo unategemewa kuhudumia wananchi wa Wilaya zote za Mkoa wa Mbeya na Rukwa pamoja na maeneo mengine mbalimbali:-

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kujenga barabara za Mbalizi – Ileje, Mbalizi – Mkwajuni kupitia Mchewe, na Isonje - Makete kupitia Igoma kwa kiwango cha lami ili kuharakisha usafiri na usafirishaji kwenda kwenye uwanja huo?

(b) Kama hakuna mpango wa kuzijenga barabara hizo kwa lami. Je, Serikali inaweza kuziimarisha kwa kokoto; na je kazi hiyo itaanza lini?

(c) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba, kama barabara hizo hazikujengwa kuwawezesha viongozi kuwafikia wananchi na kuhamasisha kuzalisha mazao mbalimbali, uwanja huo hautaweza kutumika kikamilifu na kwa muda mrefu baada ya ujenzi kukamilika?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA ABEID DAFTARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Richard Said Nyaulawa Mbunge wa Mbeya Vijijini, kwanza napenda maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara alizozitaja Mheshimiwa Mbunge ni barabara za Mkoa zinazohudumiwa na wakala wa barabara *TANROADS*. Barabara hizo hujulikana kwa majina ya Mbalizi – Shigamba - Isogole km 98.9, Mbalizi – Mkwajuni-Makongolosi Km 116.6, Isonje – Kikondo Km 22.3 kwa upande wa Mkoa wa Mbeya na Kikondo – Makete Km 74.1 kwa upande wa Mkoa wa Iringa.

Barabara hizi zinajumla ya ya urefu wa km 311.8 na zimejengwa kwa kiwango cha changarawe na udongo. Serikali kwa kupitia wakala wa barabara *TANROADS* ime kuwa ikizifanyia barabara hizo matengenezo ya aina mbalimbali kulingana na upatikanaji wa fedha kwenye bajeti ya kila mwaka ili kuzifanya ziendelee kupitika.

Mheshimiwa Spika baada ya kutoa maelezo hayo sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Richard Said Nyaulawa, Mbunge wa Mbeya Vijijini, lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifutavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inaona umuhimu wa kuzijenga barabara zote muhimu kwa kiwango cha lami zikiwemo barabara alizozitaja Mheshimiwa Mbunge isipokuwa kinachokwamisha utekelezaji wa jambo hili ni uwezo wa kifedha kwa kuwa kiasi cha fedha kinachopatikana kwenye bajeti zetu hakitosherezi ujenzi huo kwa kiwango cha lami. Hivyo napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kuzijenga na kuziimarisha kwa kiwango cha changarawe. Hivyo kwa sasa kipaumbele cha juu kimewekwa katika kuzijenga barabara kuu kwanza kwa kiwango cha lami.

(b) Kwa sasa napenda niseme Serikali haina mpango wa kuzitengeneza barabara hizo kwa kiwango cha lami bali namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kuziimarisha kwa kuzifanyia matengenezo ya aina mbalimbali katika kiwango cha changarawe ili barabara hizo ziendelee kupitika wakati wote. Matengenezo ya aina hiyo hufanyika kwa kuzingatia uwezo wa kifedha na aina ya matengenezo yanayohitajika katika sehemu mbalimbali za barabara hizo.

(c) Mheshimiwa Spika, matengenezo yaliyofanyika kila mwaka kama nilivyoeleza hapo awali yamewezesha kuzifanya barabara hizo ziendelee kupitika hivyo viongozi watawafikia wananchi na kuwahamasisha kuhusu uzalishaji wa mazoa mbalimbali na kuweza kuutumia uwanja huo wa Songwe kikamirifu pindi utakapo kamilika.

**MHE. RICHARD SAID NYAULAWA:** Mheshimiwa Spika asante sana. Kwanza nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo ameweza kuyatoa. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Ni kweli kwamba ukarabati huwa unafanyika mara kwa mara katika hizo barabara lakini ukarabati huo mara nyingi unakuwa ni duni sana kiasi ambacho kupitika kwake kila mwaka kunakuwa kwa shida sana kwa hiyo usafiri unakuwa ni wa shida sana. Je, Serikali inaweza kunihakikishia namna gani hizo barabara ukarabati wake unaweza kuwa ni wa hali ya juu kiasi ambacho usafiri na usafirishaji wa mazao unaweza kuwa ni wa uhakika zaidi kuliko ilivyo sasa hivi?

La pili, ili kuweza kufanya matayarisho kwa siku za baadaye nilikuwa nafikiri kwamba uchambuzi yakinifu ungeweza kuanza mapema, kwa sababu kwa hakika uwanja wa ndege hauwezi kuanza kabla barabara hazijawa nzuri. Je Serikali inaweza kunipa taarifa kuhusu uchambuzi yakinifu ambao unastahili kufanyika katika hizo unaweza kuanza lini kama inawezekana?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA ABEID DAFTARI):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali la nyongeza la Mheshimiwa Richard Nyaulawa kama ifuatavyo:-

Napenda nimhakikishie kwamba tutazungumza na tutamfuatilia kwa karibu *Regional Road Engineer* ahakikishe kwamba barabara zile anampa *contractor* ambaye anafaa kufanya kazi ile ipasavyo si hizo tu na nyingine zote ambazo zinatengenezwa kwa changarawe.

Mheshimiwa Spika, muda wote tulikuwa tunasema kwamba ili kiwanja cha ndege kiweze kufanya kazi zake vizuei ni lazima tuboreshe uzalishaji katika maeneo yale na hayo yanasemwa kila leo. Kwa hivyo pale panapohitajika upembuzi yakinifu kwa upande wa Mkoa kuona namna gani watakitumia kiwanja cha ndege cha Mbeya cha Songwe *more efficiently* watafanya hivyo na kwa upande wa barabara hatutasita kufanya hivyo. (*Makofi*)

**Na 69.**

**Hali ya Kivuko cha Buchosa**

**MHE. SAMUEL M. CHITALILO** aliuliza:-

Kwa kuwa hali ya kivuko cha Buchosa kinachotumiwa na wananchi wa Kisiwa cha Kome na Nyakalilo ni mbaya sana kiasi cha kuhatarisha maisha ya watu na mali zao; na kwa kuwa, jambo hilo limekuwa ni kama mazoea kwa kivuko kufanya kazi katika hali ya hatari:-

(a) Je, ni lini Serikali itanunua kivuko kipya kwa sababu kilichopo kinahatarisha maisha ya watu na mali zao, na ni hatua zipi zimekwisha chukuliwa hapo awali?

(b) Je, kwa nini kivuko kilichokuwepo awali na kuondolewa kwa ajili ya matengenezo hakijarudishwa?

(c) Je, Serikali ipo tayari kulipa fidia ya watu waliopoteza maisha na mali zao baada ya kivuko hicho kushindwa kufanya kazi na kusababisha wananchi kutumia mitumbwi ya kawaida?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA ABEID DAFTARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Samuel Chitalilo, Mbunge wa Buchosa, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Pantoni ya *MV Kome* inayotoa huduma katika kivuko cha Buchosa kati ya kisiwa cha Kome na Nyakalilo ilinunuliwa na Serikali mwaka 1972. Pantoni hii yenye ukubwa wa tani 20 ina uwezo wa kubeba magari matatu na abiria 50 kwa mara moja. Pantoni inaendeshwa kwa *engine* mbili zenye *Horse Power* 50 kila moja.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Samuel Chitalilo, Mbunge wa Buchosa, lenye sehemu (a) , (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali ina mpango wa kununua vivuko vipya saba ikiwa ni pamoja na kivuko cha Buchosa. Vivuko hivi vitanunuliwa kwa awamu kwa muda wa miaka mitano. Kivuko kipya cha Buchosa kitanunuliwa kwenye Bajeti ya mwaka wa fedha 2007/2008 na kitakuwa na uwezo wa kubeba tani 50.

(b) Pantoni ya *Mv Geita* iliyokuwa inatoa huduma pamoja na Pantoni ya *MV Kome* katika kivuko cha Buchosa iliondolewa mwezi Desemba 2004 na kupelekwa Mwanza ili kufanyiwa matengenezo makubwa. Baada ya matengenenzo kukamilika Pantoni hii itarejeshwa kutoa huduma kati ya Nyakalilo na Kome. Tunategemea matengenezo hayo yatakamilika mwezi Juni mwaka huu 2006.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali haiwezi kufidia watu waliopoteza maisha na mali zao baada mitumbwi binafsi kupinduka kwa kuwa kivuko cha Serikali hakikuhusika katika ajali hiyo.

**Na. 70**

**Jengo la Polisi Bumbwini**

**MHE. COL. FETEH SAAD MGENI** aliuliza:-

Kwa kuwa, mwaka 2002 niliuliza Serikali juu ya hali ya mbaya ya Jengo la Polisi lililoko Bumbwini huko Unguja, na Serikali kupitia Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi wa wakati ule iliahidi kulifanyia ukarabati katika mwaka wa fedha wa 2003/2004 lakini hadi sasa hakuna kilichofanyika:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba hali ya jengo hilo sasa inahatarisha maisha ya wapiganaji wetu?

(b) Je kama jengo hilo likianguka na kuhatarisha maisha ya Askari na au kusababisha kupotea kwa maisha ya Askari ni nani atawajibika?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia, naomba kujibu swali Mheshimiwa Col. Feteh Saad Mgeni, Mbunge wa Bumbwini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba jengo la Kituo cha Polisi cha Bumbwini liko katika hali mbaya kwani jengo hilo ni la zamani kama yalivyo baadhi ya majengo mengine ya vituo vya Polisi chini. Jengo hilo halijaweza kufanyiwa ukaratiba kutokana na ufinyu wa bajeti. Hata hivyo Serikali ina mpango wa kuboresha vituo vya Polisi hapa nchini kikiwemo kituo cha Polisi Bumbwini.

(b) Mheshimiwa Spika, ni jukumu la Serikali kuhakikisha kwamba watumishi wake wakiwemo Askari Polisi wanafanya kazi katika mazingira bora. Hivyo Serikali kupitia Jeshi la Polisi inachukua kila jitihada kuhakikisha kuwa jengo hilo la kituo cha Bumbwini linakuwa salama ili lisihatarishe maisha ya Askari wetu.

**MHE. COL. FETEH SAAD MGENI:** Mheshimiwa Spika, nimefurashwa sana na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri yamenipa moyo. Lakini nina swali moja dogo, kutokana na hali ya jengo ilivyo je, Mheshimiwa Waziri asingeona vyema wale vijana kwa wakati huu wakatolewa mule na wakatafutiwa mahali pengine?

Lakini la pili ni kwamba, nitafarijika mimi na wewe Mheshimiwa Spika pamoja na Wananchi wangu wa Jimbo la Bumbwini endapo Mheshimiwa Waziri atanidhibitishia katika Bunge hili kwamba katika Bajeti ya mwaka huu 2006/2007 kama jengo hilo litashughulikiwa.

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Feteh Mgeni anajua nimetembelea kituo kile na kukiona hali yake na kwa sababu tulishauriana sana na Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Kaskazini Unguja kwa nia ya kutafuta mahala pengine hasa kwa kujenga kituo ambapo patakidhi haja zaidi kuliko ilivyo hivi sasa.

Kwa wakati huu tunapatumia kwa muda, namwomba Mheshimiwa Mbunge atupe subra zaidi. Lakini napenda kumhakikishia kwamba katika Bajeti ya mwaka huu kituo kile tutakifanyia *repair* lakini kubwa ni kujenga kituo kipya.

**Na. 71**

**Kigezo cha Urefu kwa Jeshi la Polisi**

**MHE. ALI JUMA HAJI** aliuliza:-

Kwa kuwa moja ya vigezo vinavyotumika katika kuajiri askari wa Jeshi la Polisi ukiacha elimu basi ni urefu wa mtu:-

(a) Je, ni jambo gani la msingi linalopelekea kuzingatia zaidi urefu wa mtu katika Jeshi hilo?

(b) Je, Serikali haioni kwamba, kuchukuliwa vijana warefu tu kwa kigezo ambacho hakieleweki kimsingi ni kuwanyima haki ya msingi ya kupata ajira wale vijana ambao ni wafupi?

(c) Je, Serikali haioni kwamba ipo haja ya kuondoa sharti hilo na badala yake pasiwe na ubaguzi wa urefu na ufupi wa mtu?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ali Juma Haji, Mbunge wa Chaani, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, sharti la urefu kwa wanaojiunga na Jeshi la Polisi, ni kwa mujibu wa Kanuni ya Jeshi la Polisi yaani *Police General Orders No. 54.* Aidha msingi wa kuzingatia kanuni hii ya urefu wa mtu katika Jeshi la Polisi ni kuweza kumudu na kudhibiti vyema mhalifu, mtazamo ambao siyo tu kwa Tanzania bali ni mtazamo wa Kimataifa.

(b) Mheshimiwa Spika, sharti la kuchukuliwa vijana warefu katika Jeshi la Polisi haliwanyimi haki ya msingi ya kupata ajira vijana wafupi, kwani hao huchukuliwa kwa ajili ya kufanya kazi maalum ndani ya Jeshi hilo zisizohitaji kigezo cha urefu. Mifano ipo ya askari wa vyeo mbalimbali ambao ni wafupi, ikiwa ni pamoja na Makamishna.

(c) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika sehemu (b) hakuna ubaguzi wowote kwani hata vijana wafupi wanaajiriwa katika Jeshi na kupanda vyeo kama askari wengine.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Spika, baada ya majibu mazuri sana na Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali moja tu la nyongeza. Kwa mujibu wa maelezo yake inaonesha watu wafupi hawakubaliki Polisi. Sasa je, Uphilipino kwenye wafupi kabisa hakuna Polisi huko?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, ni kwamba katika nchi uliyotaja pia werefu wapo lakini nataka nimhakikishie kwamba katika kipindi hiki, hawa Askari wanaotoka mafunzoni Askari 249 ni wafupi na wameajiriwa kutoka Mikoa mbalimbali kwa hiyo halipo tatizo hilo.

**Na. 72**

**Kuchelewesha Malipo ya Pensheni**

**MHE. MWANNE ISMAILY MCHEMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa kuna malalamiko ya watu walioitumikia Serikali kutolipwa pensheni zao kwa muda unaotakiwa hasa mfanyakazi husika anapofariki, na kwa kuwa, mara nyingi watu huambiwa mafaili yao yamepotea au hayaonekani na Serikali imekua ikisema kuwa jambo hilo litashughulikiwa:-

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuunda Tume ya Wataalam ili kushughulikia jambo hilo na kuleta mapendekezo ya kudumu?

(b) Je, Serikali iko tayari kuruhusu Wabunge kuorodhesha watu wote wenye matatizo ya pensheni katika majimbo yao, Halmashauri au Wilaya zao ili yashughulikiwe?

(c) Je, Serikali haioni umuhimu wa kupeleka ufagio wa chuma katika kitengo hicho muhimu cha pensheni au mpango wa dharura katika Wizara zote?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwanne Ismaily Mchemba, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, upungufu na ucheleweshaji wa kumbukumbu kutoka kwa mwajiri ndiyo sababu kubwa ya ucheleweshaji wa malipo ya mafao ya mstaafu. Masuala yafuatayo hayana budi kukamilishwa na mwajiri pamoja na mtumishi mwenyewe ili malipo yake yalipwe kwa wakati wake:-

(a) Mtumishi hana budi kutoa taarifa kwa mwajiri wake akimjulisha azma yake ya kustaafu miezi sita kabla ya tarehe ya kustaafu.

(b) Mwajiri anatakiwa awasilishe Hazina majalada ya mstaafu mtarajiwa miezi mitatu kabla ya tarehe ya kustaafu ikiwa na kumbukumbu zote muhimu.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa Serikali haijaona umuhimu wa kuunda Tume ya Wataalam kushughulikia matatizo ya pensheni kwa kuwa yanajulikana na yamekuwa yakitafutiwa ufumbuzi. Baada ya kuanzisha Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma na kuhamishia malipo ya wastaafu huko Hazina sasa inashughulikia malipo ya mirathi ya waliofariki siku nyingi, miaka mitano na zaidi kabla Mfuko huo haujaanza kulipa mafao. Tunawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwamba, tayari wamekuwa wakituletea malalamiko ya wastaafu/warithi katika Majimbo yao. Hivyo Waheshimiwa Wabunge wanaweza kuorodhesha wote walio na matatizo ya pensheni na kuwasilisha Hazina ili mradi wanahakikisha kuwa kumbukumbu zote zinapatikana kabla ya kuyawasilisha.

Mheshimiwa Spika, mchakato wa kuandaa malipo ya mirathi unahusu ndugu/ familia ya merehemu ambao wanawajibika kufungua mirathi mahakamani; mwajiri wake naye anawajibika kuandaa nyaraka zote zinazohusika na kuzituma Wizara ya Fedha au Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa Umma. Hivyo, mwajiri, mstaafu/ wategemezi na Hazina wote wanawajibika katika mchakato huo. Kwa kuwa mchakato huo hauhusu Hazina peke yake suluhisho siyo kupitisha ufagio wa chuma katika kitengo cha pensheni bali jambo muhimu ni kila mmoja kufahamu wajibu wake na kuutekeleza ipasavyo.

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwa kuwa tatizo hili la kuandaa malipo ya wastaafu limekuwa sugu. Je, Serikali haiwezi ikaweka utaratibu wa kudumu na kuhakisha kwamba taarifa za wastaafu wote zinawekwa kwenye mtandao ili wakati ukifika sio mstaafu atoe taarifa bali Serikali imtaarifu na malipo yake aweze kulipwa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Spika, ushauri tunaupokea tutautazama.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ni kwamba utaratibu wa sasa ni kwamba Serikali inawaandikia wale ambao wanatarajia kustaafu kabla ili waweze kuelewa muda gani wao wanastaafu. Kwa hivyo taarifa kamili zinatolewa kwa wale ambao wanatarajia kustaafu.

Na. 73

**Utendaji wa *TBS***

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA** aliuliza:-

Kwa kuwa, kuna uuzaji wa vyakula na vinywaji ambavyo muda wake wa matumizi umekwisha, na kwa kuwa jukumu la kupitisha ubora wa vyakula hivyo ni la *TBS*:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba kuna kasoro za kiutendaji ndani ya *TBS*?

(b) Je, Serikali inasema nini juuu ya athari za matumizi ya vyakula hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Anastazia Wambura, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na ( c) kama ifuatavyo:-

(a) Shirika la Viwango Tanzania (*TBS*) limefanikiwa kuweka utaratibu unaoeleweka na kutambulika hapa nchini wa kusimamia viwango kwa mujibu wa Sheria. Kwa upande wa bidhaa zinazotengenezwa nchini, usimamiaji wa viwango, vikiwemo vyakula na vinywaji, hufanyika kwa kumpatia leseni ya kutumia alama ya ubora ta *TBS* mtengenezaji wa vyakula na vinywaji.

Kabla ya kupatiwa leseni hiyo, sharti bidhaa zipimwe na kukidhi matakwa ya viwango hivyo, ikiwemo tarehe na muda wake wa kutumia.

Aidha, *TBS* hufanya ukaguzi wa ghafla katika viwanda bila taarifa kwa mtengenezaji (*surveillance inspection*) na pia hununua bidhaa kutoka madukani (*market surveillance*) na kuona kama bidhaa hizo zimefikia matakwa ya kiwango husika. Iwapo kuna tatizo la bidhaa hizo kupitiliza muda wake wa kutumika, *TBS* kwa kuwasiliana na mamlaka ya Chakula na Dawa (*TFDA*) huhakikisha kwamba bidhaa ambazo muda wake wa kutumika umekwisha au ni duni zimeondolewa madukani.

Aidha ni wajibu wa mlaji kuhakikisha bidhaa anayonunua imetimiza masharti ya viwango na tarehe za mwisho za kutumika na kutoa taarifa kwa vyombo husika anapoona taratibu zinakiukwa ili hatua dhidi ya wahusika zichukuliwe.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kuhusu bidhaa zinazoagizwa kutoka nje ya nchi, *Tanzania Bureau of Standards* na *TRA* pamoja na Idara ya Forodha kwa pamoja huzipima bidhaa hizo. Ikiwa zimefikia matakwa ya viwango, *TBS* huziruhusu kuingia nchini kwa kutumia Sheria ya *Import Regulations* ya Mwaka 1998 kwa kutoa cheti maalum *(Batch Certificate)*. Cheti hiki ni kwa kila shehena inayoingizwa nchini.

Mheshimiwa Spika, tarehe ya mwisho ya matumizi ya chakula au kinywaji haina maana kwamba yatakuwemo madhara ya kiafya kwa mtumiaji. Ukweli ni kwamba baada ya tarehe hiyo inawezekana ladha ikawa tofauti na ile ya awali, ndiyo sababu

watengenezaji wengine badala ya kuandika *expiry date*, huandika *best before a certain date.* Hizi zote zikiwa ni lugha za kibiashara na zinakubalika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utafiti uliofanywa na Serikali ili kugundua ubora na udhaifu wa vifaa au vyombo vinavyotumika kutayarisha na kuhifadhia vyakula na vinywaji, ni kwamba, *TBS* inapofanya ukaguzi wa awali *(pre-realization inspection)*, pia inaangalia ubora wa vifaa na vyombo hivyo kwani ni moja ya matakwa ya viwango vya bidhaa husika. Viwango hivyo huelezea wazi vifaa, vyombo na mazingira ya kutengeneza chakula na vinywaji *(code of hygiene)*.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha. Ni bahati mbaya pamoja na jitihada limebaki swali moja. Namwomba Mheshimiwa Ramadhani Athumani Maneno avumilie kama akipenda tunaweza kuliorodhesha kwenye shughuli za kikao cha kesho.

Matangazo:- Tangazo la kwanza linahusu Waheshimiwa Wabunge kuomba kutembelea ukumbi mpya unaokamilishwa. Naomba sana msubiri tuwapeni utaratibu. Sasa hivi wajenzi na *Consultant* wako katika hatua nyeti sana ya kuweka baadhi ya vifaa.

Kwa hiyo, watu wakiwa wanakwenda bila mpango inaweza kuwa ni shida. Kwa maana hiyo nawaomba wenzetu wa Kamati ya Maadili waliotaka kutembelea saa Tano, wajenzi hawako tayari kwa saa hizo, ndiyo maana inabidi tuelewane kuhusu hilo. Tutafanya mpango Waheshimiwa Wabunge wote wanaotaka kuuona Ukumbi, watauona tu.

Lakini msubiri utaratibu tutakaopanga. Kwa taarifa tu, kabla ya ukumbi ule kutumika, Waheshimiwa Wabunge tutawaomba mtangulie siku nne, kutakuwa na semina, maanake mambo ya mle ni tofauti kabisa na haya mnayoyaona hapa. *(Kicheko)*

Tangazo la pili; saa 6.00 nitampisha Mheshimiwa Jenista J. Mhagama – *Presiding Oficer*. Nimeona nitangaze kwa sababu ningefanya ghafla mngedhani labda Mheshimiwa Spika anajaribu kwenda kurekebisha tai kwa ujanja kumbe sivyo.

Kwenye kazi hii inakubidi mtu kuvumilia saa nyingi sana bila kuwa na visingizio vya kwenda kurekebisha tai. Kwa hiyo, ni utaratibu wangu tu wa kujaribu kuwazoesha wenzetu ambao watakuwa wanakaa kwenye kiti hiki na kama mnavyofahamu mwezi wa sita tutakuwa na kikao kirefu sana na kwa hiyo ni vizuri wawe wameanza anza kuzoea ili tusaidiane kwenye kikao cha Bajeti.

Waheshimiwa Wabunge, tumeanza na Jenista J. Mhagama kwa sababu ni utaratibu kwamba tunaheshimu akina mama. Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, tutafanya utaratibu kesho ama kesho kutwa. *(Makofi)*

Wajumbe wa Kamati ya Utekelezaji ya *UPNAC* wakutane saa 9.00 chumba namba 133 jengo la Utawala.

Waheshimiwa Wabunge wote wa Mkoa wa Lindi wa aina zote, ndiyo, Wabunge wa Majimbo, Wabunge wa Viti Maalum na Wa Kuteuliwa. Kwa hiyo, wote wanaotoka Mkoa wa Lindi kwa maana hiyo, wabaki mara shughuli za Bunge zikisitishwa asubuhi hii. Kuna Mkutano muhimu sana.

Kamati ya Fedha na Uchumi, ikutane saa 5.00 leo chumba namba 219 ghorofa ya pili jengo la Utawala. Kamati ya Bunge ya Kilimo na Ushirika, na hapa nitamke tu; kutakuwa na kikao cha Kamati ya Kanuni ambacho nimeitisha, kiondoe utata uliopo hivi sasa.

Majina ya Wizara yamebadilika, kwa hiyo baadhi ya Kamati zinagongana katika kusimamia shughuli za sekta. Kamati ya Kanuni itauondoa utata huo kabla ya kikao cha Bajeti. Kwa sasa tuvumilie hivyo hivyo. Kwa hiyo Kamati inayoshughulika na Kilimo na Ushirika itakuwa na kikao saa 5.00 leo asubuhi chumba namba 423.

Mwisho Kamati ya Huduma za Jamii itakutana leo saa 5.00 asubuhi chumba namba 231 ghorofa ya pili jengo la Utawala. Katibu!

## KAULI ZA MAWAZIRI

## MABADILIKO YA MITAALA YA ELIMU YA MSINGI NA SEKONDARI

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge watakumbuka kuwa Serikali ilifanye mabadiliko ya Mitaala ya Elimu ya Sekondari Mwaka 2004. Mabadiliko hayo yalipunguza idadi ya masomo kwa kufuta michepuo ya Ufundi, Biashara, Kilimo na Sayansi Kimu na kuunganisha Somo la Fizikia na Somo la Kemia kuwa Somo moja la *Physics With Chemistry* kwa Shule za Sekondari. Aidha, masomo ya Jiografia, Historia na Uraia kwa Shule za Msingi yaliendelea kuunganishwa na kufundishwa kama somo moja la Maarifa ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, tangu mabadiliko haya yalipotangazwa, wadau mbali mbali wakiwemo Chama cha Mameneja na Wamiliki wa Shule na Vyuo visivyo vya Serikali *(TAMANGSCO)*, Chama cha Walimu Tanzania *(CWT)*, Wanafunzi wa Shule za Sekondari; kwa kupitia vyombo vya habari, risala na matamko katika nyakati mbali mbali, wameonesha kutoridhika na mabadiliko hayo ya Mitaala. Aidha, wazazi wengi na wananchi kwa ujumla walionesha kutokubaliana na mitaala iliyobadilishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imetafakari kwa makini suala hili na kwa kuzingatia uzito wa malalamiko hayo, Serikali imeamua kama ifuatavyo kuhusu Mtaala wa Elimu ya Msingi:-

Mtaala utarejea kwenye utaratibu wa zamani wa kutenganisha Somo la Maarifa ya Jamii kuwa Masomo matatu yaani Historia, Jiografia na Uraia. Uamuzi huu utaanza kutekelezwa na masomo hayo kuanza kufundishwa kuanzia Januari 2007. Aidha kwa Mtaala wa Elimu ya Sekondari, Serikali pia imeamua yafuatayo:Kurejesha masomo ya Michepuo yaani Ufundi, Biashara, Kilimo na Sayansi Kimu. Uamuzi huu uanze kutekelezwa na masomo hayo yaanze kufundishwa kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza kuanzia mwezi huu wa Aprili 2006 kwa kutumia Mihutasari iliyopo. Pia kutenganisha Somo la *Physics with Chemistry* ili lifundishwe kama zamani yakiwa masomo mawili tofauti yaani *Fizikia* peke yake na K*emia* peke yake kuanzia mwezi huu wa Aprili 2006 kwa kutumia mihutasari iliyokuwepo kabla ya mabadiliko ya mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, katika kuhitimisha tamko hili, naomba kuchukua fursa hii kuwaeleza Waheshimiwa Wabunge kuwa maamuzi haya ya Serikali yamezingatia kuwaandaa wanafunzi wa Elimu ya Msingi na Sekondari ili kukabiliana na changamoto zifuatazo: Soko huria, Dunia ya Utandawazi, Mahitaji ya Sayansi na Teknolojia, Falsafa ya Elimu ya Kujitegemea, Ajira katika Sekta binafsi na Sekta isiyo rasmi, mahitaji na matakwa ya jamii kwa wakati huu na kuhuisha masomo ya taaluma na mafunzo ya ufundi. Aidha, maamuzi haya ya Serikali yamezingatia pia kuweka msingi bora wa Taaluma unaounganisha kwa ufanisi zaidi masomo kuanzia ngazi ya Elimu ya Msingi, Sekondari na Elimu ya Juu ili kutoa Wataalam walibobea kama inavyolenga Dira ya Taifa ya 2025.Serikali inawashukuru sana wadau mbali mbali waliowezesha kufikia maamuzi haya yanayolenga kutoa elimu bora kwa manufaa ya Taifa letu kwa wakati muafaka. Kwa kupitia Bunge letu, napenda kuwahakikishia wananchi kwamba Wizara yangu kwa kutumia ushirikishwaji wa dhati wa wadau chini ya Falsafa ya Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya, itakuwa tayari kupokea maoni yanayoelekeza katika kuboresha Elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge bila shaka mtakubaliana nami kwamba Mheshimiwa Waziri huyu ni mmoja wa wale Mawaziri ambao wanaenda na Kasi ya Awamu ya Nne. Sasa, kwa sababu Tamko hili limepokelewa vizuri kiasi hiki, nadhani ni vizuri Waheshimiwa Wabunge wapate nakala. Kwa hiyo namuagiza Katibu atoe nakala za kutosha kwa Waheshimiwa Wabunge wote ili wawe na Tamko lenyewe kama lilivyo. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Tunaendelea. Katibu endelea na *Order Paper.*

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Benki Kuu wa Mwaka 2006

*(The Bank of Tanzania Bill 2006)*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa, nilikuwa na wachangiaji kumi na ilikuwa atangulie Dr. Lucy S. Nkya. Lakini kwa sababu ya kazi maalum ambayo Mheshimiwa Mhagama ataifanya, ningeomba wengine wawe na subira, aanze yeye. Kwa hiyo, namwita sasa Mheshimiwa Jenista J. Mhagama ambaye ndiye atafuatiwa na Dr. Lucy S. Nkya.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika,…

**SPIKA:** Nadhani Mheshimiwa Mhagama ungesubiri kwanza, kwa sababu Waheshimiwa Wabunge wengi wanakwenda kwenye Kamati zao na kukatiza katiza tutakuwa tunavunja Kanuni.

*(Hapa Wabunge wa Kamati mbali mbali za Bunge walikuwa wanatoka ukumbini kwenda kwenye shughuli maalum za Kamati)*

**SPIKA:** Nadhani sasa tuna utulivu wa kutosha. Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, unaweza kuendelea. Kuna ombi maaluim la Mheshimiwa Suzan Lyimo ambaye anakwenda kwenye shughuli maalum za Kamati, ajiandae ili afuatie.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza ya kuchangia. Lakini naomba nikushukuru kwa kutamka rasmi kwamba leo nitaanza kwa mara ya kwanza kufanya zoezi rasmi la kuongoza Vikao vya Bunge. Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na shukrani hizo, naomba nichukue nafasi nyingine kuipongeza sana Serikali yetu ya Awamu ya Nne kwa kutimiza Siku 100 ikiwa na sura ya mwelekeo wa Kasi Mpya, Ari Mpya na Nguvu Mpya. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri wote na Serikali nzima kwa ujumla. Ni kwamba naunga mkono hoja iliyoko mbele yangu na niseme kwamba ninapounga mkono hoja hii, tunakubali kwamba ili kuendelea ni lazima mabadiliko yafanyike na wenzetu Wazungu wanasema *Development involve Changes*. Lakini, *changes* zinapotokea ama mabadiliko haya yanapofanyika yanakuwa na utaratibu wake na katika utaratibu huo sina maneno sana katika Muswada wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ninakubali kwamba yale ambayo Waheshimiwa Wabunge wenzangu wamekuwa wakiyazungumza wiki nzima iliyopita, ni mambo ya kimsingi kabisa, ukizingatia kwamba tunapoishauri Serikali kuangalia umuhimu wa kuwa na mipaka ya uhuru wa kiutendaji wa Benki Kuu, ni suala la Msingi sana. Tunasema ni suala la msingi kwa sababu uhuru ukizidi mipaka kwa kweli utekelezaji wake unakuwa hafifu na unakuwa hati hati na matokeo yake unaweza ukaleta matatizo makubwa katika nchi yetu.

Lakini, nikubaliane na ushauri uliotolewa na Wabunge katika maeneo mbali mbali na hasa katika kipengele cha Manaibu Gavana na ukizingatia kwamba Waheshimiwa Wabunge wameomba sana angalau pamoja na *qualification*, mmoja kati

ya wasaidizi hao awe mwanamke, na mimi naomba niunge mkono ukizingatia na mimi ni mwanamke pia.

Mheshimiwa Spika, mimi wakati nikiwa nasoma toka nikiwa katika ile shule ya awali kabisa wengine wamezoea kuita shule ya wadudu ama sijui shule ya awali. Toka kipindi niko katika shule hiyo, nilikuwa naelewa na nimejifunza sana kwamba ili tuendelee ni lazima tuwe na vitu vinne. Kwanza, tuwe na ardhi, lakini tuwe na watu, vile vile tuwe na siasa safi halafu tuwe na uongozi bora. Kwa hiyo, mimi toka nikiwa nasoma, hayo mambo yamekuwa katika akili yangu na tulikuwa tunaimba, hata katika vyombo vya habari "ili tuendelee lazima tuwe na vitu hivyo vinne".

Mheshimiwa Spika, lakini mimi nasema kwamba toka tulikotoka hivi vitu vinne ni lazima sasa vibadilike kuendana na wakati na kuendana na mabadiliko ya Dunia. Sasa nadhani leo tuongeze na kitu cha tano. "Ili tuendelee tuwe na ardhi, watu, siasa safi, uongozi bora, lakini tuwe pia na fedha ili tukiwa na fedha ndiyo tutaendana na mabadiliko na maendeleo yanayotokea katika ulimwengu huu wa sasa.

Mheshimiwa Spika, ardhi tunayo na wote tunajua katika ardhi tuna raslimali kubwa sana. Tuna madini, tuna mali asili, Kilimo kinategemea ardhi. Sasa basi, Serikali yetu kwa muda mrefu imekuwa ikiweka mikakati mbali mbali ya kuoanisha vyombo vya fedha na mpango huu wa ardhi ili nchi yetu ya Tanzania iweze kuendelea. Nakumbuka tumepitisha hapa Mkakati wa Kurasimisha Ardhi kwa Maendeleo ya Watanzania (MKURABITA).

Katika Mpango wa MKURABITA, kadri ninavyoelewa na taarifa nilizo nazo mpaka sasa, katika Mpango wa MKURABITA ili kweli MKURABITA usaidie suala zima la kuwasaidia Watanzania kuondokana na umaskini, mambo mawili makubwa yameanza kufanyiwa kazi ingawa katika Sekta Mtambuka na Kuhusisha Wizara mbali mbali.

Mheshimiwa Spika, la kwanza ilikuwa ni kuhakikisha kwamba ardhi inarasimishwa. Watanzania wanathaminishwa ardhi walizonazo katika thamani ili waweze kukopa. Lakini vile vile Wizara ya Mambo ya Ndani inafanyia kazi suala la Msingi sana la kuwa na vitambulisho vya Uraia katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nasema kwamba, kama tayari Mtanzania akishaweza kutathmini ardhi aliyo nayo na kupata hati ya miliki na ikawa *computerised at the same time* upande mwingine Wizara ya Mambo ya Ndani ikatambua uraia ama ikamtambua Mtanzania huyu akawa na kitambulisho akajulikana kwamba ardhi yake imeisha rasimishwa na iko *computerised* na huku picha na *data bills* zote za kila kitu viko sawa sawa, hapo sasa mimi nataka katika mabadiliko haya ya huu Muswada *BOT* ndiyo ingie katikati, Benki Kuu ndiyo ianze kutizama. Ifanye nini?

Itengeneze sasa hapo Sera itakayoweza kuoanisha suala la Mtanzania kujulikana kama ni raia wa nchi hii, akimiliki ardhi ambayo inaeleweka, sasa *BOT* itengeneze sera

ya vyombo vya fedha ili Watanzania waweze kukopa kwa kurasimisha ardhi yao ndani ya mkakati wa MKURABITA na hivyo waweze kukopeshwa fedha zitakazowasaidia kupambana na umaskini na kuendana na malengo ya MKUKUTA ambayo tumejiwekea.

Mheshimiwa Spika, nimesema kwa kupitia ardhi kama nilivyosema mwanzo, kuna madini, kuna mali asili n.k. Kwa hiyo, tutawaona Watanzania wanarasimisha vipi ardhi hiyo kulingana na namna inavyowezekana. Lakini, niingie katika ajenda ya pili ya ili tuendelee tunahitaji vitu vinne, nimezungumza ardhi, sasa nakuja kwenye watu.

Mheshimiwa Spika, watu tunao. Watanzania tunao na idadi ya watu tayari tumeishafika huko milioni ngapi kadri ya sensa ya taifa inavyosema. Sasa watu hawa wakoje? Wako tayari kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, leo nimesema nimeomba ili tuendelee tunaongeza kitu cha tano baada ya ardhi kwa sababu siasa safi tunayo, siasa ya Chama Cha Mapinduzi. Safi kabisa tunayo. Uongozi bora tunao. Serikali ya Awamu ya Nne imeishadhihirisha uongozi bora, hakuna Matata. Lakini tumesema kwamba watu tunao lakini sasa katika siasa safi, uongozi bora sasa tuangalie hawa watu wanafananaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nasema tunapozungumzia suala zima la kuwasaidia Watanzania na hasa kuieleza Benki Kuu kama chombo kinachodhibiti mwenendo mzima wa fedha na leo mimi nimeongeza hicho kitu cha tano fedha ndiyo msingi mwingine mkubwa wa maendeleo, tunafanya nini? Watanzania wengi wanazifikia *SACCOS* peke yake kule vijijini na kuweza kupata mitaji kwa maendeleo yao ya kila siku.

Mheshimniwa, Spika, *SACCOS* ndiyo chombo pekee kwa Watanzania ambacho kina riba nafuu na kina masharti yanayofikika ukilinganisha na hayo Mabenki na vitu vingine.

Lakini, Mabenki hayo makubwa ambayo yanasimamiwa na Benki Kuu, tumeona kabisa kwamba riba na masharti yake ni magumu sana na hayatekelezeki.

Sasa ni lazima tutafute dawa na tumwombe Gavana anapopewa uhuru wa kuendesha chombo hiki atafute dawa ya kusaidia vyombo hivi vya asasi za fedha vya kati vinavyofikika na Watanzania wengi na hasa wakulima na wakulima wangu wale wa Jimbo la Peramiho ambako mvua zinanyesha mwaka mzima bila matatizo. Wanawezaje wakaingia kwenye suala la fedha kama kitu kingine cha msingi cha kuwaletea maendeleo.

Sasa, hapo ni lazima kuangalia, mimi nafikiri kwamba baada ya kuwa na mabadiliko ya sera za fedha katika nchi yetu ya Tanzania kumeingiza vyombo vingi katika mfumo huria vinavyofanya biashara ya fedha na vinachukua kigezo cha umaskini wa Watanzania ili kuendesha shughuli zao, lakini si kwa kuwasaidia Watanzania, ni kwa kuwaumiza Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri sasa tujiulize, nini kifanyike? Kama Benki Kuu ndiyo yenye dhamana ya kusimamia vyombo hivyo vyote vya fedha. Sasa tuone

tunasaidianaje na Benki Kuu ili kuweza kuwasaidia Watatnzania hao Maskini ambao *SACCOS* ndiyo chombo cha pekee kabisa mpaka sasa hivi kinacho fikika, kiko kwenye nyumba zao katika maeneo yao ya uzalishaji kule wanakoishi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Benki Kuu isaidie kuziinua hizo asasi za kati za fedha kwa namna yoyote inavyowezekana na ninaomba ijitahidi kuzifanya asasi hizo ziwe na viwango vyenye ubora katika kufanya kazi. Viingie katika mfumo wa *best practice* kama vinavvyofanya hivyo vyombo vingine vya fedha vya juu, Mabenki hayo ambayo tunayasema. Benki Kuu ikifanya hivyo itakuwa inawasaidia sana Watanzania.

Mheshimiwa Spika, isadie basi kuimarisha mtandao unaohudumia vyama hivyo vya akiba na mikopo nchini *(SCULT)*. *SCULT* imefanya kazi kubwa katika nchi yetu ya Tanzania.

Sasa kama itawezeshwa vizuri na Benki Kuu itaifanya *SCULT* iweze kusimamia vizuri sana vyombo hivyo vidogo vidogo vya fedha hizo *SACCOS* ambazo tunazo na zikaweza ku-*deliver* huduma inayotakiwa lakini kwa kufuata utaratibu wa ushindani wa kibiashara ambao utasaidia kuvielekeza vyombo hivyo katika utaratibu mzuri wa kuwasaidia wananchi wa nchi hii ya Tanzania katika picha nzima ya *win-win situation* ama katika picha nzima ya *fair deal* katika ya Mabenki hayo makubwa na hizi asasi ndogo za fedha.

Mheshimiwa Spika, mfano nchi ya Cameroon, wanawake wamekuwa ni mfano mzuri sana kwa tabia ya kuweka akiba na kukopa na hivyo vyama vya akiba na mikopo katika nchi ya Cameroon vinafanya vizuri sana na badala yake sasa, Mabenki yanakopa kwenye vyama vya akiba na mikopo na siyo vyama vya akiba na mikopo kukopa kwenye Mabenki, na hivyo tukifikia hapo ukombozi wa mwananchi wa Tanzania utakuwa ni mkubwa sana. Hii kazi yote isimamiwe na Benki Kuu kwa mujibu wa Sera na Utaratibu wake.

Mheshimiwa Spika, nguvu za *SACCOS* katika nchi yetu bado ni ndogo. Kwa mfano katika nchi yetu ya Tanzania tuna wanachama 254,651 tu. Katika Soko angalau la watenda kazi kama milioni 16 katika nchi ya Tanzania ukiacha wale wengine ambao tunaweza kusema kwamba siyo soko la watenda kazi.

Lakini tukijilinganisha na nchi ya Kenya, nchi ya Kenya wenzetu wamefikia kuwa na wanachama 2,500,000 katika soko la wananchi milioni 14. Sasa unakuta kiasilimia, sisi tuna asilimia 1.6, lakini wenzetu Kenya wamefika asilimia 17.

Mheshimiwa Spika, hapo nina mifano ya nchi kama Malawi na nchi nyingine nyingi. Sasa tunaona kwamba bado tuna kazi ya kufanya. Tutengeneze ajenda ya vyama vya akiba na mikopo kama ajenda maalum kama tulivyoweka ajenda ya MMEM, kama

tulivyoweka ajenda sijui ya nini. Kwa nini hatuamui ajenda ya vyama vya akiba na mikopo kama ajenda ya lazima katika nchi yetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naomba sana katika Bajeti hii inayokuja Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninakuomba sana Serikali iangalie ajenda ya Vyama vya Akiba na Mikopo kuwa ajenda ya lazima, kwa sababu ndiyo ukombozi pekee kwa kweli wa mwananchi wa Tanzania katika Kasi Mpya, Ari Mpya na Nguvu Mpya.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli tuna haja ya kubadili mifumo hii ya utendaji wa vyombo vya fedha katika nchi yetu ya Tanzania na ninaomba nirudie tena, atakayetusaidia kubadilisha mfumo huu ni Benki Kuu peke yake. Anao uwezo, na mimi naamini Gavana namfahamu vizuri sana, ni mtenda kazi. Akiamua kulivalia njuga suala hili kwa kuzingatia kwamba tunae Waziri ambaye ni mchapa kazi mzuri katika Serikali hii ya Awamu ya Nne. Mimi naamini tunaweza ku-*deliver* kabisa maendeleo ya wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna ajenda ya kuboresha kilimo, tuna ajenda ya kuboresha masoko, tuna ajenda nyingi sana za kupambana na umaskini zilizo ainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi. Lakini nimesema ili tuendelee kama siasa safi ya Serikali ya Chama Cha Mapinduzi tunayo, uongozi bora wa Serikali ya Awamu ya Nne tunao, watu tunao, ardhi tunayo, tunaweza ku-*deliver* kabisa maendeleo ya wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, tuna ajenda ya kuboresha kilimo, tuna ajenda ya kuboresha masoko na tuna ajenda nyingi sana za kupambana na umaskini zilizoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. Lakini nimesema, ili tuendelee, kama siasa safi ya Chama cha Mapinduzi tunayo, uongozi bora wa Serikali ya Awamu ya Nne tunao, watu tunao, ardhi tunayo, fedha ndiyo tatizo, ni lazima tukubaliane. Ni lazima suala hilo nalo tuliangalie ili tuweze kufanikiwa katika mkakati huu wa kupambana na umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nichukue fursa hii kukushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuchangia mada hii leo. Lakini ninaomba niseme kwamba ninaunga mkono Muswada huu na ninaomba sana Waziri wa Fedha ashirikiane na chombo hiki kikuu katika nchi yetu ya Tanzania kuzingatia haya mambo mawili, MKURABITA na suala la *SACCOS* kuwa ni suala la lazima na siyo hiari. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Susan Lyimo, wakati huo huo Mheshimiwa Martha Mosses Mlata ajiandae. Naye ametoa sababu ya kwenda kwenye kikao. Kwa hiyo, ndiye atakayefuata na baada ya hapo atafuata Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya. Nakuomba radhi sana Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, lakini nimejaribu kuona kwamba niyakubali maombi ya hawa ambao wana kazi maalum sasa hivi. Nakuomba radhi sana.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii. Awali ya yote niipongeze sana Wizara ya Fedha hususan Waziri

pamoja na timu yake nzima iliyoweza kutayarisha Muswada huu ambao nadhani kama unavyoonesha lengo lake ni uwazi zaidi na uwajibikaji kwa Watendaji wa Benki Kuu. Pia, niwapongeze kwa sababu kwa kweli Muswada huu umekuja wakati muafaka ambapo dunia nzima iko katika mageuzi si tu ya kifedha, lakini ya kiuchumi na kijamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, ningeomba kuchangia katika sehemu mbalimbali ambazo ninaamini zitaleta maboresho katika Muswada huu. Kwanza kabisa kama ambavyo Wabunge wengi wamechangia, ningependa kuchangia kwenye suala la riba.

Mheshimiwa Spika, riba ya kukopea na riba ya kukopeshea katika nchi ya Tanzania kwa kweli haina uwiano wowote. Utakuta riba ya kukopea kwa mfano ni asilimia mbili tu, wakati ile ya kukopeshea ni asilimia 22 mpaka 30. Kwa mantiki hiyo basi, wananchi wengi hasa wale wa chini kama vile wakulima, wameshindwa kukopa, hivyo wakopaji wamekuwa ni wafanyabiashara wakubwa tu na hivyo kuwafanya wakulima ambao ni asilimia 80 ya wananchi wa nchi hii wakiendelea kuwa maskini na hivyo wale wafanyabiashara wakubwa wakiendelea kuwaibia.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hii *Central Bank* inajulikana kama ni *Bank of the Banks* na kwa sababu ndiyo Mdhibiti Mkuu wa Sera ya Fedha, nilitegemea pia wahakikishe kwamba riba katika mabenki yetu inakuwa na uwiano ili wananchi wa kawaida waweze kukopa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuchangia hoja hiyo, kuna suala zima la *SACCOS* ambalo limeongelewa kwa kirefu na Wabunge wengi na mimi pia kwa kuwa ninatetea maslahi ya wananchi, sina budi kuliongelea.

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema mchangiaji aliyenitangulia, suala la MKURABITA linajulikana na mpaka sasa hivi kuna *levels* mbili ambazo ni pamoja na kuhakikisha kwamba wananchi wanajiorodhesha na kupewa *identity cards.* Pia, kuna suala zima la kuorodhesha mali zao. Nafikiri sasa kwa sababu *SACCOS* imekuwa na wateja wengi sana na pia *SACCOS* hizi hazipati fedha za kutosha, basi wale wananchi wote ambao watakuwa chini ya MKURABITA wapewe mikopo na Benki mbalimbali. Benki Kuu ndiyo itakuwa kama *guarantor* wao ili wale wengine ambao hawatakuwa chini ya MKURABITA wawe sasa wanahudumiwa na *SACCOS*. Nadhani hii itatusaidia sana ili wananchi wale wa kawaida, wa kipato cha chini na hawana mali zozote waweze kusaidiwa na *SACCOS*.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nataka kuongelea ni suala la *ATM*. Kwa kweli hizi mashine sasa hivi zimekuwa ni kero kwa wateja wengi hasa siku za *weekend*, unakwenda unakuta hazifanyi kazi. Mtu anahangaika kwenda kwenye *ATM* zaidi ya tano anakuta huduma imesitishwa na wakati huo huo Benki zote zinakuwa hazifanyi kazi. Kwa hiyo, nafikiri kwa sababu hizi *ATM* pia zinahusiana na masuala ya fedha na Benki Kuu kama msimamizi mkuu wa fedha nchini, basi wangehakikisha kwamba hizi *ATM* angalau zinafanya kazi na kama hazifanyi kazi kwa sasa hivi labda utaalamu haujawa wa kutosha, basi zifungwe ili tuwe tunategemea Benki kama siku za nyuma.

Mheshimiwa Spika, naomba pia niongelee suala la marupurupu katika Bodi. Hii iko katika ukurasa wa 42 *section 24.* Inavyoelekea ni kwamba hii Bodi imejiwekea mamlaka ambayo watakuwa wanajipangia marupurupu. Pia, wanasema kwamba haitatangazwa kwenye gazeti la aina yoyote. Mimi najiuliza, kama lengo la Muswada huu ni kuweka uwazi na uwajibikaji, ni kwa nini hili suala la marupurupu wanajipangia? Sisi tutajua watajipangia Shilingi ngapi? Mimi nafikiri hili suala kwa kweli lifanyiwe *amendment*. Sioni sababu kwa nini hii Bodi ijiwekee marupurupu yenyewe na pia wasitangaze. Kuna usiri gani hapo? Ni vizuri Waziri ahusishwe na ikiwezekana watangaze kwenye *Gazette*.

Mheshimiwa Spika, kuna suala pia la uchakavu wa sarafu hasa sarafu ya Sh. 100/= na sarafu ya Sh. 50/=. Ukienda Vijijini kwa kweli hizi fedha zimekuwa hazijulikani kwa sababu wala hazina sura ya Rais au sura ya kitu chochote. Lakini zaidi ya hapo, nafikiri wakati tunaongelea suala la uchakavu wa hizi fedha, basi Benki Kuu iangalie ni jinsi gani wanaweza kuboresha sarafu hizo. Labda wazibadilishe badala ya kuwa shaba ziwe hata za *silver* kwa sababu zile za *silver* naona zinadumu zaidi.

Mheshimiwa Spika, lakini pia ieleweke kwamba suala la uchakavu wa fedha hizi umekuwa unaleta matatizo makubwa sana hasa kwenye vyombo vya usafiri hususan Miji kama ya Dar es Salaam. Mfano unakuta mtu ametoa nauli labda Sh.150/=, lakini ile hela kwa kuwa haitambuliki ni hela gani, imekuwa ni ugomvi sana kati ya msafiri na *conductor*. Kwa hiyo, nadhani Mheshimiwa Waziri aliangalie suala hili.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye suala la *qualities* za Gavana katika *section (8) page 31.* Hapa wanasema awe na *degree* ya Chuo Kikuu. Mimi najiuliza, hii ni *degree* ya kwanza *bachelors* au ya pili, yaani *Master* au ya tatu yaani *Ph.D.*! Kama ni suala la *degree* ya kwanza, nadhani limepitwa na wakati kwa sababu kwa kweli kuendana na utandawazi na hali halisi, nafikiri hii *condition* iliwekwa wakati ule wa uhuru ambapo kuwa na *first degree* ilikuwa unaonekana kama ni Profesa. Kwa hiyo, hii hapa nafikiri ieleweke kwamba ni *degree* ya kwanza au ya pili. Kama ni *degree* ya kwanza, nadhani sio sahihi, labda iwe *Ph.D.* au *degree* ya pili yaani *Masters*. Kwa kuzingatia sasa hivi *first degree* kwa cheo cha Ugavana ni hafifu sana.

Mheshimiwa Spika, kuendana na kipengele hicho cha pili cha *experience*, nadhani *experience* ya miaka 15 ni halali kabisa. Kwa sababu kama tukichukulia mwanafunzi anamaliza Chuo Kikuu akiwa na miaka 20 halafu tukampa *experience* ya miaka mitano au kumi, huyu atakuwa na miaka 25 hadi 30 tu. Kwa hiyo, tuangalie kwamba Gavana ni mtu nyeti sana na ni mtu ambaye ni *professional*.

Mheshimiwa Spika, suala la *experience* ya miaka 15 naliafiki kabisa kwa sababu kuu mbili. Kwanza, huyu mtu atakuwa amesha-*mature* na ana *levels* zote za *maturity,* yaani *psychological, mental* na *physical* na zaidi ya yote ana *wisdom*. Kwa hiyo, kusema mtu wa miaka 25 au 30 awe Gavana wa Benki Kuu na tumeshaambiwa Benki Kuu maana yake inadhibiti au inaangalia uchumi wa nchi usitetereke, siamini kama kijana wa miaka 25 anaweza kufanya kazi hiyo. Lazima tukubaliane Gavana sio *Branch Manager* au

*Cashier.* Kwa hiyo, nakubaliana kabisa kwamba miaka 15 ya *experience* ni sahihi kabisa na ninamwomba Mheshimiwa Waziri asibadilishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakubaliana nalo kabisa kuwa na *Deputies* watatu. Lakini toka tumeanza hii hoja, wengi wamekuwa wakisema kwamba mwanamke awe mmoja, tena angalau. Kwa sababu hii namba ya Gavana na *Deputies* watatu jumla yake ni nne, ukigawanya kwa mbili yaani jinsia mbili ya mwanamke na mwanaume inakuwa mbili. Kwa hiyo, nafikiri ni wakati muafaka kabisa *Deputy* awe mwanamke mmoja na Gavana pale juu awe mwanamke. Kwa sababu toka nchi hii imepata uhuru hatujawahi kupata Gavana mwanamke! Lakini nimeangalia kwenye *internet,* kuna *Governors* wengi sana wanawake duniani.

Kwa hiyo, nafikiri kwamba, kwa kuwa cheo cha Ugavana kinatokana na *professional* na kwa sababu kuna wanawake wengi ambao wana *professionals* za fedha sasa hivi, basi ifike mahali tuone kwamba sasa hivi wanawake wanaweza kushika nafasi hiyo ya ugavana. Hivyo *Deputy* awe mmoja mwanamke na *Deputies* wawili wanaume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inaonyesha pia kwamba Benki Kuu kama Benki nyingine pia zinafanya biashara ya dhahabu. Dhahabu kwa nchi zote ni kipimo cha *currency* na uchumi wa nchi. Kwa kuwa mikataba mingi hasa ya migodi ya dhahabu imekuwa na utata na kwa sababu tuna wataalam wa Benki Kuu, basi nafikiri wakati muafaka umefika Benki Kuu pia iwe inasimamia masuala yote ya biashara ya dhahabu.

Mheshimiwa Spika, kama walivyoongelea Wabunge wengi na mimi kusoma katika sehemu mbalimbali, suala hili la uhuru wa Benki Kuu kwa kweli nadhani lina utata. Labda kama Watoa Muswada wataweza kutueleza vizuri zaidi huu uhuru wao ni wa namna gani na mipaka yao ni ipi, kwa sababu suala lolote ambalo halina mipaka, kwa kweli itakuwa ni vurugu. Nadhani labda wana nia njema ila tu sisi Wabunge hatujaelimishwa vizuri au hatujaeleweshwa vizuri huu uhuru unafikia wapi na labda watueleze pia katika *statistics* zao wameona Benki zipi duniani zenye uhuru na zimefanya vizuri zaidi. Nafikiri ifike mahali sasa Watoa Muswada watuelimishe kwa kina huu uhuru ulikuwa unadhamiria kitu gani ili kusiwe na matatizo kati yetu. Pia isionekane kama tumekuwa na uadui nao, bali tunataka kuelewa kwa sababu Benki Kuu ni chombo cha nchi hii na hivyo tunahitaji kupata maelezo ya kina.

Mheshimiwa Spika, suala hilo hilo la uhuru katika kusoma nimeona hata nchi zilizoendelea sana kama Uingereza na Marekani, uhuru katika *Central Banks* zao umepatikana hivi karibuni. Kwa mfano Uingereza wamepata uhuru huo miaka ya tisini mwishoni. Lakini pamoja na uhuru huo, bado Waziri wa Fedha kwa mfano wa Uingereza ana mamlaka katika Benki Kuu. Kwa hapa kwetu tumepata uhuru miaka 40 tu iliyopita. Kwa hiyo, naamini kabisa hii Benki Kuu bado haijawa na uhuru wa kuweza kujitawala yenyewe. *Unless* Watoa Muswada watatuelimisha, naamini tutakuwa katika mtazamo mmoja.

Mheshimiwa Spika, naomba pia niongelee suala la *Bureau de Changes* hapa Tanzania. Sasa hivi kumekuwa na *Bureau de Changes* nyingi sana ambazo naamini kwa kuwa nazo zinafanya biashara ya fedha, basi kwa njia moja au nyingine ziko chini ya Benki Kuu. Hizi *Bureau de Changes* nyingi zipo sehemu ambazo kwa kweli hazina usalama. Ukienda Kariakoo unakuta *Bureau de Change* iko ndani ya duka la nguo! Kwa hiyo, nadhani Benki Kuu iliangalie kwa sababu wateja wanaweza kupata matatizo kutokana na sehemu ambazo *Bureau de Changes* hizi zipo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni suala la Gavana kuwa Mwenyekiti wa Bodi. Binafsi sina tatizo nalo kwa sababu kama tulivyosema awali Gavana ni Mtendaji Mkuu, kwa hiyo hapa hakuna suala la *politics*. Kama tunataka tumweke Mwenyekiti ambaye hana uelewa wa masuala ya fedha, hivyo vikao havitafanyika. Itakuwa ni kazi ya Gavana kuanza kumuelimisha Mwenyekiti au Mwenyekiti kuwa na mvutano na Gavana.

Nafikiri kwa sababu wale *Board Members* nao ni wataalam wa fedha, basi Mwenyekiti akiwa ni Gavana, mimi sioni tatizo kabisa kwani suala hili pia liko katika Benki zote za dunia. Siku zote Gavana wa Benki ndiyo pia Mwenyekiti wa Bodi. Sioni kwa nini Tanzania tuwe tofauti. Zaidi ya hayo, Mwenyekiti kama hana uelewa wa utendaji wa kila siku wa Benki Kuu itakuwa ngumu sana hivyo kumnyima uhuru Gavana.

Mwisho, tuelewe kwamba Benki Kuu siyo Kampuni ya biashara kama *TLB, TCC* na kadhalika. Kama tulivyoona mabenki mengi yamekuwa yakitoa faida kubwa, nawahamasisha wanawake wenzangu tuanzishe Benki ya akina mama ili na sisi tuweze kujikomboa. Kwa kuwa ni muda mrefu sasa akina mama wamekuwa na hali duni kiuchumi, Benki Kuu itakuwa mkombozi wa akina mama. Tunaomba Benki Kuu itusaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani nimechangia katika vipengele ambavyo vitaboresha Muswada huu. Lakini mwisho kabisa naomba niongelee kipengele cha 20 katika ukurasa wa 40 kinachohusiana na *Auditing Committee.* Ukiangalia hii *Auditing Committee* haifafanui itakuwa na watu wangapi. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Watoa Muswada huu watusaidie kutuelimisha ili tujue hii *Committee* ina watu wangapi na inafanya kazi gani.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, naomba kuwasilisha na nitaunga hoja mkono pale tu vipengele nilivyovizungumzia na vile ambavyo Wabunge wengine wamechangia vitakuwa vimeingizwa kwenye Muswada huu. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Martha Mlata, atafuatiwa na Dr. Lucy Nkya na Mheshimiwa Paul Kimiti ajiandae.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia Muswada huu. Nami napenda kuungana na wazungumzaji waliotangulia kwa kuwapongeza Waziri pamoja na timu yake kwa

kufanikisha suala zima la Muswada huu na hatimaye kuufikisha hapa ili na sisi tuweze kuchangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sitakuwa na mengi sana ya kuchangia kwa sababu mengi yameshachangiwa na ninaamini yamepokelewa na yatarekebishwa kutokana na jinsi wachangiaji walivyoshauri. Pia, napenda kuungana na wazungumzaji waliotangulia hasa kwa nafasi ya zile nne za Gavana kwamba kuwe na nafasi moja au mbili za wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia nina ushauri mwingine kwamba, pamoja na kuwa tunasema kuwe angalau na mwanamke mmoja, imefika wakati sasa kwa sababu wanawake wanaweza, wamesoma na wameelimika sawa tu na wanaume, tusianze kusema 'angalau' kuwe na mwanamke mmoja. Kwa nini isiwe 'angalau' kuwe na mwanaume mmoja? Kwa hiyo, nafikiri haki hizo zote ni sawa, wanawake wote wapewe haki sawa na wanaume. Mwanamke asiwekwe kwamba 'angalau'. Ukiweka 'angalau' ina maana umempendelea wakati anaweza kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu uhuru wa Benki Kuu. Huu uhuru ninauunga mkono, lakini uhuru ukiutumia vibaya itakuwa ni matatizo. Ila utakapoutumia vizuri, basi itakuwa ni manufaa kwa nchi nzima. Ninaomba uhuru huu Benki Kuu iutumie vizuri, tusije kuwapa uhuru ikawa ni sawa na kumpa kichaa rungu, sisi wenyewe tukaja kujutia kwa nini tulitoa uhuru huu. Tunaomba uhuru huu utumiwe vizuri.

Mheshimiwa Spika, ninarudi katika masuala ya maendeleo hasa ya kijamii. Kwanza katika Muswada ule nimesoma kwamba Benki Kuu imetaja Benki nyingi sana, lakini sikuona ikitaja Benki ya Wakulima pamoja na Benki ya Wanawake. Kwa hiyo, ninaomba kuuliza, Serikali ina mpango gani kuhusu Benki ya Wakulima na Benki ya Wanawake? Maana Serikali ilitaja hili, lakini Benki Kuu haijataja.

Mheshimiwa Spika, katika Sera ya Uwekezaji, nchi yetu inategemea sana uchumi hasa kwa wananchi ambao wanafanya biashara zao ndogo ndogo pamoja na wakulima, maana wao wanategemea hivi Vyama vya Kuweka na Kukopa hasa *SACCOS*. Wazungumzaji waliotangulia wamesema, lakini mimi ninaomba Benki Kuu, basi ijaribu kuweka mkono wake zaidi hasa katika kupunguza ile riba kwa vile Vyama vinavyokwenda kukopa kwenye mabenki kwa sababu riba inakuwa ni kubwa, wanakopa pesa ambazo zinakuwa ni ndogo, zinakuwa hazikidhi mahitaji ya walio wengi. Benki Kuu iweze kudhibiti zile Benki zinazotoa mikopo kwa *SACCOS* ili *SACCOS* ziweze kutoa mikopo zaidi kwa wananchi kwa ajili ya maendeleo ya nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo napenda kuzungumzia ni kuhusu viwanda. Benki Kuu ni msimamizi mkuu wa uchumi wa nchi yetu. Sielewi Benki Kuu ina utaratibu gani kuhusu viwanda vyetu. Ninaamini viwanda vinapata mikopo, lakini sina uhakika kama vinapata mikopo kwenye Benki hizi za kawaida.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kuzungumzia ni kwamba, uchumi wa nchi yetu utakua pale tu viwanda vyetu vitakapokuwa vinafanya kazi na viwanda hivi vinahitaji kuwezeshwa, viwanda vikubwa pamoja na vidogo ambavyo vyote vinawafikia wananchi. Benki Kuu iweze kuweka mkono wake pale kupitia Benki zile za kawaida ili Benki hizi

ziweze kuweka mahusiano mazuri na viwanda hivi, ili viwanda hivi viweze kuendelea kufanya kazi kwa ufanisi zaidi na vile ambavyo vimekufa viweze kufufuliwa ili uchumi wetu uweze kukua maana tunategemea kilimo kama tunavyosema.

Mheshimiwa Spika, mfugaji anapofuga ng'ombe wanaishia kuliwa kwenye mabucha, lakini tuna viwanda ambavyo vimekufa kama *Tanganyika Packers.* Ili kuweza kumwezesha mkulima huyu au mfugaji huyu, basi tunaomba viwanda kama hivyo na vingine vingi viweze kufufuliwa kupitia Benki za kawaida. Lakini Benki Kuu iweke utaratibu ambao itaweza ku-*control* kupitia Benki hizi ndogo kushirikiana na viwanda hivi ili kuweza kufufua viwanda na kuviwezesha.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda kuzungumzia ni kuhusu utamaduni wa wananchi kuweka fedha kwenye Benki. Walio wengi hawaweki fedha kwenye Benki. Ni kweli watu hawaweki kwa sababu kwanza kabisa unapopeleka hela Benki, masharti yale na usumbufu ule unaokuwepo unamfanya mtu aone kwamba sasa kwa nini nihangaike! Anarudi na anakaa na pesa zake. Pia, anapofanikiwa kuweka pesa zake Benki hakuna faida kubwa anayoipata, ile hela imekaa tu kule, ipo tu, yaani faida ni ndogo. Ninaomba Benki Kuu kwa sababu yenyewe ndiyo Bosi, iweze kuweka mkakati wa kuzibana hizi Benki za kawaida ili ziweke utaratibu mzuri kwanza wa kufungua akaunti; pili, angalau iongeze riba nzuri kwa mwekaji wa pesa zile ili mtu atakapoweka pesa zake, wakati anapokwenda kuchukua akute angalau kuna unafuu. Hiyo inakuwa ni motisha ya kusaidia watu kuweza kuweka pesa Benki.

Mheshimiwa Spika, lakini pia Benki Kuu yeye ni Bosi, ana uwezo wa kupandisha Shilingi na ana uwezo wa kushusha ile Shilingi, lakini kila wakati ile Shilingi inashuka, sielewi kwa nini Benki Kuu inaachia thamani ya Shilingi yetu inaendelea kushuka. Ninaomba Benki Kuu ijitahidi kupandisha Shilingi yetu ili iweze kwenda katika kiwango cha Kimataifa na uchumi wetu utakua zaidi. Kwa hayo niliyochangia, mimi ndiyo nitakuwa mchangiaji namba moja kuchangia kwa muda mfupi sana. Ninaunga mkono Muswada huu. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Paul Kimiti ameomba achangie jioni. Kwa hiyo, sasa namwita Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya. Badala ya kufuatiwa na Mheshimiwa Kimiti atafuatiwa na Mheshimiwa Anna Richard Lupembe.

**MHE. DR. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Spika, naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi hii. Nami pia ningependa niungane na Wabunge wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kutimiza siku 100 za uongozi ambao umeonyesha matumaini kwa Watanzania. Nampongeza na Serikali yake pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda niwapongeze waliotengeneza Muswada huu; Mheshimiwa Waziri, Mama Meghji na wasaidizi wake wote. Huu Muswada umekuja kwa wakati ambao tunahitaji kuona mapinduzi katika *Bank Institutions* za Tanzania. Umefungua milango kwetu sisi watunga sheria na wawakilishi wa wananchi tuweze kuzungumzia mapungufu na kero ambazo wananchi wanazo katika Taasisi zetu za Benki.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea, ningependa nizungumze kwanza kuhusu changamoto ambazo nafikiri Benki Kuu inatakiwa kuziona na kuzi-*address*. Changamoto moja kubwa ni kwamba, kama walivyozungumza wenzangu kuna biashara huria ya fedha katika nchi hii. Kuna vikundi ambavyo vimeanza vyenyewe, wenye uwezo wa kuchangisha pesa wanakopesha wananchi kwa riba kubwa na wanawapa *grace period* ya wiki moja wanaanza kuwa-*harass*. Naomba kusema kwamba wahanga wakubwa au *victims* wa hii biashara ni wanawake.

Mheshimiwa Spika, kuna watu wanaowakopesha wanawake pesa, ni watu binafsi, wanawakopesha kwa mamlaka gani, hatuelewi! Wala siyo *NGO* inayotambulika kisheria! Wanawakopesha kwa riba ya asilimia 30 na wanatakiwa kuanza kurudisha baada ya wiki moja. Badala ya kuwasaidia hawa wanawake inawafanya wanaingia kwenye matatizo makubwa mpaka wengine wanafikia kuuziwa nyumba zao na watu binafsi kwenye nchi yenye utawala wa kisheria na kwenye nchi ambayo ina Taasisi kubwa kama Benki Kuu ya kuweza kuhakikisha kwamba wananchi wanafahamu sera za ukopeshaji na biashara za kifedha.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya pili, amezungumza mchangiaji mmoja kuwa kuna *Bureau de Changes* ambazo zimefumka nyingi sana katika nchi hii, hadi unafika mahali unajiuliza, hivi *Bureau de Change* imekuwa ndiyo biashara sasa kama maduka ya Mitaani au vipi? Sisi kama nchi tunafaidi nini kwenye hizi *Bureau de Changes*? Wengine hata ukienda kubadilisha pesa wanafanya haraka haraka hata risiti hawakupi unabakia kujiuliza: Je, Benki Kuu kweli inapata chochote kutoka kwa hawa watu? Tunaomba Benki Kuu iangalie na kutengeneza mfumo mpya wa kufanyia tena marejeo au *review* huu mfumko wa *Bureau de Change* kwa sababu wengi wanatorosha pesa kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ni hizi Benki ambazo zinakuja nchini. Kule kwao masharti ya riba ni nafuu, lakini wanapokuja hapa inakuwaje wanabadilisha? Kama kule kwao walikuwa wanatoa riba ya asilimia 10 kwa mtu anayekopa wanakuja hapa wanafanya mpaka asilimia 20 wanatumia kigezo gani? Wamekuja kufanya biashara au wamekuja ili na wao waweze kuchangia katika uchumi wa nchi hii? Naomba Benki Kuu pia ione kwamba hiyo ni changamoto kwa huu mfumo mpya unaoanza kuhakikisha kwamba wanafanya kazi yao ya *regulation properly* kwa maslahi ya Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine, nakwenda kwenye ibara ya 52 kifungu cha 1(a) pale ambapo wanasema kwamba pamoja na majukumu mengine itakuwa na jukumu la *import, export , buy, sell or otherwise deal in gold.* Kama hii shughuli itafanyika vizuri italeta matumaini katika kuwasaidia wachimbaji wadogo wadogo. Naomba kushauri kwamba Benki Kuu kama itakuwa inashughulika na ununuzi wa madini hasa madini ya dhahabu, waongeze pia na kununua madini ya *Tanzanite* kwa sababu mbili muhimu. Sababu ya kwanza ni kuweza kuwahakikishia wachimbaji wadogo wadogo fursa ya kuweza kupata soko la uhakika ambalo litawapa bei ambayo inastahili yale madini. Pili, itasaidia kupunguza utoroshaji wa madini.

Mheshimiwa Spika, nashangaa ninaposikia kwamba Kenya inasema inauza *Tanzanite* nje. Madini haya wao wanachimba wapi? Soko lao liko pale Arusha, wanakuja wanahakikisha kwamba wananunua kutoka kwa wachimbaji wadogo wadogo kwa sababu wale wachimbaji hawana mfumo maalum wa kusaidiwa na Serikali yetu wa kuweza kujua kwamba kuna *centre* au mahali ambapo wanaweza kwenda kuuza madini yao kwenye uhakika na usalama na mahali ambapo watapata bei iliyo nzuri. Basi kama wataamua kwamba watawasaidia wachimbaji wadogo wadogo kununua madini.

Mheshimiwa Spika, ningeomba kushauri kwamba Benki Kuu iangalie iwezekano wa kuweza kutengeneza Taasisi ya Kifedha ambayo itasaidia kutoa mikopo midogo midogo kwa wachimbaji wadogo ili waweze kununua mitambo pamoja na nyenzo za kuweza kuchimba madini kwa njia ya usalama zaidi na ya uhakika ambayo itawasaidia waweze kuongeza uzalishaji wao.

Mheshimiwa Spika, kwa njia hii tutakuwa tumeongeza ule uwezo wa Mtanzania wa kawaida wa kuweza kumiliki uchumi unaotokana na madini ambayo ni mengi katika nchi yetu. Kwa masikitiko makubwa ni kwamba, wanaofaidi zaidi ni wachimbaji wa kutoka nje na nchi za jirani ambazo kuna wafanyabiashara wajanja wanaweza kuja wakanunua na wakaondoka na hayo madini.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ambayo ningependa nizungumzie kuhusu Benki Kuu ni namna watakavyoweza kusaidia *SACCOS*. Wengi wamezungumzia *SACCOS*, lakini labda naomba nitoe *experience* tu. Kwa mfano, kazini kwangu ambako nina *NGO,* wale wafanyakazi wameanzisha *SACCOS*, lakini inabidi wakafungue akaunti *NBC* kwa masharti yao na wanapokwenda kuchukua pesa wanachajiwa *service charge*. Wakitaka kukopa kule watalipa riba kubwa.

Sasa unaangalia, unasema sawa, hizi *SACCOS* tunaanza kwa sababu tumewachoka hawa watu. Lakini pamoja na kuwachoka hatuwakwepi kwa sababu ni lazima tukawekeze kule kwao hela zetu. Tunapiga kelele tuanzishe *SACCOS* lakini hizi *SACCOS* hazitamkomboa Mtanzania, tunaendelea kuwapa faida hawa watu. Kama Benki Kuu haitakubaliana na sisi Wabunge kwamba wakati umefika sasa tuanzishe Taasisi ya kifedha ambayo itashughulika na kuimarisha *SACCOS*, itahusika na kuweka mazingira ya *SACCOS* kutunza akiba zao, kusudi ile riba na *service charge* zibakie hapa nchini kwa uchumi wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa nilizungumzie ni kuhusu uongozi. Ni kweli kwamba tunataka tulete mageuzi na mapinduzi katika kuboresha huduma za Benki Kuu. Nisingependa kupiga kelele sana kama walivyopiga wengine, lakini na mimi niwaunge mkono wenzangu kwamba tunapofikia kwamba Gavana ndiye anayekuwa Mwenyekiti wa Bodi, yanapotokea malalamikio na matatizo mengine kwa utamaduni wetu wa Kitanzania tunavyokuwa tunaendesha shughuli zetu, kumekuwa na Bodi ambayo ni *independent.* Unakuta kwamba *the Chief Executive* wa ile *institution* anakuwa kama ni Katibu wa ile Bodi. Sasa inapotokea malalamiko au matatizo unayapeleka tena kule inakuwa kama unachukua kesi ya ngedere unaipeleka kwa nyani. *What do you expect?*

Mimi nafikiri wananchi hawatakuwa na imani kubwa sana, watakapoona kwamba yule yule bwana ambaye anafanya kazi tumempa dhamana ya kufanya kazi, ni yeye mwenyewe sasa anakuwa ndiye mdhibiti wa shughuli zake na kujidhibiti mwenyewe na wenzake, tunakuwa na swali kulikoni? Hata kama wakifanya kazi nzuri sana, hatutaisha kusikia malalamiko na migogoro inaibuliwa kwenye magazeti ya uongo na ya kweli kwa sababu watakuwa wanasema kwamba wanaojidhamini *watch dogs of that institution* ndiyo hawa wanaoendesha shughuli. Tunasema kwamba kuwepo na *the proper watch dog of the government* ni wananchi ambao ndiyo wanaipa hii Benki dhamana ya kuangalia shughuli zote za uchumi na kifedha za nchi hii. *(Makofi)*

Mimi nafikiri kwamba kama walivyosema wenzangu, Serikali iangalie namna ya kuboresha tena huo Muswada ili kuhakikisha kwamba angalau basi tunakuwa na Mwenyekiti, kama siyo Mwenyekiti wa kudumu, basi Mwenyekiti Mwenza ambaye anaweza akanyoosha kidole akasema kuna hili, tubadilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niangalie tena *composition* kijinsia, naomba niseme kwamba tunaposema angalau, ni kwamba mnatudhalilisha wanawake. Ni kama tunakuwa ombaomba. Mimi naomba kabisa Muswada huu uzungumze wazi kwamba ni lazima awepo mwanamke kwa wale Wasaidizi watatu, mmoja awe ni mwanamke na ikiwezekana tuseme wawili kwa sababu nchi hii sasa hivi wote wanawake na wanaume ni wadau wa maendeleo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunaomba sisi wanawake kama ni wadau wa maendeleo na tunaochangia pato kubwa la nchi hii ili tupate uwakilishi unaolingana na wanaume kwenye vyombo vyote ambavyo vinaangalia maendeleo na uchumi wa nchi hii. Ninaomba lile neno “angalau” liondoke tuseme kwamba basi asilimia 50 ya uongozi iwe ni wanawake na asilimia 50 iwe ni wanaume kwa sababu hata Serikali yetu na Chama cha Mapinduzi, imeona kwamba kuna umuhimu wa kuchangia katika uongozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakumbuka *speech* ya Waziri wa Kilimo na Chakula ya mwaka 2001, alisema kwamba: “Wanaochangia maendeleo ya kilimo nchi hii asilimia 80 ni wanawake.” Sasa kama kilimo ndio uti wa mgongo, ndio tunategemea sana kwenye *export* na kuleta uchumi wa hii, kwa nini wanawake hawa wasiwakilishwe? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie lingine. Tunazungumza kwamba tunataka tuanzishe Benki nyingine, lakini wananchi wa nchi hii wanajiuliza *Tanzania Housing Bank* ilikufa kwa sababu gani? Kwa sababu gani *CRDB* imebinafsishwa ikaondolewa kwenye mikono ya wananchi? *CRDB* ilikuwa ni *Rural Cooperative and Development Bank.* Sasa tuzungumzie tena kuanzisha Benki nyingine, *what happened?* Utamfanyaje mwananchi wa nchi hii awe na imani kwamba Benki itakayoanzishwa itakuwa inafanya kazi na haitakufa tena na haitabinafsishwa?

Ninaomba wanaohusika na Muswada huu watueleze kwamba watafanya nini, kuna uchawi gani? Sasa kama kutakuwa na uchawi kweli wa kusaidia basi tunaomba kama tunataka kweli kuanzisha, tuanzishe Benki ya Maendeleo ya Wananchi Tanzania na

tuhakikishie wananchi kwamba tutakapoweka fedha zetu kule haitafilisika, tutakapoweka fedha zetu mle haitabinafsishwa tena, aje mtu wa nje kufaidi jasho letu. Tunaomba tupewe uhakika huo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza hayo, naomba nikumbushie suala la *SACCOS*, Taasisi ya kuhakikisha inaboresha *SACCOS* na kuimarisha *SACCOS* na kutoa fursa ya wananchi kuweza kuwekeza hela zao na Taasisi, ambayo itawasaidia wachimbaji wadogo wadogo na *commitment* ya Benki Kuu, kwamba watahakikisha wananunua madini yanayozalishwa na wachimbaji wadogo wadogo tukiwa na nia moja ya kuboresha uchumi unaotokana na madini na kuweza kuwaendeleza wachimbaji wadogo wadogo ili ifike mahali dhana ya kusubiri Makampuni makubwa kutoka nje, kuja kuchimba madini yetu na kuondoka nayo iweze kuondolewa, tujenge *capacity* ya Watanzania kumiliki uchumi wetu kwenye madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kuunga mkono Muswada huu. Nawapongeza watu wa Benki Kuu.

Mheshimiwa Spika, miaka ya 1970, 1980 kulikuwa kuna Benki moja kubwa sana ambayo ilikuwa inaitwa *NBC*. *NBC* ilikuwa ni chombo ambacho ni cha Serikali, ilisambaa nchi nzima mpaka Vijijini. Benki hii iliweza kufanya kazi vizuri mpaka Tarafani.

Mheshimiwa Spika, Benki ile ilivunjwa ikawa Benki ya *NBC,* ikawa *NMB*, ikawa *NBC Holding*. *NBC* ikawa Benki ya Biashara, *NMB* ikawa Benki ya watu wa Vijijini ambayo hiyo *NMB* ilikuwa inasaidia watu wa Vijijini huko Wilayani.

Mheshimiwa Spika, Benki hiyo sasa hivi imekuwa nayo Benki ya Biashara, siyo Benki tena ya watu wa Vijijini. Sasa Benki hiyo imekua mpaka Mikoani. Sasa; je, *BoT* kwa nini isiwape leseni *NMB* ili iweze kufika mpaka Tarafani? Vile vile kuna Benki ya *CRDB*, tulikuwa tunasema ni Benki ya wakulima. Sasa hivi *CRDB* nayo vile vile imekuwa Benki ya Biashara, siyo Benki tena ya wakulima. Nashangaa Benki Kuu hawataki kuwapa leseni *CRDB! CRDB* ni Benki ya wakulima ambayo inawalenga wananchi Vijijini. Benki ya *CRDB* na *NMB* zingefanya kazi kubwa sana kutusaidia masuala ya Vijijini kama ilivyo mfano *SACCOS*. Maana yake wangetoa leseni kwa *NMB* ambayo imesambaa mpaka Wilayani, *NMB* wangekwenda mpaka Tarafani. *CRDB* wangekwenda mpaka Tarafani ili waweze kusaidia masuala ya *SACCOS*.

Mheshimiwa Spika, *SACCOS* ni chombo cha wananchi wenyewe. Mwananchi mwenyewe anachangia, maana yake sisi Wabunge, tumewahamasisha wananchi wajichangie wenyewe kutoa Sh.10,000/= ili wajiunge na vikundi vya *SACCOS* ili wapewe hela na Benki. Sasa je, Benki ya *NMB* na *CRDB* haziko Vijijini, zamani ilipokuwa *NBC* mwananchi alikuwa anajua Benki, maana yake *NBC* ilikuwa inaingia Vijijini kwa *Agency*. Ilikuwa kama anatoka Wilayani anakwenda Tarafani kupeleka labda mishahara, wananchi walikuwa wamehamasika kujua Benki. Lakini sasa hivi wananchi

hawajui maana ya Benki ni nini, maana yake ni muda mrefu toka mwaka 1997 Benki hizi zilivyovunjwa, zikagawanywa *NBC, NMB* na *NBC Holdings.*

Sasa nilikuwa naomba Benki Kuu itoe leseni kwa *CRBD* na *NMB* kwa vile wenyewe wako Wilayani. Maana yake sasa hivi *NBC* hatuwezi kuwaingilia kwa sababu wenyewe ni wafanyabiashara maana imeshauzwa kwa Makaburu, wenyewe ni wafanyabiashara hawawezi kwenda Wilayani au kwenda Vijijini wala hawawezi kuwakopesha wanavijiji wadogo wadogo. *NMB* na *CRDB* ndio walengwa kwa wanakijiji. Sasa nilikuwa naomba Benki Kuu watoe leseni ili *NMB* na *CRDB* watoe mikopo. Kwa vile *CRDB* ni Benki ya wakulima na *NMB* ni Benki ya wafanyabiashara wadogo wadogo, nilikuwa naomba wawape leseni ili waweze kuingia mpaka Tarafani.

Mheshimiwa Spika, ukizingatia sasa hivi Walimu wanaofundisha Vijijni kama kule kwetu Mpanda - Inyonga, anatoka Inyonga mpaka Mpanda ni kilomita nyingi sana, hana uwezo. Akifika pale anakaa muda mrefu anaacha shughuli za Shule, kuwafundisha watoto ili aje kuchukua mshahara Mjini. Sasa kama Benki Kuu ikitoa leseni kwa *NMB* ni rahisi kutoa *Agency NMB* kutoka kwenda Tarafani kuwasaidia wale wanavijiji na kujua wale wanavijiji kama kuna Benki inaitwa *NMB* na kusaidiwa zaidi na vikundi vya *SACCOS* kujiunga zaidi, maana yake Wabunge wengi sasa hivi wamekwenda kuhamasisha wananchi kwamba jiungeni na *SACCOS.* Sasa unakuta wengine wako Vijijini mno kiasi ambacho hawajui hata maana ya *SACCOS* ni nini, hawajui maana ya Benki ni nini.

Sasa nilikuwa naomba Benki Kuu ihamasishe, itoe leseni kwa Mabenki haya mawili ili yaweze kusaidia wananchi walengwa hasa wa Vijijini ili waweze kupata hii mikopo ya *SACCOS* ambayo tumeilenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Benki Kuu, ndiyo chombo kikuu cha fedha katika nchi yetu. Lazima kiwe na sura ya nchi na lazima kisimamiwe na Watanzania wenyewe. Kinachoshangaza sasa hivi, sarafu ya Shilingi hamsini kusema kweli wananchi wa Vijijini wanapata taabu sana kwa sababu zile hela namba zimefutika kabisa na akichukua ile akienda nayo dukani wanamkatalia. Wakati mwingine akienda Benki kusema labda amekusanya hela zake nyingi aende Mjini apeleke zile hela, Benki yenyewe wanagoma kuzipokea hizo hela. Je, mwananchi wa Kijijini atafanya nini kwa hizo *coins? (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa kuchangia kwamba Waziri wa Fedha awe anashirikishwa kutoa maamuzi yanayofanyika Benki Kuu, maana yake hapa mimi silewi kama Gavana na Waziri nani mkubwa, hii inachanganya sana. Nani ana maamuzi zaidi? Au ni vyombo viwili tofauti!

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, napenda kuchangia kuhusu mikopo kwa wakulima. Nilikuwa naomba Benki Kuu itusaidie kutukopeshea wakulima wetu walioko Vijijini. Maana yake sisi, kwa mfano Mkoa wetu wa Rukwa ni Mkoa wa kilimo. Naomba tungepewa pembejeo au tungeletewa matrekta na Benki Kuu. Nafikiri tungezalisha chakula kingi sana nchini Tanzania. Haya masuala mengine ambayo yametuletea shida kipindi hiki kama njaa yote hayo yasingekuwepo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuungana na wenzangu kuunga mkono Muswada huu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, ninapenda nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia machache kuhusu hoja ya Benki Kuu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono moja kwa moja Muswada huu. Kwa kweli umelenga kutukwamua katika matatizo yetu ya kiuchumi na ikiunganishwa na utashi wa Serikali yetu ilivyojionyesha katika siku 100 nina uhakika tuna mwelekeo mzuri na nina uhakika tunaweza tukafikia malengo yetu ya kuweza kujikwamua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningeomba kwamba chombo hiki kisiwe chombo cha kupokea amri tu au Wakala wa Mabenki ya Nje au Taasisi za Fedha kama *IMF* na Benki ya Dunia. Maana mwelekeo wa muda mrefu umekuwa ni kunufaisha zaidi watu wa nje. Sasa tungekuwa na malengo ya ndani zaidi kama ambavyo wenzangu wamezungumza, katika kutusaidia., wabuni mbinu za kututoa katika umaskini wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi huwa nasononeka sana ninapoona nchi yangu iko mkiani katika nchi za *The Least Developed Countries.* Sijui kama tumeshaondoka kuwa wa pili kule kwenye mkia, sijui tuko wa ngapi! Ni aibu na mimi huwa nakataa na katika kukataa huwa najiwekea kigezo changu mimi mwenyewe nilipo. Lakini sasa ukija kuangalia hali halisi ya wananchi, mara nyingine unalazimika kukubali unapotembea, unapoona umaskini uliokithiri, wakati tumezungukwa na utajiri mkubwa sana. Sidhani katika *region* hii kama kuna nchi ambayo inatupita.

Sina haja ya kuainisha utajiri wetu, kila mmoja anajua. Lakini sasa sisi tumekuwa ni *conduit* tu, utajiri wetu unatoka na Benki hizi ndiyo zimekuwa *conduit* kama nilivyosema, mali zetu zinatoka hazinufaishi wananchi wetu wa ndani, bali zinakwenda kunufaisha watu wa Mataifa mengine. Unapoambiwa *Tanzanite* inapatikana Tanzania peke yake inaongoza kwa uzalishaji lakini unaambiwa India au Kenya nazo zinaongoza kwa uzalishaji wa *Tanzanite.* Basi unashindwa kuelewa maana yake nini! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi ningeliomba sana kwamba Benki hii ijaribu kutusaidia iweke sawa sawa vyombo vyake, Mabenki ya fedha yaweze kutusaidia na yaingize uzalendo ndani. Kwa mfano tunapoanza kuona tena magazeti hata hatujapitisha huu Muswada tunaanza kuona uvundo, tunasoma vitu ambavyo kwa kweli vinatukatisha tamaa. Tuko katikati ya kujadili huu Muswada, lakini unakuta magazeti yanaripoti vitu vingine kwamba zile *twin towers* zina matatizo, gharama zake ni kubwa kuliko ilivyokadiliwa.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nadhani tufikie mahali tupate watu ambao wanaweza kuwa na uchungu wa nchi hii na tumeona jinsi viongozi wetu hapa walivyotuonyesha katika siku hizi 100 jinsi walivyo na uchungu wa nchi hii. Kwa hiyo,

mimi nina hofu kidogo ninapokuta kwamba kuna vitu kama hivyo na kama ni kweli, basi inatukatisha tamaa. Ningeliomba sana tuwe makini katika kuwasaidia wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, ningeomba sana, sambamba na kulenga wakopaji wa ndani tungeliwaomba sana hawa watu wa Benki na Taasisi, zake zielewe kwamba utamaduni wetu sisi bahati mbaya haukutusaidia kuwa mbele kuweza kuyatumia haya Mabenki. Tumekuwa waoga kwa sababu ya riba zao, tumekuwa waoga kwa sababu ya masharti yao magumu. Basi ninachoomba elimu itolewe, waje na program maalum na mahususi ili ziweze kuwaelimisha wananchi wetu nini maana ya kukopa na nini maana ya kurudisha mikopo. Kwa hili ninaona bado kuna kazi ya ziada. Sidhani kama wameweza kuwafikia wananchi sawa sawa kuweza kuwaelimisha ni nini umuhimu wa kukopa na ni nini umuhimu wa kurudisha mikopo.

Mheshimiwa Spika, sekta isiyo rasmi haitambuliwi. Mimi ningeliomba kwa makusudi Benki Kuu na Mabenki yake iweze kuelekeza Mabenki yake yaweze kuja na program maalum za kuweza kuwasaidia wananchi wetu waweze kuelewa nini maana ya kukopa. Sidhani kama wafugaji na wakulima wameelimishwa sawa sawa. Mfugaji kuachana na mifugo yake labda pengine akauza au labda akaenda kukopa Benki bila kumwelimisha sawa sawa na hata jinsi ya kuweza kutumia hizo fedha, basi tutakuwa tunatwanga maji kwenye kinu kwa sababu haelewi, wala hajui akipata hizo fedha afanyie nini. Lakini nadhani elimu pia inahitajika kutolewa kama kweli tuko *serious* katika kuweza kujikwamua kwenye huu umaskini. Tunaweza kuwa na pesa na Mabenki yakawa *open* kukopesha lakini kama hakuna elimu kwa walengwa itakuwa ni kazi bure.

Mheshimiwa Spika, ningeliomba kwamba Mabenki haya yaende kwenye *potential areas.* Tuna sehemu kemkem ambazo kuna rasilimali nyingi, lakini sehemu hizi hazifikiwi na Mabenki. Hakuna Benki. Mimi eneo langu ninalotoka kuna biashara nzuri sana kama mbao, asali, nta, tumbaku, kuna *Game Reserve* na kila kitu, lakini hakuna Benki. Watu wanatoka kilometa 150 mpaka 200 kwenda kufuata Mabenki.

Mheshimiwa Spika, sidhani kama kuna utashi, haya Mabenki yanavyojizatiti zaidi Mjini mimi kila siku ninapofika Dar es Salaam kila nikieneza macho nakuta Benki mpya, hata majina mengine ni vigumu kutamka. Lakini sasa unapokwenda Vijijini kule hakuna huduma hizi. Ningeomba tuzifuate hizi rasimali ili tuzitumie vizuri tuweze kujikwamua kwenye matatizo tuliyonayo.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ambacho nataka kuchangia ni tatizo la ulinzi wa Mabenki yetu, imekuwa kero kila siku kusikia kuna uporaji, wizi katika Mabenki haya na imetokea kwamba Mabenki haya mara nyingine yanalindwa tu na watu wasiokuwa na silaha na kumetokea kwamba Mabenki haya mengine yamekataa hata msaada wa ulinzi wanaopewa na Serikali.

Sasa hii inaonyesha dhahiri nia ya hizo Benki. Ziko pale kuvuna na ikiwezekana kupora kwa sababu kwa nini wakatae ulinzi? Haileti picha nzuri! Kama tunaweza kuwa na mali ambazo zinaweza zikaporwa mchana, asubuhi na watu wanaelekezwa na Serikali lakini hawasikii, hizo taratibu na Kanuni zao zinalenga nini hasa? Ningeliomba Benki

Kuu, ijaribu kuona utaratibu wa utendaji wa Mabenki yake ili fedha hizi ziweze kutumika kwa utaratibu uliokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, mimi nitatofautiana kidogo na wenzangu kwa sababu katika muundo wa utumishi huyu Gavana pamoja na wasaidizi wake watatu, ningeliomba kigezo kikubwa kiwe *professionalism* kweli kabisa. Ifuatwe taaluma bila kujali *gender issue*. Sasa wakiwa wanawake watatu humu ndiyo wajaze hizo nafasi basi, iwe hivyo, lakini ufuatwe uwezo, taaluma na vigezo vifuatwe sawa sawa. Lakini hii *euphoria* na *fanfare* ya kwamba wanawake tu, kwa kweli tutajiweka mahali pabaya, tutasababisha *brain drain* kwa upande wa vijana wetu wavulana kwa sababu watakapokuja kuona kwamba kuna upendeleo kwa kufuata vigezo vya *gender* na siyo *competitiveness* ya taaluma, basi wanaweza kuamua kuondoka kwenda kutafuta kazi nchi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ninazungumzia hili kwa makusudi kabisa kwamba hii nafasi iwekwe wazi kulingana na vigezo vilivyowekwa. Mimi sidhani kama kuna kigezo kimewekwa kusema kwamba mwanamke asijaze hiyo nafasi. Sasa kama mwanamke anafaa, basi ajaze nafasi, kama mwanaume anafaa naye ajaze hiyo nafasi isiwe wazi. Katika sehemu zozote za taaluma tafadhali sana suala hilo liangaliwe. *(Makofi)*

Kuna nafasi nyingi, mimi ninawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge, akina mama waliopata nafasi nyeti kwenye Baraza la Mawaziri kwa kweli nimefurahi sana. Lakini sidhani kama walipata kazi hizo kwa sababu ya upendeleo wa *gender issue,* haiwezekani! Nani asiyemfahamu Mama Zakia Meghji alivyo mahiri, nani asiyemfahamu Mama Nagu na wengine ni watu mahiri katika kazi zao na ndiyo maana wamefikia hapo. Kwa nafasi za kisiasa na kadhalika, tunaweza tukatoa upendeleo maalum tuwasukume wenzetu.

Mheshimiwa Spika, lakini kwenye nafasi za taaluma tafadhali ningeomba sana hilo suala ni *sensitive,* tuwaache watu wa-*compete.* Tunaambiwa kwenye Muswada mtu akae miaka 15 ili awe Gavana. Sasa amefikisha miaka 15 na akitumikia Benki hiyo, karibu miaka yake yote leo kwa sababu ya kigezo cha *gender* anaachwa anakuja mama anawekwa pale kwa sababu ya *gender issue,* labda kafanya kazi miaka nane au kumi. Sasa tunakwenda wapi? *We should not be carried away* na *euphoria fanfare!* Tuangalie ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tusije tukasababisha *brain drain,* halafu pili wakishindwa hata kupata kazi huko, basi wakarudi, wanaweza kuiga Utamaduni wa Magharibi wakabadili jinsia zao kama upendeleo ndiyo huo. Kwani sio kitu kigeni kwa nchi za Magharibi, mtu anakwenda anatoa hela anabadili jinsia na anadungwa sindano anaota kifua, basi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba wenzangu waelewe kwamba tunawapenda akina mama lakini, wakazane kuhakikisha tunakwenda kulingana na utaratibu. Hakuna anayemkataza mwanamke kusonga mbele.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuchangia hayo machache, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Ahsante. *(Makofi)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kukupongeza kwa kujaa vizuri kwenye Kiti hicho. Nakuombea baadaye pengine huko tunakokwenda uvae kabisa na joho. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupewa fursa hii ya kuweza kuchangia kwenye Muswada huu. Madhumni na sababu za Muswada huu zimeelezwa vizuri kabisa, zimeeleweka kwamba ni kuongeza uhuru na madaraka ya Benki Kuu katika kuendesha shughuli zake. Lakini nilikuwa nina mawazo ya kuomba wenzangu Wabunge kwamba kadri tunavyopanua uhuru na madaraka ya vyombo hivi vya umma, tujikumbushe na sisi vile vile kupanua uwajibikaji wa vyombo hivi vya umma kwa umma. Huko ndiko kwenda na *best practice.* Nilikuwa naomba pengine nijaribu kuwakumbusha baadhi ya wenzangu matamshi ya Gavana wa *US Federal Reserve,* Bwana Laurence Meyer kuhusu uwiano wa uhuru wa *Central Banks* na vile vile uwajibikaji wake kwa wananchi.

Alikuwa ametoa mawazo katika *lecture* aliyoitoa Wisconsin. Nilikuwa naomba uniruhusu tu nisome kipengele kidogo. Anasema: *"Independence does not mean literally independence from the Government because Central Banks are part of Government. Independence of the Central Bank has to balance with accountability, accountability to the public and, specifically, to the elected representatives." (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napenda kuona kwenye Muswada huu, tukitoa uhuru zaidi kwa Benki Kuu na tukitoa madaraka zaidi. Lakini wakati huo huo tuongeze uwajibikaji wa Benki Kuu kwa Wawakilishi wa wananchi. Zipo njia nyingi za kuongeza uwajibikaji wa Benki ambazo zinatumika duniani kote. Naweza kutoa mifano mitatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu sasa hivi tumepunguza madaraka ya Waziri chini ya Muswada huu, lazima uwajibikaji wa Benki Kuu kwa Wabunge uongezeke kidogo.

Nitoe mifano mitatu. Wa kwanza, ni kutenganisha nafasi ya Mwenyekiti na nafasi ya Gavana. Mimi nina uhakika *US Federal Reserve* ina Mwenyekiti, ina Gavana, na mambo yanakwenda vizuri tu. Tunaweza tukafanya hivyo hapa sisi ili ku-*facilitate,* kuweza kuruhusu *accountability*.

Pili, uteuzi wa nafasi hizi nyeti za Gavana, Mwenyekiti na hata Wajumbe wa Bodi, napendekeza uthibitishwe na Bunge hili ili kuongeza *accountability*. Inafanyika kote duniani na hiyo ndiyo *best practice* na nchi zote za Europe sasa hivi nafikiri nyingi zaidi lazima nafasi hizo zithibitishwe na Bunge. Kwa mfano, *European Central Bank, President* na Wajumbe wote lazima wapitishwe na *European Parliament*. Jamani hata

*Central Bank of Russia,* vile vile Viongozi wa Benki hiyo lazima wathibitishwe na Bunge. Marekani, *US FederalReserve*, viongozi wote wanathibitishwa na Bunge.

Lakini na njia ya tatu ni *Annual Report* ambayo iko chini ya Muswada huu, ibara ya 21, inawasilishwa na Benki Kuu. Mimi nilikuwa napendekeza iwasilishwe kwenye Kamati inayohusika ya Bunge kuweza kujadiliwa. Huko ndiko kuongeza uwajibikaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Benki Kuu ya 1995 ambayo inatumika mpaka leo, inatamka wazi chini ya kifungu cha tisa kuwa Gavana na *Deputy Governor* watatumikia kwa vipindi vya miaka mitano mitano ambavyo vinaweza kurudiwa mara ya pili. Lakini hawawezi kutumikia zaidi ya misimu miwili. Muswada huu uko kimya. Nimesoma *Hansard* ya 1995 na mjadala wa Waheshimiwa Wabunge ndani ya Bunge hili. Sababu zilizofanya Bunge hili liweke vipindi viwili ni nzuri mpaka leo. Sioni kwa nini tunaondoa hii ili mtu aendelee kuteuliwa, kuteuliwa na kuteuliwa. Hapana, tupokezane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani tusitunge Sheria kwa kuangalia sura za watu. Tutunge Sheria kwa kuangalia ni kitu gani tunataka ku-*achieve*. Tulikuwa tunaongea hapa juzi ni jinsi gani vijana wanaweza nao wakawa Magavana. Tumetaka hata kubadilisha vigezo, kupunguza mpaka *qualifications*. Hapana tusipunguze *qualifications*. Ibakie miaka 15 na uzoefu wa kutosha. Lakini tupokezane. Miaka 10 ikiisha basi *bye, bye,* ahsante kwa kazi nzuri. Ndiyo hivyo. Lakini *Bill* iko kimya. *It is silent!* Naomba Mheshimiwa Waziri arudishe hicho kipengele cha vipindi viwili. Kilikuwa na sababu nzuri wakati ule na ni miaka 10 tu imepita, hizo sababu hazijaondoka.

Halafu Muswada unataka, *Deputy Governors* watatu! Tumekubali. Tumeambiwa sababu: kazi zimeongezeka, ni nyingi sana. Lakini tukisoma ibara ya 13 ibara ndogo ya nane inasema, huyo Gavana na ma-*Deputy* wake wanaweza vile vile kuwa ma-Gavana, Wakurugenzi, Wajumbe wa Bodi kwenye Mabenki ya Dunia na Taasisi zake. Sasa kumbe wana muda, mpaka kuwa huko kwenye Mabenki ya Dunia.

Tumeambiwa wanakuwa watatu kwa sababu kazi zimeongezeka hapa. Sasa hiki kipengele kinawawezesha kuwa Wakurugenzi wa Mabenki ya Dunia. Halafu kipo kipengele kingine cha 13 (viii) (b) kwamba wanaweza kuwa hata Wakurugenzi kwenye *any Corporation in Tanzania which the Bank has promoted.* Jamani! Maana kama kazi imeongezeka mbona wanazidi kujiongezea kazi! Hebu tuige mifano ya Benki nyingine ambapo hawa watu wako *fully devoted to the affairs of the Bank.* Tuachane na masuala mengine ya pembeni huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara ya 41 iangaliwe upya na Wataalam. Nisingependa kuiongelea kwa muda mrefu kwa ajili ya muda. Ujumbe hautoki sawasawa kwenye hiyo ibara. Inahitaji *recasting*. Vile vile, Benki Kuu naomba iache kuendesha shughuli zake kwa usiri. Sasa hivi wanayo huduma ya kutoa *guarantee* kwa Watanzania na Makampuni ambayo yanataka kukopa pesa kwenye *Commercial Banks.* Kwa mfano mwaka jana wameshafikia mpaka kutoa guarantee kwa kampuni moja ya

bilioni 30. Lakini wananchi wengi hawaijui huduma hii. Benki Kuu kuweni wawazi ili kila mtu ajue kwamba hiyo *facility* ipo, lakini wekeni vigezo na masharti yanayoeleweka. Sasa kusikiasikia tu kwamba fulani amepata *guarantee* siyo vizuri kwa chombo cha umma kama hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumalizia kwamba Benki Kuu wanadai madaraka zaidi kama nilivyosema, wakati madaraka waliyonayo chini ya mwaka 1995 ni makubwa mno. Lakini wao wenyewe hawataki kuyatumia. Hasa pale inapohusu kuwadhibiti Wazungu, sijui wanapata kigugumizi gani!

Mwenyekiti, nina mifano kadhaa, wenzangu wameongelea kidogo. Tumekuwa na utamaduni wa kulinda Benki zetu kwa silaha miaka mingi. Wamekuja wawekezaji wa Afrika Kusini, wakasema hapana, sisi hatutaki watu wenye silaha kwenye Benki zetu. Wakaifuata Benki Kuu, Benki Kuu ikaridhia. Leo matokeo yake tunayaona. Benki Kuu ina bahati sana kwamba Watanzania siyo watu wanaopenda kushitakishitaki. Ilitakiwa wahusishwe katika kesi za madai ya watu walioathirika, kwa sababu ilikuwa ni uzembe kukubali kumwachia *a private investor,* mfanyabiashara kutoka nje, asimamie usalama wa raia hapa! Haiwezekani kabisa!! Uamuzi huo ulikuwa tu kuwasaidia wa *South Africa* hawa walioingia wakati huo walete Makampuni yao ya *security.* Ndiyo ambayo yanalinda Benki zetu hapa kwa virungu.

Pili, huo ni udhaifu wa Benki Kuu. Tuna Mabenki mengi sasa ambayo yanashughulikiwa na Benki Kuu. Lakini kinachoniuma sana ni kwamba zipo Benki ambazo kwa zaidi ya miaka mitano *Data Bank* zao, *main server* zao ziko nje ya nchi. *NBC main server* iko *South Africa* na Benki Kuu inaangalia tu.

Tuliwahi kuwauliza jamani, kwa nini mnaruhusu hawa watu wanakuwa na *main server* nje ya nchi? Benki Kuu inatoa majibu ya *technical* ya ajabu ajabu tu. Lakini mimi nawahakikishia, nimekuwa ndani ya *NBC,* naelewa *what is happening.* Naelewa *the Computer System* tuliyoweka pale. *Data* yote inayoingia kwa siku, *transactions* zote kwa siku ndani ya *NBC,* zinakwenda kwanza *South Africa. You can't retrieve the records* mpaka kesho baada ya kukarabatiwa. Ndipo wanapewa Benki Kuu, nao wanaziamini kwa miaka yote mitano. *(Makofi)*

Lakini sheria imewapa madaraka yote. Nenda Kenya, nenda Uganda, sijaona Benki ambayo imeruhusiwa iwe na *Data Bank* nje ya nchi. Mimi nashindwa kuelewa, hivi Benki Kuu inapatapataje takwimu zake sahihi za *daily transactions* kwenye mabenki kama *NBC?* Siku hizi nafikiri imeingia mkumbo na hii Benki ya *Standard Chartered.* Nayo huweka *data* zake Nairobi.

Suala la *interest rates* wenzangu wameliongelea sana. Bila Watanzania walio wengi kuwa na *access to credit,* kwa kweli hili zoezi la ujasiriamali litakuwa gumu kwa watu wengi sana. Historia yetu sisi Watanzania, Waswahili, ni historia ya kuwekwa pembeni, kunyimwa *credit,* kunyimwa mikopo tena kwa Sheria.

Kwenye Semina hapa nilijaribu kuielezea hiyo Sheria iliyotungwa mwaka 1931 mwezi Mei. Inaitwa *Credit to Natives (Restriction) Ordinance.* Waswahili tulikuwa tunazuiwa kupata mikopo. Kwa hiyo, toka mwaka 1931 mpaka 1961 miaka 30 ilipita tukiwa tumezuiwa na Sheria tusipewe mikopo. Mwaka 1961 mpaka 2006 miaka 45, Waswahili tumeendelea kuzuiwa kupewa mikopo kwa riba kubwa ya kutisha. Hiyo riba ni ya kutuzuia. Ni sawa na kuweka Sheria kwamba Waswahili msikope na Benki Kuu inaangalia tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, dai kubwa la Benki zetu zilizokuwepo hapa ni kwamba sisi ni *risk*. Niliongozana na mwenzangu hapa Mheshimiwa Waziri, kwenda kwenye Benki kukopa. Naye vile vile akaambiwa ni *risk.* Sasa kama nchi hii wote sisi ni kuti bovu, sasa wanatafuta nini hapa? Yaani kila mtu ni *risk* katika nchi hii na Benki Kuu inaangalia hivi hivi. Benki Kuu tumieni utaalam wenu, elimu yenu yote muiokoe nchi hii. Tuna uhakika kabisa mkidhamiria, hizi Benki zitawasikiliza.

Nitoe pendekezo moja dogo. Mnazilipisha Benki kodi na malipo mbalimbali, ziondoleeni kodi mbalimbali Benki ambazo ziko *willing* kushusha *interest rates*. Vile vile, mnaweza mkashusha hata viwango vya hii mnayoita *Statutory Minimum Reserve* kwa Benki ambazo zinaonyesha *indication* ya kuitikia kilio chetu. Kwa kweli sasa hivi, tumefikia mahali ambapo bila Benki Kuu kufanya *intervention,* basi tunapoteza muda kupiga kelele kuhusu ujasiriamali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kusema kwamba Benki Kuu isipofanya hivyo, basi heri Benki Kuu tuikodishe kwa mtu tu. Tujue moja tu kwamba iko pale ku-*serve* Mashirika ya nje. Haina kabisa *interest* na sisi Watanzania. *(Makofi)*

Namalizia kwa kuunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. STELLA M. MANYANYA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti au Spika wa muda. Hapo naamini leo hata kule Ruvuma watakuwa wamefurahi kukuona hapo. Pongezi sana. *(Makofi)*

Awali ya yote napenda niwapongeze waliotayarisha Muswada huu akiwemo Waziri pamoja Timu yake yote. Kwa kuwa kweli tunahitaji mabadiliko na mchakamchaka wa maendeleo ya kiuchumi, basi tunaamini Muswada huu ulitayarishwa ili kulenga uwezekano wa kufikia malengo hayo. Lakini nami nikiwa kama mchangiaji, kwanza kabisa najaribu kuoanisha Benki Kuu kama msimamizi kuhusiana na Taasisi nyingine ambazo zinatoa huduma hii ya fedha.

Mara nyingi nimekuwa nikipitia pia makaratasi ya wale wanafunzi pale Chuo Kikuu kwa mfano kwenye *entrepreneurship center* na katika kozi mbalimbali. Imekuwa ni suala kabisa ambalo karibu kila sehemu lazima linaulizwa kwamba kwa nini Benki wanalalamika kwamba pesa wanazo nyingi lakini watu hawakopi na kwa nini wakopeshaji wanalalamika sisi hatupati mikopo? Kwa nini kunakuwa hakuna uweiano kati ya hao wa pande hizo mbili. Lakini tulipofuatilia zaidi tukagundua kwamba kwa kweli Benki zetu zimekuwa na ukiritimba, yaani ile kusema kwamba wamebinafsisha

hakuna faida. Ni ukiritimba mkubwa kutokana na hali ile ya kuwekewa nafasi ya kuwa na riba kubwa. Kwa hiyo, hawapati hasara, ndiyo maana unaona sisi hata tukiwa na silaha, tusipowafuatilia hawa wateja wetu kwa karibu zaidi, yaani hawana hasara.

Ni tofauti sana na mkulima ambaye akishapanda mbegu kwenye shamba lake anafuatilia mara kwa mara ili kuhakikisha kwamba anavuna vizuri. Benki zimekaa pale zinasema mteja atakuja tu na nitamwambia masharti yangu, asipotimiza shauri yake. Lakini wanasahau kwamba wao wako pale kama chombo cha kuwezesha kiuchumi. Nazungumzia kuhusu hii riba ambayo sasa hivi inatolewa. Mimi sioni sababu kwa sababu kama kuna mteja ambaye sio mwaminifu, mimi mwananchi wa kawaida ambaye nachukua mkopo mdogo ndiyo niwe sasa ni kigezo cha kumfanya yeye aendelee ku-*exist*. Kwa sababu kama yeye ambavyo anahofia *risk,* hivyo hivyo hata huyu mjasiriamali mdogo na yeye katika biashara yake ana-*risk* ambazo zinamkabili mbali ya ile *risk* mkopo. Sasa yeye *risk* zake anazihamishia wapi. Kwa hiyo, wawe *pro-active* waangalie njia nzuri za kuhakikisha wanakuwa na mahusiano mazuri na wateja wao ili kuhakikisha wanapunguza hali ya kuwa na *risk* zisizo za kiwango.

Vile vile, nilikuwa nafikiria kwamba, tuweke utaratibu kwamba nikishachukua mkopo, kwa hiyo riba wanaitaka wao ya *percent* kwa mfano 24, nikilipa mkopo wangu nirudishie asilimia 10 kwa sababu nimeshakulipa. Kwa sababu mwanzo uliogopa *risk,* sasa nimekulipa, basi nirudishie. Kwa hiyo, nafikiria kuwe na ki-*scheme* ambacho kitakuwa kama kinatoa *incentive* kwa wale wanaokuwa wamelipa vizuri.

Baada ya kuzungumzia hilo, nilikuwa naomba pia nije katika suala la kiwango cha mtaji. Kwa kweli mimi naomba wafikirie sana zile Benki ambazo zinawafikia wananchi. Nafananisha na Benki Kuu kwa utaratibu unaoendelea. Ni sawa na mtoto wako ambaye umemsomesha atafika huko mbali akapata kazi nzuri halafu akasema siwezi kwenda Kijijini kumwona mama yangu kwa sababu njia ni mbaya, maisha ni magumu. Kwa hiyo, siwezi kurudi huko. Ni sawa na kwenye mashindano, yaani itokee *Miss Tanzania* au *Mr. Tanzania* avae kilemba kizuri halafu huku kwenye mwili mwingine asiweke kitu chochote. Kwa sababu wanatembea peke yao na wanaacha lile gurudumu la maendeleo huku liko peke yake. Inasikitisha sana.

Tunazungumzia kuwaondolea umaskini watu wetu na ndiyo *actually* wanaochangia mtaji kwenye Benki Kuu. Lakini hakujawa na utaratibu maalum wa kuwawezesha hao wanaochangia. Ni sawa na mtu kukata mizizi ya mmea wake anaoutegemea. Sasa mimi nafikiria iundwe *Department* maalum itakayoangalia Watanzania hawa wa kawaida na siyo hawa wageni tu.

Tunafurahia kuona *GDP* ya Tanzania inaongezeka. Lakini *GDP* ile haina faida kwa sababu imeangalia hali ya watu wachache wakati wengi wako katika hali mbaya. Kwa hiyo, naomba sana kwanza kufuatana na huu mtaji, kwa sababu Benki zile ambazo sasa hivi tumeona ni mkombozi, haziwezi kuwa na kima hicho kikubwa wanachofikiria. Watubakizie angalau mtaji usizidi milioni 30 kwa ile milioni 80 au 100 faida ambayo itaonekana shughuli zake zime-*improve* kuonekana kuwa na mwelekeo.

Vile vile, waweke taratibu za masharti tofauti. Kwa mfano sasa hivi kwenye kurudisha mahesabu. Benki hizi ndogo ndogo zikichelewesha kurudisha mahesabu vinachajiwa karibu sawa kabisa na Benki zile kubwa kubwa. Hivi kweli *Mbinga Community Bank* kwa mfano, ui-*charge penalty* milioni 10. *City Bank* ile kubwa na yenyewe *penalty* milioni 10. Hivi kweli kuna uwiano hapo?

Mimi nadhani tuangalie haya mambo, kwa sababu utakuwa tu na faida au utakuwa usomi wako una faida, utakapokuwa unaweza kuanisha kazi yako na mazingira halisi ya wale wanaokutegemea. Kama huwezi kuainisha haina faida. Kwa hiyo, nilikuwa naomba katika hilo aliangalie vizuri na vile vile nilikuwa nimerejea kipengele chao Na.12 kinachozungumzia kuwa na *Monetary Policy Committee* pamoja na *Audit Committee.*

Mara ya mwisho kwa siku za karibuni nimekuwa kwenye Mikutano ya *World Trade Organization* inayozungumzia mazingira ya biashara sasa hivi ulimwenguni. Mimi nafikiria wangeongeza *Committee* nyingine ili uwajibikaji wao uwe mpana zaidi, unaohusiana na masuala ya kilimo na masuala ya wafanya biashara ndogo ndogo. Kwa sababu ukiangalia wenzetu sasa hivi wana-*subsidize,* sisi huku kinachoendelea hakuna. Hakuna msimamo unaoelekea, kiasi kwamba sasa hata maafikiano hayafikiwi.

Kwa hiyo, naomba hilo walichukue kama suala la msingi la kulifanyia kazi na watufahamishe tusiwe tunakwenda wenzetu kivyao na sisi kivyetu. Tumeona mfano wa *TASAF* jana jinsi ambavyo wameweza kushirikisha mfumo mzima mpaka kwenye jamii ya kawaida. Tunaomba watushirikishe pia katika hayo na vile vile sasa hivi tunajiandaa kuingia kwenye *East African Community.*

Najaribu kuangalia Benki Kuu, hawa wakiwa kama Wadau Wakuu wa Uchumi wetu wanaliangalia vipi hili kwa Mtanzania wa kawaida? Kwa sababu tutakaa tunasema kwamba tujiunge tuanze, tuanze. Ni vizuri kuanza, lakini huyu Mtanzania wako umemweka katika hali ipi? Ni wewe tu unafurahia kwamba basi mimi zaidi ya hapa kuna hela sijui zinapita kwenye dhahabu, unasema tayari hii imetosha. Au nchi inaangaliwa vipi kama nchi? Kwa hiyo, nadhani kufanya shughuli zetu kwa kufuata *theories* au ilimradi nchi fulani imefanya hivi, haitatusaidia. Turudi tutafakari tuhakikishe kwamba kila tunalolifanya linaanzia kuwa na maslahi kwa Mtanzania na pili yule mwingine ambaye anakuja katika kujiunga nasi katika kuendeleza uwezo wetu wa kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, naomba niseme imetosha kwa hayo niliyochangia na ninaamini Muswada huu kwanza mbali ya kuunga mkono na waliopigia makofi, niliacha agenda ya msingi, kwa kweli suala la kumwangalia mwanamke ni la msingi. Sensa yetu inaonyesha wazi kuwa wanawake ni wengi zaidi Tanzania. Siyo wengi tu, hata waliosoma ni wengi na wana uwezo mkubwa. *(Makofi)*

Sasa kumekuwa na huu ukiritimba wa wanaume kujipendelea, tukubali tusikubali. Nachukulia mfano kwenye Bodi ya *TANESCO*, mwanamke mmoja! Siyo kwenye Bodi tu, hata kwenye Menejimenti, mwanamke mmoja. Lakini ukifuatilia chini yake wako

watu chungu mbovu wenye uwezo. Ukiulizia kwa nini masharti ya kutangaza zile kazi unakuta lazima ulishakuwa Meneja, nitakuwaje Meneja wakati hiyo nafasi ya Umeneja ulikuwa hujanipa?

Mimi nafikiria iko haja ya kuona hayo na kwa sababu tunawahakikishia hilo ni kwa nini, angalia hata shughuli katika maisha ya kawaida. Mwanamke akishakuwa mjamzito, kama mwanamme aliyempa ujauzito yule mama yeye hana kazi, atakwambia mimi siwezi kumwoa huyu, sasa hivi sijawa tayari. Lakini mama awe na kazi asiwe na kazi lazima alee mtoto na amsomeshe na anafanikiwa. Katika hili, tuangalie hivyo na sisi wenzenu sio kwamba tunashindwa, ni *priority* uwezo tunao. Tupeni nafasi hizo. Kwa hiyo, mimi nafikiria tuchukulie tu kwamba kwa sababu hii tunaifanya kama msukumo na hao wenzetu kwa sababu hawataki kukubali tuweke asilimia 50 wawe wanawake. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mhehsimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia katika Muswada huu wa Benki Kuu. Awali ya yote, majukumu ya Benki hii ni uwazi na uwajibikaji. Nikitazama kifungu cha 9(2)(a) na (b) *Board of Directors* Mwenyekiti ni Gavana mwenyewe. Wasaidizi wake nao ni *Board Members.* Lakini katika Wizara ya Fedha, Katibu Mkuu au yule atakayekuwa amemteua kumwakilisha wa Jamhuri na yule wa Zanzibar wa Serikali ya Mapinduzi, hao wote ni *Board Member,* nusu nzima ni Watendaji Wakuu. Haki na uwazi vinatendekaje? Hivi inawezekana kabisa Hakimu katika kuhukumu kesi yake akasema mimi nina kosa! Mbona tunajidanganya! *(Makofi)*

Mnaposema kwamba eti katika baadhi ya Mabenki, sio yote duniani Magavana ndiyo *Board Members,* wakiwa ni Wenyeviti kwani imekuwa ni Msahafu, Quran Tukufu au Biblia kwamba lazima tufuate? Siyo lazima! Lakini katika kifungu cha 10 (a) na (b) na vifungu vingine vitafuata huko, ninaangalia pale, Mbunge Mwakilishi na Diwani wanasema ni marufuku, haruhusiwi kuwa *Board Member* katika (b) kifungu cha 10 (1)(b) pia kinamkatalia Mtumishi mwingine yeyote wa Umma ambaye ameajiriwa kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma kwamba naye haruhusiwi.

Kama vile haitoshi, kifungu hicho hicho cha 10 ukitazama kifungu kidogo cha 1 (b), (c) na (d) kifungu cha 2 (a) hadi (f) na kifungu kidogo pia cha tatu kinakataza watu mbalimbali wasiingie kwenye U-*Board Member* kuitazama Benki Kuu inafanyaje mambo yake. Kwa nini? Kuna siri gani mnayoificha mnataka muingie nyie Watumishi watupu? Katika eneo hili kuna tatizo. Ndiyo maana Mabenki mengi duniani yanapoona mambo yamekwenda vibaya mahali pengine Benki itaungua, Mahali pengine kutakuwa na tatizo la hapa na pale, kwa sababu ni wale wale wanaojilinda, maana ni binadamu! Maana Hakimu hawezi akahukumu kesi yake. Hili liweze kubadilishwa. *(Makofi)*

Kama kweli majukumu ya Benki hii ni uwazi na uwajibikaji, watakaposhindwa kuwajibika ni nani atakayeweza kuwabana endapo Mwenyekiti ni Gavana na Wasaidizi wake wote nao ni *Board Members* na wao ndiyo wameharibu na watu wa Wizara wako pale; nani atakayeweza kuwadhibiti? Tusidanganyane! Katika nguvu mpya, ari mpya na kasi mpya ni lazima tubadilike! Mambo mengine tusiende tu maadam fulani kafanya na sisi twende hivyo.

Ukitazama katika kifungu cha 8(2), kinatazama Gavana ni lazima awe na *Degree.* Ndiyo! Haitaji ni *degree* ya aina gani. Lakini pia wanasema awe na uzoefu ambao haupungui miaka 15 ambayo atakuwa amejikita katika fani moja kati ya uchumi au Mabenki au uhasibu au mambo ya kifedha. Ndivyo inavyosema katika kifungu cha 8(2) (b). Sina tatizo na hilo. Lakini nadhani itaje wazi wazi zile *qualifications.* Wanazo nyingi! Kwanza *degree* isiwe chini ya *degree* ya kwanza. Iwe *degree* ya pili na kuendelea. Lakini pamoja na kufanya shughuli hizi, tunahitaji pengine tumwone mtu ambaye labda ana elimu ya *CPA*, elimu ya *MBA* na mengineyo kwamba kweli huyu ni mtu aliyebobea katika eneo hilo. Hii itatusaidia kumpata Gavana ambaye kwa kweli ni mtu ambaye amebobea katika fani ya shughuli hizi za kibenki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu cha 70 nikitazama angalau kifungu kidogo cha tatu na nne, Mheshimiwa Waziri hajapewa madaraka ya kutosha katika Benki hii. Amepewa tu katika kifungu kidogo cha kwanza na cha pili na yeye katika kurekebisha masuala mbalimbali kwenye shughuli hizi za kisheria anaambiwa la kufanya. Hayo ni lazima apeleke kwenye Gazeti la Serikali. Lakini Bodi katika kifungu kidogo cha tatu na cha nne wanapobadilisha mambo mbalimbali hawalazimiki kupeleka *notice* kwenye Gazeti. Wataamua wao tu hata kama mambo yanawa-*favour* yatapita lakini hawapeleki kutoa *Government Notice* katika kifungu cha tatu na cha nne ni vidogo.

Kwani, uwazi uko wapi hapa? Sioni kama kuna uwazi. Ni ujanja tu tuliozoea sisi Watanzania! Naomba tubadilike kama kweli *we are serious* kujenga nchi yetu. Hizi Sheria mara nyingi Bunge tunatunga, inafika wakati fulani tunakuta Sheria tuliyoitunga ni mbovu. Sijui hatusomi sana au tunatunga kwa kutazama watu wengine tu kuwaonea haya! Baada ya dakika mbili tunaona kuna matatizo,kisha zimerudi kurekebishwa. Benki Kuu na Benki nyingine kwa mujibu wa Sheria hizi na kwa kupitia utungaji wa Sheria hizi katika Bunge, Mabenki yanawanyanyasa sana wananchi wa kawaida katika kuwakopesha, tena zinawanyanyasa sana. Maana Mabenki wana msemo wao unasema hivi, Benki siyo rafiki wa maskini, kwa Tanzania Benki siyo rafiki wa mkulima. Ni rafiki wa mfanyabiashara. *(Makofi)*

Ni mbaya sana kwamba raia wetu wakazi na hapa nakusudia kusema *indigenous citizens,* wengine hutumia neno wazawa, wala hawana faida na mabenki haya. Wafanyabishara na mara nyingi wafanyabiashara wengi ni wa nje au wenye asili za kutoka nje ndio wanaopapatikiwa na kuwakopesha na wanazidi kuwa matajiri. Ni nani anayewakopesha? Ni hawa hawa ambao tunawapatia madaraka. Wazazi wao wakulima wako Vijijini wanaona hawafai, tukishawapa madaraka katika Mabenki wanawapapatikia hao kwa kupewa *percentage*, 10%, 20% kama zipo au kuwa katika ubia na mmojawapo kutoka katika Mabenki aje anikatalie. *(Makofi)*

Ni watumishi wangapi wenye ngazi za juu wanaotaka kukopa Benki wamekataliwa? Ni wangapi wamekataliwa? Wananchi wa kawaida wapi walikuwa *favoured* katika kupewa mikopo? Hakuna! Orodhesheni tangu tumepata uhuru mpaka leo, nani ambao wamekopeshwa mikopo mikubwa mikubwa Sh. 50,000,000/= kuendelea hadi Shilingi mia ngapi bilioni. Kama yupo mkulima na kama wapo kama wanazidi

wakulima hata kumi, sidhani. Mnithibitishie hilo ili kunieleza kwamba maneno yangu ninayosema sio ya kweli. Lakini tukichunguza kwenye Mabenki yote wanaokopeshwa mapesa mengi mengi ni hao hao! Hoteli gani nimeiona ya mkulima kubwa na unaambiwa hii alikopeshwa na Benki fulani? Hakuna!

Nilipokuwa Ujerumani Mjini Berlin kuna Benki moja kule *Regent* Hoteli kubwa sana ni ya wakulima, ukienda pale gharama yake ni kubwa mno kuliko Hoteli kama vile Berliner Hoteli. Ni kitu cha ajabu, Ndugu Lembeli anaelewa hilo! Kwa sababu wakulima wanawajali zaidi. Hata ukienda nchi za Marekani, wakulima wanakopeshwa zaidi. Sisi tukishasoma, tukishakaa mahali pazuri, tukishalalia godoro na kukaa katika makochi, tunawasahau wakulima, tunawakumbatia wale wafanyabiashara, tena wengine ambao hawafanani na sisi. Tunakwenda wapi? Tutabakia maskini hivyo hivyo mpaka Yesu atakaporudi! Tutabakia hivyo hivyo na tutaendelea kuwahusudu wale na kuwadharau watu wetu. Naomba tubadilike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, tuna fedha yetu ya akiba nje ya nchi kwa ajili ya matumizi yetu labda ya dharura na kadhalika. Lakini uamuzi wa matumizi hayo, mbona sisi Wabunge hatuhusishwi na wala hatujui kinachoendelea? Mimi nadhani wakati umefika wa kuanza kujua mambo yote haya. Tunaona baadhi ya Marais waliostaafu katika nchi nyingine za jirani, wameshitakiwa kwamba wametumia fedha ile kinyume cha sheria kwa ajili ya shughuli zao binafsi, leo hii wako mahakamani. Je, Tanzania haiwezi ikatokea? Haiwezi ikatokea? Kesho na keshokutwa, kama haiwezi, sisi ni Malaika!

Lakini kama tunadhani kesho na keshokutwa inaweza ikatokea iwe baadhi ya Watumishi wanahusika na utunzaji wa fedha hizo au upelekaji na kadhalika, basi tuwe macho.

Lakini kama mnadhani tupo Malaika wa kutosha, basi tuache kama ilivyo mambo yaende kama yanavyokwenda. Lakini mimi nadhani sio sahihi, labda kama mtu haelewi fedha inayowekwa nje kwa ajili ya dharura kama haelewi mambo yake yakoje hapo ataunga mkono kwamba tutaendelea kuwa kama Malaika.

Pamoja na hayo, bado Muswada naona ni mzuri yarekebishwe hayo mambo mawili matatu tusiende tu kama *stamp* unayoletewa weka sahihi unaweka mhuri hata kama hukusoma, kitu kinachoendelea kesho na keshokutwa unaambiwa kwamba wewe uliweka sahihi unatakiwa uende ukafungwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kwa kuwa katika orodha yangu hapa mezani bado nina jina la Mheshimiwa Gaudensi Kayombo na Mheshimiwa Paul Kimiti, na kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge wote wawili wako katika vikao muhimu vya Kamati, basi ninaomba nisitishe Bunge kwa sasa na Wabunge hao wawili wataanza kuchangia mada yetu katika kipindi cha jioni na tutafuatiwa na Naibu Waziri na baadaye Mheshimiwa Waziri atafanya *windup*.

Waheshimiwa Wabunge nasitisha kikao cha Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 06:31 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11:00 jioni)*

*(Saa 11:00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Tunaendelea, ninayo majina miwili hapa kabla ya kumuita Naibu Waziri, lakini kama kuna Mheshimiwa yeyote ambaye anadhani anaweza akachangia kwa sasa hivi si vibaya ninaweza kupokea jina. Kwa hiyo, sasa namwita Mheshimiwa Paul Kimiti wakati huo Mheshimiwa Gaudence Kayombo, ajiandae.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, na mimi napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi kuchangia hoja hii muhimu kwa maisha ya Watanzania mchana huu lakini kabla ya kuchangia hoja hiyo nataka nitumie nafasi hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Rais wetu Jakaya Mrisho Kikwete na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Lowassa pamoja na Baraza la Mawaziri kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa kipindi cha siku mia moja tuliyoambiwa.

Mimi nina imani kabisa ni kazi nzuri iliyofanyika na tunadhani ya kwamba watendaji wote wa Serikali wana kila aina ya sababu ya kujifunza kutokana na viongozi hawa jinsi wanavyofanya kazi zao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kazi ya Uwaziri siyo ya kubahatisha wala ya kubabaisha, ni kazi na ni mzigo mkubwa sana, unapopewa dhamana ya Uwaziri si utani tena, nalisema hilo kwa sababu kubwa mbili, hakuna kitu kinachotusikitisha sisi, unapopewa Uwaziri watu wanakupongeza na kukutakia kila la kheri lakini kwa kweli tungekuwa tunawapa pole.

Mheshimiwa Spika, unapoitwa Waziri kwa mfano wa chakula wakati huna chakula nchini unajisikiaje? Unapoitwa Waziri wa Maji huna maji, unapoitwa Waziri wa Michezo hakuna michezo na mnafungwa kila siku unajisikiaje?

Mheshimiwa Spika, juzi Waziri wetu Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, alifurahi kidogo alipoona kwamba kijana wetu mmoja amekuja na medali ya dhahabu. Mimi nataka nimpongeze huyu kijana ni Koplo anaitwa Samwel Ramadhan, ametujengea heshima kubwa sana katika nchi yetu na hii inadhihirisha kwamba kumbe inawezekana Watanzania wapo wanaoweza kufanya maajabu katika nchi hii mradi tuwape nafasi tuwasaidie ili angalau waweze kufanya majukumu waliyokuwa nayo.

Sasa lakini yapo miwili au matatu ambayo nadhani ni vizuri nikayaongezea katika kipindi tulichokuwa nacho tunapozungumzia suala zima ambalo ni la uhai wa Taifa letu nalo ni *Bank of Tanzania.* Mimi nataka nimshukuru kabisa Rais kwa kumteua Ndugu yetu Mama Zakia Meghji kuongoza Wizara hii, Rais hakubahatisha hata kidogo,

hakubahatisha kumteua hata kwa ajili ni mwanamke, hapana kwani uwezo wake ni wa hali ya juu. *(Makofi)*

Mimi namfahamu kwa muda mrefu labda amesahau. Kwa taarifa yenu Waheshimiwa Wabunge, Mama Zakia Meghji mara ya kwanza kuingia katika shughuli za siasa ilikuwa Kilimanjaro, mimi nilikuwa Mkuu wa Mkoa na yeye kwa mara yake ya kwanza aliteuliwa kuwa Mkuu wa Wilaya ya Moshi na mimi nikiwa Mkuu wake wa Mkoa. Mama Meghji mwanzoni alisita kidogo nataka niwaambieni, alisita kidogo kukubali uteuzi huo kwa sababu yeye shida alitaka aone namna ya kushirikisha washirika vijijini na alikuwa anafanya utafiti wake kuhusiana na ushirika katika nchi hii akaona akiingia katika siasa mambo yote sasa hayatawezekana. Nikampa kila aina ya moyo na ujasiri ili akubali nafasi hii na nikamuahidi ya kwamba ningeweza kumsaidia afanye kazi yake vizuri kwa sababu niliona huyu mtu ana uwezo, upeo na nyota yake ni nzuri, Mama Meghji.

Mheshimiwa Spika, wewe ni shahidi ulipoingia Mkoa wa Kilimanjaro uliona kazi aliyokuwa ameifanya Mama Zakia Meghji na baadaye akapata nafasi akawa Mkuu wa Wilaya akapata nafasi tena akawa Mkuu wa Mkoa akarudi akawa Waziri sasa amepata nafasi ya hali ya juu katika Taifa letu Waziri wa Fedha si mtu mdogo. Mama Meghji tutakukumbuka tungeomba Gavana wa Benki akafanye haraka ili aleta noti mpya zenye sahihi yako tuwe tunakukumbuka Mama Meghji katika hilo. *(Makofi)*

Lakini pia niwapongeze Manaibu wote wawili wanaokusaidia wanafanya kazi nzuri lakini pia nimpongeze Gavana wetu Daudi Balali anajitahidi na anafanya kazi yake vizuri. Kwa kipindi cha miaka karibuni zaidi ya mitano nilichomfahamu Daudi Balali amekuwa mwaminifu akifanya kazi yake vizuri katika misingi tuliyomwekea. Tuna imani ataendelea kufanya kazi yake vizuri aendelee na watumishi wake. *(Makofi)*

Sasa nataka nizungumzie mambo makubwa manne, la kwanza ni wasiwasi ambao sisi Waheshimiwa Wabunge tumekuwa nao kuhusiana na madaraka makubwa ya chombo hiki. Mwanzoni nilisema hivi nini tafsiri ya Gavana, ukiitwa mtu Gavana nani Gavana katika nchi hii hatuna Gavana mwingine, Gavana ni Gavana wa Benki. Gavana tulikuwa nao zamani Wakuu wa Mkoa walikuwa wanaitwa Magavana na Gavana alikuwa na madaraka yote ukiitwa Gavana maana yake ni *rule with authority* ndiyo tafsiri, tafuta kamusi yoyote na utafute nini maana ya Gavana *is the rule with authority.* Ndiyo maana Gavana anapopewa madaraka haya hapewi kama *registrar* wa Kampuni, yeye ni Gavana tumempa madaraka na hayo madaraka ni lazima tumwamini ya kwamba tulipoamua kumteua basi tumempa na madaraka ya kuendesha shughuli zake.

Sasa katika hali hiyo yako mambo ambayo ningemuomba Mheshimiwa Waziri azingatie, la kwanza, malalamiko na wasiwasi wa Wabunge wote katika Bunge hili ni kwamba madaraka haya tusipoyaangalia yanaweza kutumika vibaya, leo tunaye Balali lakini kesho anaweza kuja mtu mwingine kama tutampa mtu mwingine ambaye ni mkorofi anaweza kutufikisha mahali pabaya ndiyo maana tukasema ya kwamba ni vizuri Waziri sasa kwa kutumia nafasi uliyopewa kisheria kifungu cha 70(1) kinaeleza wazi ya

kwamba Waziri utatakiwa kutunga kanuni na sheria za kuendesha shughuli hizi za Sheria.

Lakini pia nataka niombe marekebisho kidogo katika kifungu hicho, pale walipoandika *may* nataka nishauri *AG* ukiwepo hapa nadhani ni vizuri ili kuondoa wasiwasi maana yake *may* unaweza au usiweze, tuweke *shall* ili Waziri alazimike kutunga sheria zitakazosababisha mwenendo mzima wa Benki yetu Kuu na hiyo itamsaidia Waziri ili kama kuna tofauti zozote atasaidia kwa niaba ya Wabunge kuelekeza yale yote ambayo Wabunge wamekuwa wakizungumza yaende sambamba na maoni yetu na kazi mojawapo tungetaka Mheshimiwa Waziri uone namna ya kusimamia suala hilo. Hilo la kwanza.

Lakini la pili ni kifungu cha 70 (3) na (4) hiki kinanitia wasiwasi kwa sababu kinasema Bodi nayo itakuwa na madaraka ya kutunga kanuni na sheria na *bylaws* watakazotunga *of course* hazitakuwa *gazetted.* Kuna mwenzangu mmoja alizungumzia hapa. Sasa ukiangalia hiyo kama hupati maelezo, inaonekana kwamba bodi itakuwa na madaraka sawa na Waziri, sasa nani mkubwa? Ukiicha namna hiyo tutapata matatizo labda Mheshimiwa Waziri au Mwanasheria Mkuu jaribu kutusaidia kufafanua.

Mimi sina ugonvi na kifungu cha 24 ambacho sasa kinaruhusu Gavana kutunga sheria ndogo ndogo kuhusiana na mwenendo mzima wa shughuli za Benki na Watendaji, lakini akishaanza kuingilia kurekebisha na kuweka mfumo anaoutaka yeye mwenyewe anaweza kuweka yale mengine ambayo hayapo ndani ya yale ambayo tulikuwa tunafikiria ni vizuri kifungu hicho nacho kikaangaliwa ili visije vikawa vifungu ambavyo vyote vinaleta utata katika sheria.

Mheshimiwa Spika, tunapoamua suala zima la kumpa madaraka tunajaribu kuona hivi madaraka tunayompa ni ya nini? Kwa nini tunampa madaraka, kwa sababu tunajua kwamba Benki Kuu siyo Shirika la Umma hata kidogo au idara ya Serikali hata kidogo, ni mamlaka nzito na mamlaka kamili ambayo inaangalia suala zima la sera zote za kifedha na hili lazima mtu anayepewa awe ni mtu ameaminika na uongozi ili afanye kazi yake bila kuingiliwa ukishamwambia ni Gavana basi unataka ni nani tena awe juu ya Gavana *unless* mnataka mfanye lile suala liwe ni la kiasa lakini Gavana ni Gavana tunategemea Waziri utakuwa na madaraka sasa ya kupunguza *Govern* yake kama anakwenda kasi wewe kwa niaba yetu unaweza ukafanya hiyo kazi.

Lakini la pili kwa kuwa wenzangu wameshachangia mambo mengi mimi nilitaka kushauri mambo matano yafuatayo:-

La kwanza, katika ari mpya ya Serikali yetu ya awamu ya nne, Benki iweke msukumo maalum kwa vyombo na taasisi za fedha ili kutoa mikopo ya riba nafuu kwa shughuli zote za kilimo hilo la kwanza. Nalisema hilo kwa sababu mabenki yasipojibu tatizo hilo benki zitakuwa wa wafanyabishara wakubwa wakubwa, wakulima tutabaki maskini hatutapata chochote na mwishowe hata benki nayo haitafaidika na wakulima.

La pili, benki tutaomba itambue kuwa kasi kubwa ya ongezeko la watu katika nchi yetu tusipoliangalia linaweza kuathiri sana ukuaji wa uchumi wa nchi yetu. Mimi ni Mwenyekiti wa *Population,* tumeomba Serikali kama inawezekana ije na sera ambayo inashughulikia idadi ya watu. Maendeleo na mpaka sasa hatujaiona hiyo sera hiyo. Tungeomba kweli Serikali ikamilishe hiyo kwa sababu tutake tusitake kama kweli uchumi wetu hautakuwa zaidi ya asilimia 9 na watu wanaongezeka kwa asilimia 2.9 mpaka 3 hatutaondoa umaskini katika nchi hii, wataalam wote wanajua, ma-*economist* wanajua lazima uangalie kasi ya ongezeko la watu na jinsi uchumi wako unavyokwenda ndiyo maana nasema ya kwamba haya mambo lazima tuyaratibu wote pamoja na Benki Kuu itusaidie kuona namna ya kuratibu ili mambo yaweze kwenda katika hatua inayotakiwa.

Mheshimiwa Spika, la tatu, tunaiomba Serikali kama inawezekana kuona hali ya fedha hasa sarafu ya shilingi mia moja, ukiiangalia sasa hivi imechoka na hasa ukichukua noti ya shilingi mia tano kwa kweli ukifika hata mahali pengine wanazikataaa wafanyabiashara, hata baadhi ya mabenki wanazikataa kwa nini tusitafute utaratibu kama inawezekana maana yake sheria haikatai kwa hela kama shilingi mia tano ikawa na sarafu yake inakuwa ni rahisi kwa sababu shilingi 500 ndiyo iko katika *circulation* sana kwa wananchi wetu wa kawaida kuliko kuwa na noti imechanika mpaka unaogopa kuishika hivi kweli tunashindwa kutafuta *quality paper* kidogo, karatasi ambayo ina *quality* nzuri. Mbona wenzetu katika nchi nyingine unakuta noti zao zote zinang'aa kila wakati hilo tulidhani ya kwamba ni vizuri tukaliangalia.

Pia kasi ya kusaidia *Community Banks* zilizoanzishwa naona kasi kwamba kasi yake ni ndogo sana tuombe kabisa *Community Banks* ambazo zimeanzishwa na kama inawezekana tujue zipo ngapi mpaka sasa maana yake benki miaka mitano iliyopita ilianza kampeni makusudi mazima kuimarisha na kusaidia wananchi waanzishe *Community Banks,* sijui zimefikia wapi. Benki mojawapo ilikuwa ni ya *Mbeya Southern Highlands Bank* ambayo nadhani Mheshimiwa Basil Mramba wakati akiwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya aliianzisha lakini mpaka sasa imesua sijui hata kama imeanza, Benki inasema nini namna ya kusaidia hizo *Community Banks.*

La mwisho, ningeomba kabisa benki itusaidie kuona uwezekano wa namna ya kupunguza makali ya uchumi kutokana na athari ambazo zimejitokeza hapa katikati, kwanza ukame, upungufu wa umeme lakini pia njaa tuone sasa tunafanya nini benki ina mkakati gani kutusaidia ili angalau tusije katika kipindi kinachofuata tukaingia katika matatizo makubwa. Tufuatilie ujambazi ambao umejitokeza na hatua za Serikali za kuanza kupambana na wale ambao walikuwa wakijilimbikizia fedha nyingi katika mabenki kuna athari ya kwamba wengi wataanza kuogopa kupeleka hela zao benki. Benki inasema nini? Benki ina mpango gani? Kwa sababu wakiaanza kuzificha basi hatutakuwa na hela nyingi ambazo ziko *in circulation* watazificha watazitumia kwa kazi nyingine sasa ni vizuri na benki ikatuambia inaweza kuzidhibiti namna gani.

Baada ya kusema hayo nataka kusema kwamba mimi nina imani kabisa Mheshimiwa Waziri amechukua Wizara ambayo anaimudu kabisa na tutampa kila namna ya msaada aweze kufanikiwa katika kazi zake lakini pia tutaomba asimamie kanuni za

namna ya kutawala chombo hiki muhimu katika Taifa letu. Naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi, kwanza niungane na Wabunge wenzangu kumpongeza Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, pamoja na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, kwa kutimiza siku mia moja wakiwa madarakani kwa kazi nzuri sana na sisi tuliokuwa wachezaji wa mpira zamani tunaamini ukifunga magoli mapema dakika za mwanzoni basi utamaliza vizuri. *(Makofi)*

Pili, nimpongeze Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Zakia Meghji pamoja na timu yake ya wataalam katika Wizara na Gavana wa Benki Kuu pamoja na wataalamu wote kwa kutuletea huu Muswada kwa wakati huu tulionao.

Mheshimiwa Spika, wakati na mimi nilipopata Muswada huu kwa mara ya kwanza nilijiuliza maswali mengi sana kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, je, ni lazima tuwe na Bodi katika Benki Kuu kama ilivyo hivi sasa? Je, ni lazima Gavana awe Mwenyekiti wa Bodi hiyo? Na masuala mengine mengi lakini kwa sababu ninayo bahati ya kuwa katika Kamati ya Fedha na Uchumi, maswali haya nilianza kupata majibu kutoka kwenye Kamati kutoka katika maelezo ya Mheshimiwa Waziri pamoja na Gavana mwenyewe hatimaye kwenye semina na baadaye kwenye Kamati tena.

Mimi naomba niungane na Muswada huu katika hili, duniani kote katika ku-*manage* uchumi kuna mambo makubwa miwili, kuna *Monetary Policy* na *fiscal policy* na *fiscal policy* inaangaliwa na Wizara ya Fedha, sasa najaribu kuangalia uwezekano wa Waziri kuwa katika mkutano yeye akiwa kama mjumbe na ule mkutano Mwenyekiti anakuwa mwingine ni jambo ambalo pengine ni gumu kutokea kwa sababu Waziri anayo majukumu na *responsibility* ya Wizara ile kwa asilimia mia moja kwa hiyo analazimika yeye mwenyeye awe Mwenyekiti na ndicho hicho kinachotokea katika chombo chetu cha Benki Kuu ambacho kinapata hii shughuli ya kuangalia hii *Monetary Policy* na ndiyo maana Gavana sasa anawajibika asilimia 100 kwa chombo hiki na ndiyo maana kunakuwa na umuhimu wa yeye kuwa Mwenyekiti wa Bodi.

Mheshimiwa Spika, jambo hili siyo geni kwa nchi yetu wakati tulipokuwa na vyombo nyeti kama hivi kama *NBC* wakati ule Mkurugenzi Mwendeshaji pia alikuwa Mwenyekiti wa Bodi hiyo hasa kwa upande wa *CRDB.* Ni kwa misingi hiyo hiyo ya unyeti wa chombo chenyewe. Kwa hiyo, nilikuwa naomba ndugu zangu Wabunge hoja hii tuielewe katika misingi hii.

Lakini pia ningependa niongelee kifungu cha 7 *section(i)* na ya (ii) ambayo inazungumzia majukumu ya Benki Kuu katika kuendesha hii *Monetary Policy* naki-*quote* kifungu hiki ili niweze kufikia mahali ambapo sasa Benki Kuu kwa sababu inapewa meno zaidi, uhuru zaidi wa kuendesha majukumu yake izibane Benki zetu mbalimbali za biashara na mashirika mbalimbali ya kifedha katika mambo makubwa miwili.

Kwanza, katika kuangalia riba *(interest rates)* kubwa katika mikopo mikubwa sana lakini pia kwa *depositors* wanapewa riba ndogo sana kwa hiyo inakuwa haitoi motisha kwa mtu kwenda kuweka hela zake Benki na kwa hivyo watu wengi wanakuwa na mahela nyumbani na mifukoni na hii ina *disrupt Monetary Policy* yenyewe katika nchi na ina *defeat* hicho kifungu cha 7(i) na (ii).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningeomba Benki Kuu wajaribu kwa namna yoyote ile kuzibana hizi benki kuona kwamba hizi *interest rates* zinaendela kupungua, wanajitetea wanapokwenda kukopesha wateja wadogo wadogo kwamba kwa sababu gharama za kumfuata huyu mteja ni kubwa inabidi tuweke *interest rate* kubwa sana. Lakini ukilinganisha pia kwenye sera yao ya kukopesha wafanyakazi riba ni asilimia 16, 17 mpaka 20 kuna gharama gani ya kufuatilia mkopo wa mfanyakazi kwa mfano mwalimu au mtumishi wa afya au hata mkopo wa Mbunge kwa sababu chombo kinachohusika kinakata na kinapeleka kwenye lile shirika bila malipo yoyote *why such high interest rates?*

Mheshimiwa Spika, *interest rates* pia zinatumika kama chombo katika *Monetary Policies.* Kwa hiyo, mimi nafikiri Benki Kuu wakiweza kucheza na jambo hili tunaweza tukafanya maisha yakawa mazuri zaidi kwa wafanyakazi wetu, maisha yakawa mazuri zaidi kwa wakopaji wetu wadogowadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sina matatizo na wakopaji wakubwa wakubwa kwa sababu wao wanafuatwa maofisini kwao na wafanyakazi wa hizi benki na wanakwenda kujadiliana juu ya *rates* watakazopeana, nafasi hii mkopaji mdogo mdogo hana na mfanyakazi katika ofisi zetu pia hana. Mabenki haya yana *take advantage* kwa sababu wafanyakazi hawana mahali pa kwenda na wana shida ya kujenga na kununua samani kwa hiyo ni lazima watakopa na hii mbaya *its morally corrupt. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kuongelea ni juu ya *payment system* na hili ni jukumu la Benki Kuu pamoja na Wizara ya Fedha. Mimi ningependa kuwapongeza jinsi ambavyo wameweza kupunguza siku katika malipo ya *cheques* na kadhalika lakini nataka kuliangalia hili kwa maana ya jukumu la Benki Kuu kufikiria zaidi kuzisimamia au kusimamia hizi *SACCOS* tuweze kuwa na vyombo vya fedha katika vijiji, kwa nini? Kuna faida kuu tatu. *(Makofi)*

Kwanza, tunataka ku-*draw* hizi hela ziweze zikawa katika mikono ya benki na zisiwe katika majumba ya watu ambapo kama kunatokea majanga tunapata hasara kubwa sana kwa hiyo tunataka kuhamasisha *service* lakini la pili tunataka hawa watu waweze kupata sehemu ya kukopa kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, lakini la tatu, ambalo kwa kweli kwa sababu linawahusu watu wanyonge wanyonge, watu wa Benki Kuu wanaelekea kutoliangalia sana nalo ni kuhusu mishahara ya wafanyakazi wetu, walimu wa shule za Msingi, sekondari, wafanyakazi wa Wizara ya Afya, Misitu na Nyuki ambao wako vijijini wanalazimika kwa mfano kule Mbinga. Mtu anatoka Rwanda mpaka Mbinga ni kilometa 80 na wengine wanatoka kilometa 150 analazimika kuja katika makao makuu ya Wilaya ambapo kuna

benki kuchukua mshahara wake analipa nauli na inabidi alale. Lakini Waziri wa Fedha mshahara wake anaupata kiurahisi unaingia kwenye benki, Gavana anaupata kiurahisi na mimi Mbunge pia naupata kiurahisi sana, sasa kwa nini hawa wenzetu ambao wanatakiwa wapate mshahara wa laki moja anapata *actually* mshahara wa 70,000/= kwa sababu inabidi alipie nauli na malazi na chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Benki Kuu inaweza ikahamasisha au kwa kuwalipa hizi *Banks* ziweze zikafanya hizi *agency* huko au kwa namna yoyote ile au pengine kwa upande wa benki wakaingia mkataba na Benki ya wananchi wa Mbinga ikafanya hii kazi ikaiwezesha ili huyu mfanyakazi wetu apate mshahara wake ule ule na asipate adha ya kutoka kijiji chake kwenda makao makuu ya Wilaya kwa sababu hata usafiri wenyewe katika hizo sehemu ni matatizo makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba tena niipongeze Serikali kwa Muswada huu na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, tunaendelea, sasa namwita Mheshimiwa Abdulkarim Shah na nimepata ombi na nimelikubali la Mheshimiwa Lazaro Nyalandu.Kwa hiyo, huyo ndiyo atatufungia mjadala kutoka kwenye *floor.*

**MHE. ABDULKARIM ESMAIL HASSAN SHAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi kuweza kutoa mawili au matatu ya fikra ambazo mimi ninazo japokuwa nyingi zitakuwa zimeshatolewa na Waheshimiwa wenzangu lakini si vibaya na mimi nikadurusu tu yale ambayo wameyaongea wenzangu.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba kwa furaha kubwa nimpongeze kiongozi wetu mkuu wa nchi Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa ufanisi wake, kwa juhudi zake, kwa kazi yake ambayo ameionyesha na Watanzania wote wameikubali wa ndani na nje ya nchi wa Chama cha Mapinduzi na wasiokuwa wa Chama cha Mapinduzi wote wanafarijika kwa utendaji wake mzuri pia pongezi hizi zimfikie pia kiongozi wetu Serikali ndani ya Bunge Mheshimiwa Edward Lowassa, Waziri Mkuu wetu hongera sana kwa kazi nzuri. Naamini Mawaziri wote na Manaibu pia wanafanya kazi kwa ari ya kuhakikisha kwamba Watanzania wanafaidika na awamu ya nne hii zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na Manaibu Mawaziri, watendaji wote Wizara ya Fedha kwa kazi nzuri wanayoifanya toka Uhuru wa nchi umeanza hadi hii leo. Nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nami nilikuwa nataka nichangie mawili, matatu kama nilivyosema inakuwa kama tunadurusu kwa sababu ni hayo hayo tu. Nakwenda tu kuhusu hili suala dogo si dogo la uhuru wa uongozi mkuu wa *BOT.* Uhuru huu inaelekea kana kwamba wao watakuwa hawafanyi makosa. Lakini wao ni binadamu mimi nafikiria bado hapa paangaliwe lazima kuwe na sehemu wawe na ukomo, lakini na Waziri awe ndiyo msemaji mkuu kabisa wa hii taasisi kwa sababu wakiachiwa Gavana na wenzake basi binadamu wanaweza wakajikwaa, linaweza likatokea lolote Mungu apishe mbali halafu

tutashindwa kumlaumu. Nataka ifahamike kwamba Benki Kuu hii ni ya Watanzania, ni fedha za akina Juma, Omar, Cosmas, Thobias akina Shah, akina Malima na Chacha Wangwe. Sasa tukiwaachia kwamba wao ndio wawe kila kitu wao wasifuatwe wasiwe na mtu ambaye hataweza kuwahoji, hapa kidogo panatisha. Mimi nafikiria hapa paangaliwe na parekebishwe kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waziri lazima ahusike katika maamuzi yatakayofanywa na *BOT,* mimi nafikiria hilo litakuwa la maana zaidi kuliko kuachiwa bodi itakavyoamua ndiyo lazima wapeleke naye ayaridhie yale maamuzi au mawazo watakayoyatoa Magavana au Bodi ili yeye aweze kutoa fikra zake na akithibitisha kwa niaba yetu kwa sababu yeye ndiyo msimamizi kwa niaba ya wananchi na Serikali pale ndani kwa sababu imekuwa kama huu ni muhimili sasa peke yake ambao utakaokuwa unajiamulia kama vile tulivyokuwa Bunge, Serikali, Mahakama sasa wa nne utakuwa *BOT.* Mimi nafikiria hapa kidogo paangaliwe lakini Waziri apewe nguvu ya kuweza pia kuridhia yale ambayo watayaamua na bodi.

Pia kuhusu suala hili la mkopo kwa kuwa hizi ni fedha za Watanzania basi *BOT* lazima iwe inahakikisha na kwa kuwa tuseme *BOT* ndiyo Mtendaji Mkuu, ndiyo msimamizi wa shughuli zote za mabenki basi lazima iwe na malengo maalum ya kutoa motisha za kisera ili mabenki haya yawe na motisha ya kwenda Vijijini. Lakini pia kutoa mikopo na huduma zingine za kifedha kwa wakulima na tena wavuvi kwa sababu wavuvi sasa hivi hawana pa kusemea, hawana kitu cha ku-*guarantee* cha kwenda kukiweka ili waweze kufaidika na mikopo hii ya mabenki iliyokuwa Vijijini.

Mheshimiwa Spika, leo kule kwetu Mafia kuna *NMB* pekee yake. Lakini mvuvi kwa kuwa chombo chake kinaelea baharini pengine kitakuwa na thamani ya zaidi ya shilingi milioni 15 mpaka milioni 20, lakini thamani ile yote inakamatwa na kamba yenye thamani ya shilingi 3,000/= ndiyo dhamana. Sasa utakuta hata uwe milioni 80 zinaelea basi ile kamba ya nanga ndiyo dhamana kubwa ya chombo hiki cha baharini. Sasa wale watu wa mabenki wanasema ahaa kwa mpango huu sisi hatuwezi kukupa mkopo. Kwa hiyo, wavuvi hawapati mikopo.

Mheshimiwa Spika, *BOT* kupitia Serikali basi iwe na sera maalum kwa wavuvi.Wanazungumzwa wakulima, wanazungumzwa wafanyabiashara lakini wavuvi hakuna mtu anayewasemea. Kwa hiyo, naomba hili suala *BOT* iliweke na ihakikishe kwamba katika programu zao zote zinazosemwa basi akiwekwa mfanyabiashara, mkulima na mvuvi atamkwe. Japokuwa wengi wanachukulia wakulima pamoja na wavuvi, mvuvi atamkwe kama mvuvi na mkulima atamkwe kama mkulima. Mikopo ya pembejeo na mvuvi naye apate mashine, nyavu na vitu vingine vinavyohusiana na uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa nataka kuuliza kidogo hivyo ni kitu gani kinachosababisha shilingi yetu kushuka thamani kila kunapokucha, nini tatizo letu? Nini tatizo la shilingi ya Tanzania tumekwama na nini kila siku thamani ya shilingi yetu inashuka ? Serikali ingeweza kutufahamisha tatizo hili. Maana toka nimepata fahamu zangu Kenya inatushinda, shilingi moja ya Tanzania kwa shilingi kumi ya Kenya, leo

shilingi moja ya Tanzania kwa shilingi 14 za Kenya kuna nini? Tuna matatizo gani au *control* zetu zikoje? Nini uwajibikaji wa *BOT* katika kuangalia thamani ya shilingi yetu? Naomba hilo niweze kulifahamu.

Mheshimiwa Spika, ya kwangu ni hayo, lakini naomba niseme kwamba naunga mkono hoja hii mia kwa mia ili na wengine waweze kuchangia na tuweze kupata majibu mazuri ya kuweza kufanikisha.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii muhimu ya mwisho. Kwanza kabisa naomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Singida Kaskazini, kuishukuru sana Serikali kwa usimamizi wao mkubwa kwenye tatizo kubwa la njaa tulilokuwa nalo.

Sisi ambao ni Waheshimiwa Wabunge wa vijijini nafikiri wenzangu watakubaliana na mimi kazi iliyofanywa ni nzuri, tumeokoa maisha ya wananchi na natumaini mvua nzuri zinazoendelea zinatuhakikishia kwamba hatutakuwa tena na tatizo la njaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningeomba niseme mambo mawili, la kwanza, kama walivyosema wenzangu Benki Kuu inawajibu wa kushughulikia *monetary policy* hapa nchini na Serikali kwa kupitia Wizara ya Fedha wana wajibu wa kushughulikia *fiscal policy* ambayo kimadaraka *fiscal policy* ina madaraka mengi tu ambayo wanayo.

Mheshimiwa Spika, mimi ningeomba kusema kwamba kuna ushawishi mkubwa sana kutoka kwa wanasiasa na siyo Tanzania tu dunia nzima kuhakikisha kwamba wanaingilia kwa kadri inavyowezekana utendaji wa kazi wa Benki Kuu. Utendaji wa kazi wa Benki Kuu popote ambako umeingiliwa umekuwa na athari kubwa sana kiuchumi na ningeomba niwaondoe wasiwasi Waheshimiwa Wabunge nimesikia hoja nyingi sana kwamba ukimpa Gavana, madaraka yatapinda, lazima sisi tuwe sauti, lazima kipengele hiki kibadilishwe.

Mheshimiwa Spika, hakuna anayetoa madaraka kwa Gavana wa Benki Kuu, madaraka yanakwenda kwenye *Institution* ya Benki ya Kuu siyo mtu mmoja *than individual* kwamba analimbikiziwa haya madaraka. *Institution* ya Benki Kuu, *Chairman* na *Chief Executive Officer* ni lazima awe Gavana ili apate mamlaka ya kutosha ya kuweza kuifanya kazi ambayo ni *expert work.*

La pili, mimi napendekeza nafikiri iko kwenye Muswada, Wakurugenzi wa Benki Kuu wawe *independent as much as it possible be* na *voting record* zao ziwe wazi kila kunapokuwa na Muswada wa kupigia kura katika Benki Kuu ambao unaathiri uchumi wa nchi sisi tungependa kuona walivyopiga kura. Kwa sababu vyombo vyote vya fedha duniani vinafuata Benki Kuu wataamua nini juu ya *interest rate,* juu ya jambo hili ni chombo ambacho kina-*drive* dunia

Mheshimiwa Spika, tunavyoendelea mbele Afrika Mashariki benki zetu, *Central Bank* za kila nchi ziko kwenye *competition level, investors* wanaangalia *performance* ya Benki ya Kuu ya nchi inayohusika inawawezesha wao kuamua *absorption capacity* ya hiyo nchi ikoje. Na kama tunavyofahamu Tanzania inalaumiwa kwamba uwezo wa Tanzania kutumia fedha ni mdogo. Kwa sababu kwa kila kinachotokea wanasiasa wameishaingilia tayari wamekwenda kama mvua na wakati mwingine ni rahisi sisi kutaka kupata sifa ya kisiasa kwa kuingilia jambo ambalo ni la ki-*expert.*

Mheshimiwa Spika, naweza nikatoa mfano miaka miwili iliyopita ghafla sisi tukiwa Majimboni tukasikia Wizara ya Elimu na Utamaduni wanabadilisha mitaala na watu wengi sana walishangaa, walitufuata ma-*expert* wanaofundisha siku zote, wakasema *this is absolute clause.* Somo hili halipo, haya yameunganishwa. Baada ya muda, *okay* tukasikia Serikali imerejesha ile mitaala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mambo mengine *it can only be expert issue* na ni lazima tuwape nafasi wataalamu ambao tunao katika nchi hii waisaidie nchi iendelee mbele na tusiwazuie njiani na tuwaamini. Kuna njia nyingi sana za kuweza kum-*impish* Gavana kama kweli anaweza akaihujumu nchi. Lakini tusiweke huu Muswada ukawa na dalili za wasiwasi na mashaka utafikiri ni mashirika ya umma ya dhama zetu za miaka ya 1970.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni kwa Benki Kuu yenyewe tuna tatizo hapa Tanzania kwamba gharama ya kufanya biashara katika nchi hii ni kubwa *cost of doing business, bank to bank transaction,* kitu chochote kinachohusu fedha, mwananchi anapoenda kuchukua fedha zake benki anakatwa, anapoweka fedha yake anaibiwa, *basically* analipwa kidogo kiasi kwamba *you can't translate anything than* wizi. Uko katika benki hiyo unataka uweke fedha unakatwa *transaction cost* za ajabu. Sasa Benki Kuu tunapowapa *independence* hii mna kazi ya kujibu kwa wananchi kwamba *cost of doing business in this country* lazima ishuke chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika miaka michache zilipoingia *cell phone* watu wengi walikuwa wanashangaa kwa nini *transaction* zote zilikuwa zinafanyika kwa *dollar* na ziliharibu sana uchumi kwa sababu hata ukipita Manzese, ukipita Singida kule Msange watu wanakwambia na sisi tunatumiwa *message* Mheshimiwa Mbunge anaomba unitumie *dollar,* watu wote maisha yao sasa hivi ni *dollar.*

Mheshimiwa Spika, ukienda Zambia wana *Kwacha, there is no way* unaweza uka-*transact* na *dollar* yako, ukiwa na hiyo *dollar* unafika wanakubadilishia wanakupa *Kwacha.* Ukifika Israel wana *Shekel,* ukifika wanakubadilishia wanakupa *Shekel,* uchumi wa ndani ya nchi ili uwe *successful* ni lazima mtumie sarafu ya nchi *full stop.* Mtapokea *dollar as much as you want* ukipita Uingereza sasa hivi nchi zote za *EU* zinatumia *Euro,* Waingereza bado wamegoma, Bunge la Uingereza limesema hapana. Sasa ukifika Uingereza na *Euro* yako au ukifika na *dollar* unaambiwa badilisha tumia *pound. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na *prestige* ya nchi iko kwenye fedha zake. Tuna *lower down* heshima ya nchi hii kila wakati tunapobadilisha namna watu wanavyofanya kazi

na hizi *Bureau* nyingi sana zilizochipuka za mitaani ndiyo zinazosimango hizi *dollar* kila siku na wanaziondoa wanazipeleka nje. Benki Kuu ina wajibu na wamepewa wajibu wa kusimamia *Bureau de Change* na ukienda kila *Bureau de Change* wanakwamba kabisa kuna karatasi imeandikwa inasema *please demand list upon,* wameandika sana kwa Kiingereza *as if* kila mtu anaongea Kiingereza. Tafadhali *demand your list* unapo-*change* fedha, hakuna hata mtu mmoja anaye-*demand* risiti na wale watu hakuna chochote kilichofanyika. Benki Kuu mnaweza mkatuma makachero 50 wakaenda na *dollar* zao wakazibadilisha wasipopewa risiti wale watu mnawapiga faini, *it does'nt take long* kuhakikisha kwamba hii sheria mna-*implement* na mimi ningeomba muwe na meno, ningeomba muwe *independent* na ningeomba niwambie Waheshimiwa Wabunge wenzangu ninafikiri tusiwe na shaka tuwape wataalamu wetu nafasi ya kuiendesha nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kuleta Muswada huu muhimu.

Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Pamoja na kuunga mkono hoja hii napenda kuchangia maeneo yafuatayo:-

Moja, kwa kuwa riba ya mabenki ya biashara ni kubwa sana na kufanya wananchi kushindwa kuchukua mikopo, hivyo nashauri Benki Kuu kusimamia mabenki hayo ili kupunguza riba na kulegeza masharti ya mikopo.

Pia Benki Kuu isimamie mabenki haya kupeleka huduma za kibenki vijijini ambako watu wengi wanaishi na hasa wakulima, kama vile Kibakwe, Rudi, Pwaga, Mima Wilaya Mpwapwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO:** Mheshimiwa Spika, natanguliza kuunga mkono hoja hii. Kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake, Katibu Mkuu , Gavana wa Benki Kuu na wasaidizi wenu kwa mambo yafuatayo, kazi nzuri ya siku zote, uamuzi wenu wa kuleta Muswada wenye shabaha ya kuimarisha utendaji wa Benki Kuu na kusukuma maendeleo ya uchumi wa Taifa letu na kwa maelezo ya ufasaha ndani ya Muswada na ya ziada katika semina mliyotufanyia WaheshimiwaWabunge.

Mheshimiwa Spika, ni kweli Muswada huu utaongeza ufanisi katika utendaji wa Benki Kuu. Lakini ninayo machache ambayo naamini yatasaidia kuuboresha Muswada huu, moja, sina kipingamizi dhidi ya Gavana kuwa Mwenyekiti wa Bodi kwani miaka yote ilikuwa hivyo na Benki nyingi duniani utaratibu ndiyo huo.

Pili, pendekezo la kuwa na Manaibu watatu nalikubali kwa sababu chini ya sheria hii mpya shughuli za sera za kifedha *(monetary policy),* udhibiti wa mabenki na kwa kiasi fulani shughuli za *fiscal policy* na utunzaji wa fedha za Serikali *(Banker of the Government)* ni pana na zinahitaji *specialization.*

Nne, lakini kwenye *section 11(3)* nashauri yaongezwe maneno: *"Two of which members shall be the non-executive members."* Sababu Benki yenyewe itakuwa na wajumbe wanne Gavana na Manaibu watatu. Hivyo maamuzi yao ambayo naamini yatatokana na *"internal briefings/consultations,"* basi ndiyo maamuzi ya Bodi.

Tano, *section 11(8)* tayari inaweka msingi wa *equal votes.* Kwani ukiondoa hao *Ex-officials,* Wakurugenzi wanabaki nane. Kama nilivyosema awali kwa kawaida, kabla ya kikao Gavana lazima awe na *Internal Meeting* na wasaidizi wake. Hivyo, msimamo wao kwenye Bodi utakuwa mmoja. Wao watakuwa wanne na wale wa nje watakuwa nne. Tayari tunakaribisha kura ya turufu ya Gavana *(Gavana's casting vote).*

Sita, kuhusu udhibiti wa mabenki na taasisi za fedha nakubaliana na yote yaliyomo katika *section 44-48* hasa vifungu 48(1) na (2) vinavyoongelea *credit reference system* na *credit reference data bank.* Nawapongeza sana kwa utaratibu huu maana utazuia yafuatayo:-

(a) Ukopeshaji holela ambao matokeo yake ni kwa benki hizo kuwa na madai yasiyolipika *(bad debts)* ambavyo ni vianzo vya mabenki kufilisika.

(b) Ubadhirifu wa fedha unaofanywa kwa njama baina ya watendaji na wafanyabiashara wahuni kama ilivyotokea kwenye Benki ya Azania wakati ule ikiitwa *First Adili Bankcorp.* Muhuni mmoja akatoroka na mamilioni ya fedha, tena za kigeni. Nawapongeza sana kwa hatua hii.

Saba, lakini sikubaliani na *section 48(9)* inayomtaka mteja wa benki atoe kibali kimaandishi. Akikataa maana yake nini. Sharti hili liondolewe.

Nane, *section 51* inaitaka Benki ibweteke. Kwa nini kiwango cha chini kiwe miezi nne eti kwa kuwa ndiyo kigezo cha Kimataifa. Tayari tumefikia akiba ya miezi tisa, bora tungesema iwe miezi sita. Tusiwekee *easy target,* tutabweteka.

Tisa, *section 51(2),(3)* na (4) sikubaliani na maneno *"(2) ..... at a request of the Bank, (3) ..... at a request of the Bank* na *(4) .... the Bank may impose on the relevant bank ...."*

Maneno haya yataifanya *BOT* isiwe na meno dhidi ya mabenki kama hawa wanaombwa kwa nini katika 57(5) tuna-*impose a penalty?*

Kumi, mwisho na nashauri kati ya 71(1) uingizwe mwaka 1995 baina ya maneno *Act* na *is.*

**SPIKA:** Ahsante sana. Kwa kukumbushana tu kwa mujibu wa kanuni mtoa hoja pamoja na wasaidizi wako Mheshimiwa Waziri unao muda wa saa moja wa kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge. Kwa hiyo, naanza kwa kumwita Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kutoa mchango wangu katika maeneo machache yaliyozungumzwa na Waheshimiwa Wabunge na mengi yatajibiwa na mtoa hoja mwenyewe.

Hoja namba moja ambayo ilizungumzwa na Wabunge wengi ni inayoitaka Benki Kuu kupanga viwango vya riba kwa mikopo itolewayo na mabenki ya kibiashara.

Mheshimiwa Spika, Serikali kimsingi inakubaliana na hoja za Waheshimiwa Wabunge kuhusu tatizo la riba katika mabenki. Tatizo la viwango vya juu vya riba za mikopo ni la muda mrefu na lilianzia tangu miaka ya 1990 na limezungumziwa pia na idadi kubwa ya Waheshimiwa Wabunge. Ni vyema ikakumbukwa kwamba viwango vya riba za mikopo ya muda mfupi vimeweza kushushwa kutoka wastani wa asilimia 30.7 mwaka 1996 hadi wastani wa asilimia 15.7 mwishoni mwa mwaka 2005. Katika kipindi hicho hicho riba kwa amana za mwaka moja ilipungua kutoka asilimia 16.3 mpaka asilimia 7.7 na hivyo tofauti kati ya riba ya mikopo na riba ya amana yaani *interest rate spread* imeshuka kutoka asilimia 15 mwaka 1996 mpaka asilimia 8.6 mwishoni mwa mwaka 2005. *(Makofi)*

Hata hivyo, viwango vya riba havijaweza kushuka zaidi sambamba na mfumuko wa bei kwa vile Benki Kuu inalazimika kuuza kiwango kikubwa cha dhamana ya Serikali yaani *liquidity papers* ili kuzuia kuongezeka kwa mfumuko wa bei. Hatua hii imesababisha riba katika soko la dhamana la Serikali kuwa juu na hivyo kusababisha riba za mikopo kubakia juu. Pamoja na mwenendo huu si busara kwa Benki Kuu kupanga viwango vya riba kwa mabenki ya biashara kwa vile ni kinyume na mwenendo wa mfumo wa soko huria.

Hata hivyo, Benki Kuu chini ya awamu ya pili ya mageuzi katika sekta ya fedha inapanga mikakati kukabiliana na matatizo yanayosababisha riba kuwa juu ikiwemo kuimarisha taasisi na taratibu za kisheria ili kuboresha huduma za sheria na Mahakama ambazo zimechangia kwa kiasi fulani kuongeza gharama za mabenki.

Mheshimiwa Spika, aidha, hatua za Serikali kuimarisha miundombinu ya kiuchumi zitasaidia kupunguza gharama ya uendeshaji wa mabenki na hivyo kuyawezesha kuongeza riba za amana na kupunguza riba za mikopo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo haya Serikali itaandaa utaratibu wa kukutana na wadau mbalimbali wakiwemo Benki Kuu, Mabenki ya Biashara na wadau wengine kuangalia jinsi ya kushughulikia suala hili ili kuwasaidia wananchi wa kawaida kama vile wakulima, wanawake na vijana ili waweze kupata mikopo kwa riba nafuu. *(Makofi)*

Mheshimwia Spika, hoja ya pili ambayo ilizungumziwa sana na Waheshimiwa Wabunge ni msukumo unaotolewa na Serikali na Benki Kuu juu ya *Micro- Finance* na maendeleo ya *SACCOS* nchini.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge walihoji juhudi za Serikali na Benki Kuu juu ya suala zima la *Micro - Finance* na kwamba jitihada zifanywe ili kuhakikisha kuwa huduma za kibenki zinatolewa mpaka Vijijini na *SACCOS* ziimarishwe na ikiwezekana *SACCOS* hizo zipewe mikopo na Benki za Biashara bila sharti la dhamana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sera ya Taifa ya huduma za kifedha kwa wateja wadogo wadogo yaani *National Micro- Finance Policy* ilipitishwa na Serikali mwezi Mei, 2000 ikiwa na madhumuni ya kuweka msingi kwa ajili ya kujenga mfumo imara na wenye tija wa huduma za kifedha kwa wateja wadogo wadogo hapa nchini ili kuchangia katika kukuza uchumi na kupunguza umaskini. Mojawapo ya malengo ya sera hii ni kuhakikisha kwamba *SACCOS* zenye ukubwa wa kiwango kilichoainishwa kwenye kanuni za usimamizi wa *SACCOS* za mwaka 2005 zinasimamiwa kwa kanuni zinazojali usalama wa fedha za wanachama na wateja wao.

Vile vile sera hii ina mategemeo kwamba *SACCOS* zinazolengwa kwenye kanuni hizo zitakua na hatimaye kupata hadhi ya kuwa Benki za Jumuiya au kuungana na kuwa Benki za Ushirika au kushirikiana na Asasi nyingine za fedha kama inavyofanyika hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, kanuni za usimamizi wa makampuni ya *Micro- Finance* na shughuli za *Micro Finance* kwa mabenki na *SACCOS* za mwaka 2005 zilizotengenezwa chini ya Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 1991 zimeipa jukumu Benki Kuu la kutoa leseni na kusimamia vyombo hivi vya fedha. Hivi sasa Benki Kuu inatoa ushauri wa kuanzisha vyombo hivyo vya fedha kwa misingi endelevu na inapokea maombi ya leseni za Asasi za Fedha zinazotoa mikopo midogo midogo na kusimamia shughuli zake.

Kuhusu mahusiano ya kibiashara kati ya mabenki na *SACCOS* napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba hivi sasa baadhi ya Benki za Biashara zimeingia katika taratibu za kukopesha *SACCOS* bila kuweka sharti la dhamana. Benki za Biashara zinaruhusiwa kukopesha hadi asilimia 5 ya mtaji wa benki kwa mtu mmoja mmoja, Shirika, Kampuni, *SACCOS* au vikundi vya Jumuiya bila kuwepo na sharti la dhamana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maombi ya *CRBD* ya kupata idhini ya kuanzisha chombo chini ya Benki hiyo kwa ajili ya kutoa mikopo midogo midogo yaani *CRDB Micro Finance Company Limited* yalipokelewa na yalishughulikiwa na Benki Kuu chini ya utaratibu uliopo. *CRDB* imeishapewa maelekezo na Benki Kuu tokea tarehe 3 Mei, 2005 kuhusu hatua za kuchukua ili iweze kutimiza masharti yaliyowekwa kwenye miongozo na taratibu hizo juu ya uanzishwaji wa chombo kinachokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, naomba Waheshimiwa Wabunge wazingatie kuwa wakati *CRDB* ikiendelea kufanya juhudi za kukidhi matakwa ya sheria na taratibu za uundwaji wa chombo hicho leseni waliyonayo hivi sasa yaani *Commercial Bank License* inawapa *CRDB* nafasi na fursa ya kutoa mikopo midogo midogo kwa wananchi Mijini na Vijijini kama wanavyofanya hivi sasa. Kwa hiyo, benki ilivyo hivi sasa inaruhusu kutoa mikopo ya Micro-Finance mpaka Vijijini.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuwa karibu na Benki Kuu na Benki za Biashara na Asasi za Fedha zitakazoelekeza juhudi zake katika kuhudumia wananchi Vijijini na Mijini.

Hoja ya tatu ambayo ilizungumzwa sana ni uuzwaji wa hati fungani za manispaa yaani *Municipal Bonds.*

Mheshimiwa Spika, suala la kuuza hati fungani za Manispaa yaani *Municipal Bonds* limeainishwa kwenye Awamu ya Pili ya Mageuzi ya Sekta ya Fedha yaani *Second Generation Financial Sector Reform.* Kamati ya kuratibu mapendekezo ya kuanzisha uuzaji wa hati fungani za Manispaa yaani *Municipal Bonds* imekwishaundwa chini ya Uenyekiti wa Mamlaka ya Masoko ya Dhamana na Mitaji yaani *Capital Markets and Securities of Authority.* Kamati hii inalifanyia kazi suala hili na mapendekezo yanategemewa kutolewa hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii mia kwa mia. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kutoa shukrani za dhati kwako kwa kunipa nafasi wakati huu ili niweze kujibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge. Napenda pia kuchukua nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia Muswada huu ama kwa kuzungumza au kwa kuandika au mara nyingi kutusimamisha pale nje na kutueleza mawazo yao. Kwa hiyo, kwa wote nasema ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwatambua Waheshimiwa Wabunge hawa kwa majina. Kwanza, waliochangia kwa kuzungumza Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda, Mbunge wa Handeni ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Wawi na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani.

Wengine waliochangia ni Mheshimiwa Elisa David Mollel, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe, Mheshimiwa Dr. Raphael Masunga Chegeni, Mheshimiwa Wilson Mutagaywa Masilingi, Mheshimiwa Omar Sheha Mussa, Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa John Momose Cheyo, Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mheshimiwa Paschal Degera na Mheshimiwa Gosbert Blandes. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Yono Kevela, Mheshimiwa Suleiman Kumchaya, Mheshimiwa Chacha Zakayo Wangwe, Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi, Mheshimiwa Balozi Hamis Suedi Kagasheki, Mheshimiwa Richard Said Nyaulawa, Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, Mheshimiwa Prof. Idris Mtulia, Mheshimiwa Ruth Blasio Msafiri, Mheshimiwa Felix Mrema, Mheshimiwa William Mganga Ngeleja, Mheshimiwa Castor Raphael Ligallama, Mheshimiwa Kabuzi Faustine Rwilomba, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Susan Lyimo, Martha Mlata, Mheshimiwa Dr. Lucy, Nkya, Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, Mheshimiwa *Eng.* Stella Manyanya, Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Mheshimiwa Lazaro Nyalandu na Mheshimiwa Mustafa Mkulo ambaye ni Naibu Waziri wa Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna wengine ambao wamechangia kwa maandishi nao ni Mheshimiwa George Malima Lubeleje na Mheshimiwa Athumani Said Janguo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba radhi kama kuna wengine ambao wamechangia labda kwa maandishi hasa kama sijaandika majina yao, basi wanaweza kuniletea vikaratasi nitawataja kabla sijamaliza.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza napenda kutoa shukrani za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi kwa kuunga mkono Muswada huu. Aidha, napenda kutoa shukrani zangu kwa Kambi ya Upinzani nao pia kwa kuunga mkono Muswada huu. Naahidi kwamba Serikali itafanyia kazi maelekezo yote na pia mawazo mazuri yaliyotolewa na Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi na pia ya Kambi ya Upinzani. Lakini pia mawazo yote na mapendekezo yote ambayo yametolewa na Waheshimiwa Wabunge yatakuwa dira kwetu ya kuweza kufanyia kazi katika utekelezaji wetu wa bill hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa kuelezea hoja mbalimbali ambazo zimezungumziwa. Mojawapo ambayo imezungumzwa kwa muda mrefu na Waheshimiwa Wabunge wengi ni suala kwa nini Benki Kuu ipatiwe uhuru na kwa nini Gavana wa Benki Kuu awe Mwenyekiti wa Bodi.

Mheshimiwa Spika, wengi wa Waheshimiwa Wabunge wamezungumza suala hili napenda kueleza yafuatayo, suala la uhuru wa Benki Kuu limekuwa msingi wa majadiliano ya Muswada huu na ninashukuru sana kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge wengi kwanza wametambua umuhimu wa chombo hiki nyeti kufanya kazi zake bila ya kuingiliwa hususan katika kubuni na kusimamia sera za fedha. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Dr.Abdallah Omar Kigoda, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi kwa kuweza kulielezea vizuri suala hili.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, ningependa kufafanua zaidi kuhusu uhuru huu ni wa namna gani. Kwa sababu kumekuwa na wasiwasi mkubwa sana na suala zima la

uhuru na suala zima la uwajibikaji. Kwa hiyo, ningependa kusema yafuatayo, uhuru ambao Benki Kuu inapewa na Muswada huu ni katika kutekeleza majukumu yake ambayo ni kubuni na kutekeleza sera ya fedha yaani *monetary policy.* Kwa hiyo, uhuru katika kubuni haya katika sehemu yao ya *monetary policy,* pia kusimamia mabenki na asasi zingine za fedha.

Mheshimiwa Spika, tutakapokuja kwenye Muswada wa pili pengine hili litaeleweka kwa vizuri zaidi katika suala nzima la kusimamia mabenki pamoja na asasi mbalimbali za fedha. Pamoja na hayo kutoa ushauri kwa Serikali katika kubuni na kutekeleza sera za Bajeti na sera zingine za uchumi. Sasa ili kuwezesha Benki Kuu kutekeleza majukumu yake bila ya kuingiliwa katika *monetary policy* kama nilivyosema imependekezwa kuwa pawe na bodi ya wajumbe 10, wawili kati yao wakiwa Makatibu wa Wizara ya Fedha, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao wao hawatakuwa na uwezo wa kupiga kura endapo italazimika maamuzi yafanyike kwa kupiga kura. Wanne kati yao watatoka nje ya Benki Kuu na hao watateuliwa na Waziri wa Fedha na wanne watoka ndani ya Benki Kuu yaani Gavana pamoja na Manaibu Gavana watatu ambao hawa wote watateuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unaipatia bodi madaraka ya kufanya maamuzi yote kuhusiana na majukumu ya Benki Kuu. Kwa hiyo, katika *monetary policy,* siyo katika *fiscal policy* ambalo ni jukumu la Serikali, katika *monetary policy* wao wanakuwa na madaraka haya.

Mheshimiwa Spika, imependekezwa kuwa Gavana wa Benki Kuu ndiye awe Mwenyekiti wa Bodi. Pendekezo hili ni muhimu ndugu zangu kwa vile siyo vizuri kuwa na watu wawili yaani Gavana na Mwenyekiti wa Bodi kugawana majukumu ya uwajibikaji. Chombo cha Benki Kuu ni chombo ambacho ni nyeti na chombo ambacho mara nyingine kinahitaji maamuzi ya haraka na pia maamuzi ambayo ni mazito kwa kila siku. Kwa kweli huu ndiyo msingi wa uhuru ambao tunauzungumza. Utaratibu wa Gavana kuwa Mwenyekiti wa Bodi kwa kweli umekuwepo tangu kuanzishwa kwa Benki Kuu mwaka 1965 na hapajawahi kuwa na matatizo yoyote yale. Isitoshe utaratibu huu ndiyo unaotumika katika Benki Kuu zingine karibuni nchi zote ulimwenguni. Kwa hiyo, baada ya kutafakari kwa kweli Serikali inaona ni busara kuendelea na utaratibu huu.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu pia una vipengele ambavyo unavitaka Benki Kuu kuwajibika kwa Serikali kwa sababu suala zima la uwajibishaji kwa Serikali ni muhimu kwa Bunge na pia kwa wananchi.

Kwanza kabisa ni kupitia uteuzi wa Gavana, Manaibu Gavana na Wajumbe wa Bodi. Pili, ni kwa Benki Kuu kutatua kushauriana na Waziri wa Fedha katika utekelezaji wa sera hususan masuala mazima ya *exchange rate* ambayo mmeizungumza hapa sana.

Tatu, Benki Kuu inatakiwa kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa sera ya fedha yaani hiyo *Monetary Policy Statement* mbele ya Bunge mara mbili kwa mwaka. Kila

kipindi cha miezi sita inabidi kutoa taarifa Bungeni ya *Monetary Policy Statement* na pia kuwajibika kwa Kamati ya Fedha na Uchumi kwa maana hiyo.

Nne, kutoa taarifa mbalimbali kuhusu mwenendo wa uchumi kwa wananchi kupitia ripoti zake za kila mwezi, kila mwezi Benki Kuu inatayarisha ripoti, kila robo mwaka na kila mwaka na tano, kwa hesabu za Benki Kuu kukaguliwa na *Controller and Auditor General.*

Kwa hiyo, huu ndio uhuru tunaozungumza kwamba hesabu zao pia zitakaguliwa na *Controller and Auditor General* kama vile hesabu zinazofanywa za Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maamuzi ndani ya Bodi ili quorum ipatikane na hili wengi wamelizungumza na mawazo pia mbalimbali yametolewa. Hili tunalosema ni lazima angalau Wajumbe wawili toka nje ya Benki wahudhurie kikao hiki hata pale ambapo patahitajika kikao cha dharura cha Bodi. Nitakumbuka hili tumelizungumza sana kwamba kikao cha dharura cha namna gani, mbona watu wapo na Serikali imekubaliana na mawazo yenu. Kwa hiyo, Muswada huu umefanyiwa marekebisho ili angalau basi mjumbe mmoja toka nje ya Benki ahudhurie kile kikao ili maamuzi yanayotolewa yaweze kutambulika kisheria. Hii kwa hivyo itatofautisha yale ambayo mliyokuwa mnazungumza kwamba wanaweza kukaa Menejimenti wakaamua mambo yakapita na kadhalika. Serikali imetafakari na kukubaliana na mawazo yenu na kuona kwamba hii itasaidia kutofautisha maamuzi ya Menejimenti na maamuzi ya Bodi.

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili, ni mgawanyo wa hisa na mtaji wa Benki Kuu kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Muungano wa Tanzania. Jambo hili limetolewa maelezo mazuri, Waheshimiwa Wabunge mbalimbali lakini pia na Mheshimiwa William Shellukindo na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wengine. Hasa kwa kuwa Tume ya Pamoja ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeshaanza kazi zake Serikali inashauri kwamba tuiachie ifanye kazi zake ambazo ni pamoja na ushauri kuhusu mgawanyo wa mapato kati ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania juu ya mtaji wa Benki Kuu, Mashirika na vyombo vingine vya Muungano. Kwa hivyo *GEFC* imeshaanza kazi tunasema wacha wamalize kazi yao halafu suala hili litawekwa juu ya meza wazi wazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa ni juu ya Benki Kuu iweke mikakati kuwasaidia wananchi wa kawaida kukopa katika Mabenki kwa ajili ya ujenzi wa nyumba na shughuli za kilimo. Ni kweli kwamba japo kumekuwepo na mageuzi makubwa katika sekta ya fedha suala la upatikanaji wa mikopo ya muda mrefu kwa ajili ya ujenzi wa nyumba na shughuli za kilimo bado halijapatiwa ufumbuzi. Ni kweli kama watu walivyosema hapa kujenga nyumba kwa *cash* ni matatizo makubwa. Kwa hiyo, ni muhimu kuwa na mikopo ya nyumba. Aidha, viwango vya juu vile vya riba inawafanya wenye miradi mizuri pia kushindwa kukopa, Naibu Spika, pia ameelezea suala zima hili la riba.

Vile vile Benki imekuwa na wasi wasi kukopesha wateja wapya kwa kuwa hawana *credit history* na pia Mahakama na mfumo wa sheria zetu kwa ujumla

zinawalinda zaidi wakopaji kuliko wakopeshaji. Sasa napenda kusema kwamba haya ni matatizo ambayo yameonekana suala la *(mortgages)* mikopo kwa ujenzi wa nyumba itabidi kwa kweli pia kuna baadhi ya sheria zetu ziweze kufanyiwa mabadiliko. Kwa sababu unaweza wewe ukakopa wakati ukifika wa kulipa ukaenda Mahakamani na *court injunction* basi usilipe tena. Mtu mwingine ambaye atapata mkopo ule inakuwa hawezi kupata mkopo.

Kwa hiyo, kuna sheria ambazo itabidi zifanyiwe kazi kuzirekebisha ili utaratibu huu uweze kufanyika. Napenda kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali imebuni mkakati mpya wa kushughulikia changamoto zilizosalia katika sekta ya fedha na hivyo kuchangia katika suala zima la kupunguza umaskini. Mkakati huu unajulikana kama Awamu ya Pili ya Mageuzi katika Sekta ya Fedha yaani *Second Generation Financial Sector Reform.* Labda kwa kifupi ningependa kusema kwamba mkakati huu ni pamoja na mambo mengine yafuatayo ambayo yanalenga.

Kwanza katika kuimarisha Taasisi na taratibu za kisheria ili kuondoa vikwazo vya utoaji wa mikopo na kuboresha huduma za sheria Mahakamani, lazima vikwazo hivyo viondolewe ili Benki hii iweze kukopesha katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, pili, kuimarisha sekta ya pensheni ili Mifuko ya Pensheni iweze kuchangia katika upatikanaji wa mikopo ya muda mrefu. *(Makofi)*

Tatu, kutunga sera na taratibu za kisheria kuhusu utoaji wa mikopo ya muda mrefu ikiwemo mikopo ya nyumba yaani *Housing Finance,* mikopo ya kukodisha mitambo na vitendea kazi *(Leasing Finance)* na kuanzisha Taasisi ya kutoa mikopo ya muda mrefu (*Development Financial Institution).*

Nne, kuimarisha mpango wa dhamana kwa ajili ya mikopo ya biashara ndogo ndogo *(SME credit guarantee scheme)* na kuanzisha mpango wa kudhamini mikopo ya muda mrefu (*Development Finance Guarantee Facility)* kwa ajili ya miradi ya kati na miradi mikubwa, jambo hili Waheshimiwa Wabunge mmelizungumza sana ili kuwaondoa wananchi wa kipato cha chini waweze kupata mikopo na kwa maana hiyo waweze kuondokana na umaskini ambao waliokuwa nao.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni kwa nini Benki Kuu iagize dhahabu kutoka nje ya nchi. Kifungu 53 (1)(a) cha Muswada labda niseme kwamba nia yake sio kuruhusu Benki Kuu kuingiza dhahabu iliyo ghafi yaani *raw gold.* Hapa tunapozungumza ile dhahabu iliyosafishwa yaani *gold bullion.* Kwa hiyo, tunapozungumza kuingiza na kutoa ni kwamba dhahabu hii au hii *gold bullion* ni kama sarafu kwa hiyo badala ya mtu kulipa labda kwa *dollar* au *Euro* anaweza kulipa kwa dhahabu hii safi au *bullion.*

Pia nchi ikiwa na dhahabu hii ambayo bullion nao pia badala ya kulipa kwa fedha kwa dola na kadhalika itakuwa unaweza kulipia kwa kutumia dhahabu. Kwa hivyo, dhahabu inayozungumzwa sio ile dhahabu chakavu lakini dhahabu inayozungumzwa ni *fine gold* ambayo ni tofauti na hii ambayo tunayoizungumza. Hasa kwa hivyo malipo ya dhahabu yanaweza kufanya moja kwa moja, kupeleka katika akaunti za Benki zilizoko nje au kwa kuileta katika Ofisi za Benki Kuu hapa nchini ambapo huwa inahifadhiwa katika sehemu maalum inayoitwa *Gold Volt.* Kama nilivyosema katika biashara za

Kimataifa malipo yanaweza kufanyika kutumia dhahabu iliyosafishwa Dola ya Kimarekani na kadhalika. Malipo kwa kutumia dhahabu uiwezesha pia nchi kuongeza akiba ya fedha za kigeni sawa sawa na nchi inavyolipwa kwa kutumia Dola za Kimarekani na kadhalika. Kwa hiyo, hili nalo pia ni suala ambalo nilitaka liamuliwe kwamba tuweze kuendelea kuwa na dhahabu au gold bullion kwa maana ya kununua au kuuza.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni juu je, dhahabu inayochimbwa hapa nchini imesaidiaje maendeleo ya nchi kwa mfano ujenzi wa barabara? Napenda kusema kwamba kuhusu mchango wa dhahabu katika maendeleo ya nchi na tunajua kwamba hivi sasa suala hili limekuwa linazungumzwa, linafanyiwa kazi na Wizara husika ili kuangalia au kutathmini upya mchango wa dhahabu katika uchumi wetu ni pamoja labda na kuangalia sheria ile ya madini. Kwa hiyo, hili nalo pia linaangaliwa na Serikali kwa kupitia Wizara husika.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu kushuka kwa thamani ya shilingi. Hapa nimezungumza kwamba wakati huu kwamba shilingi yetu imezidi kuporomoka siku hadi siku. Waheshimiwa Wabunge kadhaa waliohoji kwa nini Dar es Salaam shilingi inashuka wakati ambapo uchumi wa nchi unakua. Vile vile walihoji kwa nini wafanyabiashara wanaanza kutumia dola za Marekani badala ya shilingi ya Tanzania kwa malipo ya bidhaa na huduma nchini.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuanguka kwa shilingi kumechangia katika kuwafanya baadhi ya wafanyabiashara kutumia dola za Kimarekani badala ya shilingi katika kupanga bei za bidhaa na huduma na kwa malipo nchini. Wafanyabiashara hao wanafanya hivyo kinyume cha taratibu isipokuwa kwa maeneo yaliyokubaliwa kisheria kwani fedha halali kwa malipo nchini ya *illegal tender* kwa mujibu wa sheria ni shilingi ya Tanzania. Hivyo Serikali inazingatia maoni ya Waheshimiwa Wabunge kuhusu suala hili na inajitahidi kulifuatilia. *(Makofi)*

Lakini pia niseme kuhusu kushuka kwa thamani ya shilingi kunatokana hasa hasa na uwezo wetu mdogo wa kuuza bidhaa na huduma nje ya nchi kuzalisha nchini kwa sababu pale ambapo utazalisha nchini kwako utathamini fedha yako ya Tanzania kwa sababu fedha ile ambayo utaitumia pale. Lakini kama wewe unaingiza siku zote utahitaji fedha za nje kwa maana ya dola ya Kimarekani na kadhalika kununua vitu ambavyo vinatengenezwa nchi nyingine.

Kwa hiyo, thamani ya fedha zetu itaweza kuimarika tukiweza kuimarisha uzalishaji wetu kwa mfano katika viwanda, kilimo na kadhalika na kupeleka vitu ambavyo vyenye thamani. Nikitoa mfano mmoja, mfano wa hapa nchini tunakuta magari mengi ya *Toyota,* magari haya yanatengenezwa Japan kwa hiyo fedha ya *Yen* kwa Japan inakuwa na nguvu zaidi sababu ndiyo inayotumika pale nchini kwa ajili ya uzalishaji.

Kwa upande wa Tanzania sio hivyo kwamba tunahitaji dola ili tuweze kuleta vitu nje lakini kama tungekuwa tunazalisha hapa tungehitaji fedha ya Tanzania na kwa maana hiyo fedha yetu ingekuwa na muhimu au strong zaidi kuliko fedha zingine. Kwa hiyo, nafikiri suala hili pamoja na matatizo na ambayo tumesema tutayaangalia lakini suala

zima la uzalishaji na kuongeza uzalishaji katika Taifa ndilo ambalo suala la umuhimu mkubwa katika kuimarisha uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala juu ya uchakavu wa sarafu na noti. Benki Kuu inaandaa utaratibu mzuri ambao utahakikisha noti chafu na sarafu zilizochakaa zinaondolewa kwenye mzunguko kutoka kwa wananchi. Utaratibu huu ni pamoja na kuangalia uwezekano wa kufufua tena vituo vya Benki Kuu vya noti na sarafu katika Kanda yaani *BOT Safety Custody Centres.* Pamoja na hatua hizo Benki Kuu inahimiza Benki ya Biashara kuwasilisha sarafu na noti chakavu kwenye ofisi za Benki Kuu ili zibadilishwe. Kwa hiyo, kilio cha wananchi kupitia nyie Waheshimiwa Wabunge, *BOT* imekisikia na utaratibu huu utaanza mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu Muswada utamke bayana kwamba mmojawapo wa Manaibu Gavana awe mwanamke. Mimi naamini na sote tunaamini kabisa kwamba wako wanawake wengi sana wenye uwezo wa kuwa Naibu Gavana au hata kuwa Gavana. Lakini tunaelewa kuwa pia kwamba katika *Constitution* yetu na hasa kupitia Wabunge imeweka wazi wazi kwamba asilimia ya Wabunge itakuwa kiasi gani. Sasa mimi nafikiri kwamba kwa msimamo huo pengine itakuwa vizuri tuiachie Mamlaka teuzi itumie busara yake badala ya kuweka suala hili katika sheria. Na unaweza kuona kwamba Mamlaka husika iliyokuwa sasa ni kwamba ina msimamo mkubwa kwa upande wa akinamama. Lakini jambo la umuhimu na sote tunaelewa ni uwezo sio suala tu la mwanamke au mwanamume ni suala la uwezo. Kwa hiyo, pale ambapo nina hakika kwamba ataonekana mwanamke mwenye uwezo basi naamini kabisa kwamba hili litaweza kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine kwa nini sheria imekataza Waheshimiwa Wabunge kuwa Wajumbe wa Bodi ya Benki Kuu. Kipengele hiki si kipya kwa kuwa kimeainisha katika Sheria ya Benki Kuu ya mwaka 1995. Itakumbukwa kwamba utaratibu huu wa kutokuwa na Wabunge kwenye Bodi ya Benki Kuu ulianza sambamba na uanzishaji wa Mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa mwaka 1992, lengo likiwa ni kutochanganya siasa na maamuzi ya Benki kama ilivyo kwa Makatibu Wakuu ambao hawatapiga kura katika Bodi.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni juu ya mgawanyo wa ajira za Benki Kuu katika ngazi za uongozi. Idadi ya wafanyakazi wa Benki Kuu ambao wanatoka Zanzibar ni 68 kati yao 55 wanafanya kazi katika Tawi la Benki Kuu la Zanzibar na wengine 13 wanafanyakazi Makao Makuu ya Benki Kuu pamoja kwenye Matawi yake mengine yaliyopo Tanzania Bara. Idadi hii ya wafanyakazi ni asilimia 5.1 ya wafanyakazi wote wa Benki Kuu ambao ni 1,331. Aidha, kuhusu nafasi za uongozi katika Benki, ajira kwa kweli katika ngazi hii inazingatia elimu, uwezo na uzoefu bila kujali mfanyakazi anatoka upande gani wa Muungano. Naamini kabisa kwamba ndugu zetu wa kutoka Zanzibar nao pia watajitahidi ili wawepo katika nafasi hizi.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni juu ya ujuzi wa kazi wa muda wa miaka 15 ili kuwezesha mtu kuteuliwa katika nafasi ya Gavana kwamba ni muda mrefu. Hapa wengine walisema ni sawa si muda mrefu na wengine wakasema ni muda mrefu. Sasa

labda niseme kwamba nafasi ya Gavana kama tunavyoona ni nafasi nyeti na yenye dhamana kubwa na inahitaji maamuzi ya hekima. Umri wa kawaida wa mtu kuhitimu shahada ya kwanza na kama vile walivyosema baadhi ya Wabunge ya Chuo Kikuu ni kama miaka 22, 23 au 25 amemaliza Chuo Kikuu. Sasa kama mhitimu huyu akiajiriwa moja kwa moja baada ya kumaliza Chuo Kikuu atapata sifa ya kuwa Gavana akifika miaka 40 na miaka 40 bado ni umri mdogo. Kwa hiyo, Serikali inaona ni busara kubakiza uzoefu wa miaka 15 kama mojawapo ya sifa ya kumwezesha mtu kuteuliwa katika nafasi ya Gavana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu Gavana kuteuliwa kuwa Mjumbe wa Bodi katika Taasisi mbalimbali nchini. Kipengele cha sheria kinachohusu kuteuliwa kwa Gavana kuwa Mjumbe wa Bodi katika Taasisi nchini kinakusudia kuhakikisha kwamba utendaji wa shughuli za Taasisi maalum kama Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa mfano *TRA* na Mamlaka ya Masoko ya Dhamana na Mitaji zinafaidika na michango ya kitaalamu kutoka Benki Kuu hasa inayohusu sera za fedha. Kwa hiyo, mara nyingi ni katika maeneo yale ambayo yanahusu masuala ya kifedha na inaonekana kwamba mchango wao wataweza kusaidia katika masuala hayo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusu kwa nini Muswada hautamki uteuzi wa Katibu wa Bodi ya Benki Kuu. Serikali imetafakari hoja hii na kuikubali kwa kuweka kipengele kwenye Muswada kinachozungumzia uteuzi wa Katibu wa Bodi na majukumu yake. Kwa hiyo, mawazo ya Waheshimiwa Wabunge tumeyakubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine lilikuwa Bodi kuweka viwango vya marupurupu na wajumbe wa Bodi. Kwa mujibu wa kifungu 14(2) cha Muswada, Bodi itapendekeza viwango vya marupurupu vya Wajumbe wa Bodi na viwango hivyo vinapaswa kupata kibali cha Waziri wa Fedha. Hivyo anayefanya maamuzi ya viwango vya marupurupu ya Wajumbe wa Bodi ni Waziri wa Fedha na sio Bodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa kinga kwa Wajumbe wa Bodi na wafanyakazi wa Benki. Kinga hapa inayozungumzwa inayotolewa chini ya sheria hii ni maamuzi yaliyofanywa kwa nia njema tu yaani *in good faith.* Kwa hiyo, hii *immunity in good faith* kwa kufuata sheria na taratibu zilizowekwa. Kwa hiyo, maamuzi yaliyofanywa kwa kufuata sheria na taratibu zilizowekwa. Vitendo ambavyo havitafanywa kwa nia njema ikiwa ni pamoja na vile vitakavyofanywa kinyume cha sheria na kinyume cha taratibu zilizopo havitahusika na kinga hii. Vitendo hivyo vitashughulikiwa kwa mujibu wa sheria nyingine za nchi.

Mheshimiwa Spika, suala lingine linahusu michango ya Benki katika utoaji wa huduma za kijamii. Nakubaliana na hoja za Waheshimiwa Wabunge juu ya umuhimu wa Benki Kuu, Benki za Biashara na Taasisi za Fedha kuchangia katika huduma kwa jamii. Benki Kuu, Benki za Biashara na Taasisi za Fedha licha ya kutekeleza majukumu yao ya kimsingi pia husaidia kutoa huduma mbalimbali za kijamii kwa wananchi. Kuna mifano mingi tu mathalani Benki Kuu ya Tanzania imeweza kusaidia katika malezi ya watoto yatima kupitia vikundi mbalimbali, kuchangia katika ujenzi wa vituo vya afya, shule za watoto wadogo, shule za msingi na hivi pia shule za sekondari.

Pia katika ujenzi wa ofisi moja katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na michango mbalimbali katika Chuo cha Usimamizi wa Fedha *(IFM),* Chuo cha Biashara na Utawala Zanzibar, Benki Kuu imeweza kuchangia katika upande wa mambo ya hospitali kwa mfano imechangia katika *Tanzania Heart Institute* katika masuala ya elimu na kadhalika. Kwa hiyo, nasema kwamba tunakubali kuna umuhimu mkubwa kwa Benki Kuu pamoja na Mabenki na Taasisi kuweza kujihusisha na masuala ya kijamii na nasema haya yanafanyika na yataendelea kufanyika.

Mheshimiwa Spika, suala lingine lilikuwa juu ya taarifa ya ukaguzi wa hesabu za ndani *Internal Audit Report* ya Benki Kuu. Awali ya yote napenda kueleza kuwa kwa mujibu wa utaratibu ulivyo hivi sasa Taarifa za Ukaguzi yaani *Internal Audit Operations Report* zinawasilishwa kwenye Kamati ya Bodi ya Ukaguzi yaani *Audit Committee* na baada ya hapo kuwasilishwa kwenye Bodi kwa hivyo inapita kwanza kwenye Kamati halafu ndiyo inakwenda kwenye Bodi. Aidha, ni vizuri kuzingatia kuwa utaratibu huu unazingatia kanuni za Kimataifa za Ukaguzi wa Ndani yaani *Internal Internal Audited Standards* kama ilivyoainishwa na Bodi ya Taifa ya Uhasibu na Ukaguzi wa Hesabu yaani *NBAA.*

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilihusu Benki Kuu kuelimisha wananchi juu ya shughuli zake. Benki Kuu napenda kusema kwamba inatumia njia mbalimbali kuelimisha wananchi kuhusu shughuli zake na hii ni pamoja na Taarifa ya Uendelezi wa Hali ya Uchumi, taarifa za robo mwaka kama nilivyoeleza, Taarifa ya Utekelezaji ya mwaka pamoja na kutoa matangazo mbalimbali kwenye gazeti, redio na pia kwenye luninga kama kunatokea na jambo lolote lile jipya basi Benki Kuu inaelimisha wananchi lakini pia kufanya semina mbalimbali kila mara kuhusu mambo mapya ambayo yanajitokeza kwa upande wa Benki Kuu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine linahusika na kutapakaa kwa Maduka ya Kubadilisha Fedha za kigeni yaani *Bureau De Change.* Hivi sasa kuna Maduka ya Kubadilika Fedha za Kigeni yapatayo 132. Maduka haya kwa sehemu mbalimbali zikiwemo Mahoteli ya Kitalii na sehemu za biashara ili kurahisisha huduma kwa watalii na wananchi kwa ujumla wake. Maduka haya hupewa leseni na usimamiwa pia na Benki Kuu. Hata hiyo, kuna baadhi ya maduka ya fedha za kigeni ambayo kwa kweli na kama mlivyoeleza Waheshimiwa Wabunge hayafuati sheria na taratibu zilizowekwa. Maduka haya yanapojulikana Benki Kuu imekuwa ikiyachukulia hatua ikiwa ni pamoja na kuyafunga. Lakini pia Waheshimiwa Wabunge wakatusaidia kwa yale ambayo wanayajua hayafuati utaratibu wa sheria. Kwa mfano, unapobadilisha fedha ni lazima upewe risiti kwa hivyo kama kuna duka lolote lile ambalo tuna hakika nalo mtupatie taarifa na kwa upande wetu pamoja na Benki Kuu tutalifuatilia.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kiwango cha chini cha akiba ya fedha za kigeni. Muswada unaitaka Benki Kuu kuwa na akiba ya fedha za kigeni wakati wote isipokuwa thamani ya mahitaji ya miezi minne ya bidhaa na huduma zinazoagizwa kutoka nje ya nchi. Hii haina maana kwamba Benki Kuu hairuhusiwi kuwa na akiba ya miezi minne. Sababu kubwa ya kuwa na kiwango cha chini cha akiba wakati wote ni kukidhi dharura inayoweza kutokea nchini kwa mfano janga la njaa na kadhalika. Kwa

hiyo, hii ni *minimum,* tunaposema miezi minne ni kiwango cha chini lakini kinaweza kwenda zaidi ya kiwango cha miezi minne. Hii ni kiwango kile ambacho tunachozungumzia cha chini kabisa.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni juu ya *ATM machine* hazifanyi kazi na hasa wakati wa usiku siku za mwisho wa wiki. Tunakubaliana na hoja hii kwamba mashine za kuchukulia fedha za *ATM* zinakuwa na matatizo na hasa siku za *weekend.* Benki Kuu itafuatilia suala hili na kuzielekeza Benki husika ili kuondoa adha kwa wateja.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kwamba *NBC* na Benki nyingine kuwa na *main servers* na *data processing centers* nje ya nchi. Mwelekeo wa Makampuni duniani kwa sasa ikiwa ni pamoja na Benki na Taasisi za Fedha za Kimataifa ikiwa ni mahali pamoja duniani ambapo kutaitwa *main server* na ndipo mahali patakapofanyika uchambuzi na matayarisho ya taarifa kwa Mawati ya Taasisi zote za Kampuni husika pamoja na Makao Makuu yaani *Consolidated Financial Statements.* Hili ni moja ya matokeo ya utandawazi na maendeleo ya teknolojia hasa ya kompyuta na mawasiliano. Hivyo baadhi ya Mabenki ambapo ni Matawi au Kampuni Tanzu za Makampuni ya Kimataifa zilizopo nchini nazo zinakumbwa na wimbi hili la utandawazi na maendeleo ya teknolojia. Mabenki ya *NBC Limited* na *Standard Chartered Bank* ni kati ya Benki ambazo zina *main server* zao na *data processing servers* nje ya nchi. Katika kuruhusu Benki na Taasisi za Fedha za kufanya hivyo Benki Kuu huzitaka Benki na Taasisi husika kutunza taarifa zote muhimu yaani *Source Documents* kwenye ofisi ya benki au taasisi husika hapa Tanzania na pia kutunza taarifa zote muhimu za kiutendaji, Bodi, Wahasibu na Wakaguzi wa ndani na nje kwa ajili ya usimamizi wa Benki Kuu. Aidha, taarifa hizi hupatikana kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, suala la uteuzi wa Gavana na Manaibu Gavana kupata kibali cha Bunge. Utaratibu uliopo hivi sasa na unapendekezwa katika Muswada ambapo Gavana na Manaibu Gavana huteuliwa na Rais unazingatia mfumo wa kisiasa uliopo nchini ambapo Rais ni sehemu ya Bunge.

Katika nchi ambazo Rais ni sehemu ya Bunge uteuzi wa watendaji unaofanywa na Rais hauhitaji uthibitisho wa Bunge. Uthibitisho wa Bunge kwa uteuzi unaofanywa na Rais uhitajika katika mfumo wa siasa ambao Rais si sehemu ya Bunge. Mfumo huu ndio unaotumika katika nchi kama vile Marekani na Ujerumani. Chini ya mfumo huu watendaji wanaohusika huwajibika moja kwa moja kwenye Bunge kwa hivyo hauhitaji kwa Tanzania tunamthibitisha tu Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kifungu namba 41 cha Muswada tumeelezwa kwamba hakieleweki na sisi tumeona ni kweli kwamba kifungu hiki hakisomeki vizuri na hivyo kifungu hicho kimefanyiwa marekebisho kwa mujibu wa jedwali la marekebisho. Pia kuna kifungu namba 23 ambacho tulileta mabadiliko *(further amendments)* na baada ya kutafakari kuhusu suala hili la *liquidation* Serikali imeona kwamba inakirudisha kifungu hiki na kwamba kifungu cha zamani kibakie.

Mheshimiwa Spika, sasa ningependa kueleza suala zima la ujenzi wa Makao Makuu ya Benki Kuu ya Tanzania yaani *BOT* na ambayo imezungumzwa pia Bungeni. Ningependa kusema yafuatayo. Jengo la Makao Makuu ya Benki Kuu ambalo limekuwa likitumika mpaka sasa lilijengwa mwaka 1969 na wakati huo wafanyakazi walikuwa 250. Hivi sasa wako wafanyakazi zaidi ya 1,300. Hivyo imelazimika kwa muda mrefu kukodi nafasi ya ofisi katika majengo mbalimbali. Wafanyakazi wako katika majumba matano, kwa mfano katika jengo la *NDC, PPF,* Jengo lazamani la *GEFCO* na jengo lililokuwa la *Import License.* Katka jengo la Makao Makuu wako wafanyakazi asilimia 35 tu na katika majengo yote haya wafanyakazi wamebanana sana kwa hiyo, kuna umuhimu kwa wafanyakazi kukaa mahali pamoja.

Sababu nyingine ni ya usalama. Benki Kuu inahifadhi fedha nyingi, nyaraka na taarifa za Serikali, Mabenki mengine na taarifa za sekta binafsi. Matayarisho ya kupanua Makao Makuu ya Benki Kuu yalianza mwaka 1987/1988 na hata msingi wa majengo marefu mawili pande zote mbili ya Jengo la Makao Makuu ulijengwa mwaka 1990. Lakini kuanzia wakati ule mpaka mwaka 1997 mradi huu ulisimamishwa mara tatu. Mwezi Septemba 1999, Serikali iliruhusu mradi wa ujenzi uendelee na hivyo *tender* ya *pre-qualification* zilitangazwa mwishoni mwa mwaka 1999. Mapema mwaka 2000 makampuni mengi ya ujenzi yalijitokeza na *tender* zao kwa awali yaani *pre- qualification* zikafanyiwa uchambuzi na *Consultancy* pamoja na Bodi ya *tender* ya Benki Kuu.

Mheshimiwa Spika, makampuni manne yalipendekezwa yaani *short listed* nayo yalikuwa ni *Greencar Construction, Group Five, Skanska Jensen* na *Veidekei.* Uchambuzi huo ulikubaliwa na Bodi ya Benki Kuu iliyokutana tarehe 25 Aprili, 2000. Hivyo makampuni haya yalikubaliwa yalete *tender* na *tender* ilifungwa tarehe 30 Mei, 2000. *Tender* zilipokewa na kufunguliwa na *Tender Committee* ya Benki Kuu, *Consultancy* walipewa *tender* hizo wazichambue, uchambuzi wa *consultancy* ulibaini kuwa *tender* ya *Skanska* ndiyo iliyoshinda kiufundi na kifedha. Bodi ya Benki Kuu ilipanga kukutana na kujadili mapendekezo hayo mwezi Julai, 2000, mara baada ya Serikali kuruhusu mradi uendelee mwezi Septemba, 1999. Barua iliandikwa na ilipelekwa kwa Balozi zote za Wahisani na Ofisi ya *IMF* na Benki ya Dunia na kwa magazeti yote. Barua hiyo ilisema kwamba Gavana na baadhi ya wafanyakazi wa Benki Kuu walikuwa wamepewa hongo ya dola milioni 4 za Marekani kutoka kwa mojawapo ya makampuni.

Lakini hakuna hata gazeti lililochapa tuhuma hii na hakuna ofisi yoyote ya wahisani ilifuatilia tuhuma hizi. Hapo ndipo gazeti la *Democrat* ambalo lilianzishwa Januari, 2000 lilichapisha barua hiyo wakati Rais, baadhi ya Mawaziri na Gavana walipokuwa Durban kuhudhuria mkutano wa *World Economic Reform Forum.* Gazeti hili lilijifilisi lenyewe mara tu baada ya kuchapa tuhuma hizi mwezi Julai.

Rais aliporudi aliitisha mkutano na waandishi wa habari na kutangaza kuwa tuhuma za rushwa zitachunguzwa kwa kina na vyombo vyote vya usalama yaani *PCB, CID* na Usalama wa Taifa. Ripoti ya uchunguzi huo ilisema kuwa hakukuwa na ukweli wowote katika tuhuma hizo. Taarifa ileleza kuwa kwa sababu hali ya uchumi na siasa

utekelezaji wa mradi huo utaarishwa kwa muda. Baada ya tangazo hilo makampuni yote yalisema kuwa yataongeza muda wa *validity* wa *tender* zao.

Mapema mwaka 2002, Serikali iliruhusu tena mradi wa kujenga Makao Makuu ya Benki Kuu endelevu. Kampuni ya *Skanska* ambayo ndiyo ilikuwa mshindi wa kwanza ilijitoa kwa sababu ya uamuzi wa kampuni hiyo katika ujenzi wa majumba katika Bara la Afrika na kuelekeza nguvu zake Ulaya na Amerika kwani *Skanska* ndiyo kampuni ya ujenzi kubwa kuliko zote Ulaya na hata duniani. Hivyo Bodi iliamua kutoa *tender* kwa mshindi wa pili yaani kampuni ya *Group Five.* Mradi ulilenga kujenga majengo matano *South Tower* na *North Tower* jengo la Mikutano jengo la *parking* na *North Block* sura ya mradi ilibadilika na kuzingazita zaidi usalama hasa baada ya Septemba 11, 2001. Hivyo *basement* ambako ziko *strong rooms* ilikuwa lazima kuimarishwa zaidi na gharama za majengo zote matano ilikuwa ni dola 108 milioni au shilingi bilioni 112.5 kwa *exchange rate* ya wakati ule.

Katika utekelezaji wa mradi mambo mengi yalijitokeza ambayo hayakuweza kujulikana wakati wa kutoa *tender* mojawapo ni usalama na upanuzi wa *strong rooms* ilikuwa lazima kuchimba kina hadi mita 15 chini ya ardhi na pia kuweka kuta mbili za *cement* yenye upana wa mita moja. Hatua hii ilikuwa ni lazima kujihadhari na wezi kuchimba chini kwa chini kwani udongo ni wa mchanga. Pili, iligundulika kuwa maji ya mvua na ya bahari yaliingia katika misingi iliyojengwa mwaka 1990 hivyo ikawa ni lazima kuimarisha misingi na kuweka tabaka la *cement* chini ya msingi kwa teknolojia ya *jet grouting* na *pyreme.* Jumba la sasa ilibidi lijengwa hivyo hivyo kwa sababu lisinge serereka.

Tatu, *North Block* ambalo lilikuwa liwe sehemu ya *North Tower* lilidhaniwa liwe jengo la kujitegemea kwa sababu ya hali ya udogo na maji mengi ardhini, hivyo gharama za jengo zimeongezeka kutoka dola za kimarekani milioni 108 mpaka kufikia 150 au kutoka shilingi bilioni 112.5 mpaka bilioni 183.9 kwa *exchange rate* ya sasa kwa majengo yote matano. Mradi huu umelipiwa kutokana na fedha ambazo Benki Kuu iliruhusiwa kuweka kila mwaka katika akaunti ya mradi kuanzia mwaka 1990 hadi hivi sasa na Benki imekuwa pia inaongeza kutokana na matumizi ya mapato yake ya kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Benki Kuu wa Mwaka 2006**
***(The Bank of Tanzania Bill 2006)***

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa ni hatua ya Kamati ya Bunge Zima na kwa kuzingatia kwamba Muswada huu ni mrefu sana na una vifungu vingi sana natumia Mamlaka yangu chini ya Kanuni ya 72, (3) ili tuweze kuupitia Muswada Sehemu kwa Sehemu badara ya Ibara kwa Ibara. *(Makofi)*

Kwa hiyo, sasa nitamwita Katibu ili atupitishe kupitia Muswada mzima kama nilivyoagiza kwa mafungu ya Sehemu za Muswada.

Sehemu ya 1

*(Sehemu ya iliyotojwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Sehemu ya 2

**MHE. BALOZI DR. GETRUDE I . MONGELLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana, katika Sehemu hii ya Pili, Ibara ya Uteuzi wa Gavana na *Deputy Governors* kuanzia Kifungu cha Sita.

Ninaomba maelezo kutoka kwa Waziri kwa nini haikutamkwa wazi wazi *gender balance* katika uteuzi huu? Nayasema haya kwa sababu sasa hivi tumefika wakati ambao kila nchi lazima iondoe kigugumizi katika kutamka kwamba wanawake wapo na hiyo inatokana na mikataba ambayo sisi kama nchi tumeridhia. Tumeridhia *The Convention of Elimination of Discrimination Against Women (CEDAW).* Marais wetu wa Afrika wamesaini *The Principle of Gender Party within the Africa Union* na *across the board at the national level.*

Kwa hiyo, tunapofika katika kipindi hiki ni vema tuache kigugumizi, tutamke wazi kwa sababu hatuwezi tukafanya vinginevyo tunapokuwa kwenye Mikutano ya Kimataifa na tunaporudi nyumbani tunashindwa kutafsiri katika sheria. Naomba maelezo katika Katiba inavyoeleza.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kabla ya Mheshimiwa Waziri hajajibu nilitaka kutoa ufafanuzi tu. Sheria zetu nyingi katika nchi hazitamki moja kwa moja *gender* na bado maendeleo ya kuwawezesha akinamama hatua kwa hatua, mwaka hadi mwaka kupata nafasi zinaendelea. Nasema hivyo kwa sababu tungechukua mantiki hiyo itabidi turudi nyuma sheria zetu zote za nchi sasa pamoja na za nyuma tufanye hivyo. Lakini Serikali inawajibu wa kujibu basi namwomba Mheshimiwa Waziri kama kuna ufafanuzi zaidi.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, nafikiri umetoa ufafanuzi vizuri kwamba Tanzania imekwenda mbele sana katika Katiba yetu imetaja wazi wazi. Kwa hivyo, nafikiri kwamba kama ulivyosema kwamba Sheria zote hazitaji lakini kwa sababu Katiba ndiyo Sheria kuu basi tunaona kwamba kwa utekelezaji naamini kabisa kwamba kwa yule ambaye anayeteua ataangalia suala hili. *(Makofi)*

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuulizia swali moja tu kuhusu *clause eighty* ama sehemu ya nane iko ukurasa wa 31, hii *clause* inazungumzia juu ya *appointment of Governor and Deputy Governors.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hiyo *clause,* sehemu ya nane ya kwanza inazungumza namna ya kupata *Governor,* sehemu ya pili inazungumzia sifa za Gavana atakataye chagauliwa, sehemu ya tatu inazungumzia juu ya uteuzi wa Manaibu Gavana. Nilitegemea baada ya sehemu ya tatu, kuwe na sehemu ya nne ambayo itataja sifa za hao watakaochaguliwa kuwa Manaibu Gavana na nilichangia na kusisitiza kwamba hilo lingezingatiwa katika sheria hii lakini nasikitika kusema kwamba katiaka marekebisho ambayo tumepewa hapa haikusema lolote kuhusu sifa za Manaibu Gavana ambao watateuliwa. Hawa watu ni muhimu kwa hiyo mimi nilikuwa napandekeza kwamba basi sifa zao zitajwe lakini kama tutaaacha wazi namna hii yoyote anaweza kuokotwa tu kwa sababu hakuana kigezo cha Sheria kinachosema kwamba awe na sifa gani. Sasa Waziri sijui kama ananona jambo hili ni jepesi sana kaliacha ama amesahau sina uhakika, naomba maelezo.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu hii ni kwamba kutakuwa na *regulations,* kwa ajili ya Ma-*deputy Governors,* na kwa upande wa Kamati ya Fedha tulipeleka hata kazi zile ambazo kila *Deputy Governor* ataweza kufanya kwa hivyo hili litakuwa hasa hasa katika *regulations.*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya majibu ya Mheshimiwa Waziri naomba nisome Kifungu cha 8 (5), hawa Ma-*Deputy Governors* pia ni *members* wa Bodi na Kifungu cha tano kinaelezea *qualifications* za *members* wa Bodi. Kinasema hivi *"Members of the Board shall be appointed on the basis of merits from the amongst persons who hold Degrees or the Equivalent qualification from Institution have learning regulars from Tanzania and experience in economics, business, finance, banking, cooperate law, accountancy etc."*

Kwa hiyo, kwa sababu hawa ni *members* wa Bodi kwa hiyo *qualification* zao ni hizi ambazo zimeelezwa hapa.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba twende kwenye ukurasa wa 31 kile Kifungu cha 8 (a), kinasema; "*Holds a University Degree,"* lakini haisemi ni *Degree* gani kwa sababu kuna *Degree* mbalimbali. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri labda *either* ya Uchumi au ya Biashara, lakini iko wazi. Umesema kwamba kuna Sheria mpya kwa hiyo ulikuwa unafikiri kwamba kwenye kifungu cha 9 (a) *The Governor who shall be the Chairman* na *Deputy* kuwa *Chairman.* Nilikuwa nafikiri kwamba tuweke *Chairperson* kwa sababu pia itahusisha wanawake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI.** Nadhani lile la kwanza kwa kuwa Gavana naye ni wa Bodi lazima naye zile fani zinamhusu. Kwa hiyo, labda hili la pili Mheshimiwa Waziri, *Chairperson rather than Chairman.*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mimi nafikiri hilo halina matatizo. Hilo la *University* nadhani limeshajibiwa.

**MWENYEKITI:** Nadhani la kwanza linatosheleza kwa maelezo ya kiti. La pili nadhani ndiyo hilo lakini nakumbushwa na wataalam hapa kwenye meza Sheria zetu zote zinasema *Chairman* na haizuiwi kuteuliwa wanawake.

**MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sipendi kusimama kuhusu kutetea haki za akinamama kama mchezo, nasimama kwa sababu ni jambo la msingi kama kuna maneno *Chairperson* yametumika ama kama tumeweza kubuni neno mtandao halikuwepo kwenye *vocabulary.* Kwa nini tufungwe na neno *Chairman* kwa sababu limekuwepo wakati wote. Kwa hiyo, kama hatukukubali *gender parity* angalau basi tukubali the *Chairperson* ambalo linatumika dunia nzima. *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Sheria inayoitwa *Interpretation of Laws Act,* ambayo kwenye Sheria hiyo ukisema he ina- *include* pia mama. Kwa hiyo, mimi nadhani ukisema *Chairman* pia hapa una-*include* pia akinamama, siyo lazima awe mwanaume hiki ni cheo tu lakini kinaweza kukaliwa na mwanaume au mwanamke. Kwa kufuata *Interpretation of Laws Act. (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani tuendelee kwa kweli hii itafanya mambo mengi, cha msingi ni nia njema ya Serikali iliyopo unaweza ukaandika unavyotaka ukipata lidikteta lisilopenda hakuna chochote, wala hakuna uteuzi. Mimi nadhani nia njema inayoendelea kuonyeshwa na Serikali ya awamu ya nne natumaini mambo yataendelea inatosha kwa sasa. *(Makofi)*

*(Sehemu iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Sehemu ya 3

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa na hoja kwenye *clause 9, sub-clause 7.*

**MWENYEKITI:** Imekwisha pitishwa tuko sehemu ya tatu.

*(Sehemu iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Sehemu ya 4

**MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI:** Kwenye Kamati tulizungumza kwamba matumizi ya neno *exchange control* ina *connotation* ambayo si nzuri kwa maana ya mwenendo wa uchumi wa dunia nzima, hivi sasa na kwa maana ya jinsi linavyotafsiriwa au lilivyotafsiriwa katika miaka ya 1970. Tulipolizungumza kifungu cha

53 kile ndicho kinaeleza habari ya *import* ya *gold, foreign exchange* na *control* ya vitu hivyo. Kwa hiyo, nilikuwa naomba kwa sababu moja ya mambo ambayo yanafanyika watu wanapoangalia nchi zinavyoendesha chumi zao ni namna gani ninyi bado mna hizi hisia za *control* za kichumi na wakatuahidi kwamba wangeweza kutatufa neno la kuweza kutumia kama wanahitaji hiyo *statement* ibaki pale. Sasa naomba maelezo kwa Waziri kwa nini hawajafanya hivyo?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii *Section 53* nimeiangalia na nimeipitia yote kuna neno tunaita *side notes* hizi *exchange control.* Lakini kwenye *Section* hiyo hakuna kitu kama hicho. Kwenye *clause* yenyewe hakuna kitu kama hicho. *Section* yenyewe inasema: *" The Bank shall perform such functions the administration of any law relating to the control of the import, export, purchase, sale or other transaction in foreign exchange and gold as may be stipulated thereof."* Ndivyo *Section* inavyosema.

**MWENYEKITI:** Sasa bahati mbaya *AG* ulivyosoma lipo neno *control* na ndiyo hilo analohoji.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** *Exchange control.*

**MWENYEKITI:** *Indeed,* ukishakuwa na *control* na inaendelea inataja na *foreign exchange, that is exchange control.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, una ushauri wowote? Naona tunapata ushauri wa kitaalam hebu tusikileze.

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha naomba nitoe maelezo kuhusu swali la Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi. Kale kakichwa kidogo yaani *exchange control* hasa tafsiri yake inatakiwa kufuatana na lili neno la kwenye sentensi yenyewe na msingi wa neno *control* wa *import* ama *export* ama *purchase* ama *sale,* ni jambo linalofanyika katika uchumi wa soko pia huwezi kuendesha uchumi wa soko bila ku-*control* vitu vingine. Kwa hiyo, neno la *control* siyo wakati wote ni baya. Kwa sababu linasimamia, kwa mfano kama una matataizo katika *foreign reserve* na huwezi kuagiza kutoka nje lazima utavi-*control.* Sasa utaviingizaje wakati wewe kama Taifa huna uwezo wa kununua vitu hivyo. Kwa hiyo, ku-*control* ni jambo jema tu na linafanywa namna hiyo na Benki Kuu ambayo ni kazi yake mojawapo. Kwa hiyo, mimi naunga mkono jambo hili.

**MWENYEKITI:** Sasa kwa kuwa Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi huna neno lolote la kushauri na inabidi twende na huu Muswada na Waziri wa Mipango anatueleza bayana kwamba *control* haina maana mbaya yoyote sijui kama unahoja tena?

**MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hoja kubwa zaidi ya aliyoisema Mheshimiwa Waziri. Lakini nilipenda kusema mimi nilishiriki, kwa mfano katika ku-*review Acts* za Benki Kuu za nchi fulani, nyingi tu kama 25. Katika mambo yanayofanyika, haya maneno yanayotumika watu wanasema *yes, they*

*still have some forms of controls.* Sasa ukilitumia hili pale *it is a still control* hailikatai hilo. Kwa hiyo, tukawa tumewaomba wafanye hivyo. Sasa neno zuri pengine ingekuwa ni kama *regulation* kwamba tuna-*regulate* tu utaratibu ambao tunauhitaji na hili ni jambo jema na lina mahusiano na jinsi tunavyoendesha chumi zetu katika dunia.

**MWENYEKITI:** Naona tafsiri hizi ni za kitaalam sana.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani labda tunaweza kuweka *foreign exchange regulation* kwa sababu inazungumzia sheria ya *foreign exchange* hapa pia. Tukisema *foreign exchange regulation* itakuwaje? Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi.

**MWENYEKITI:** Tatizo ni kwamba kuna *import, export, purchases.* Sasa siyo *foreign exchange* peke yake. Mimi nadhani Waheshimiwa Wabunge, sidhani kama kuna athari kubwa na bado tuna muda hata uchumi wetu umeendelea kuwa huria wakati maneno haya bado yapo hivi hivi. Kwa hiyo, nilikuwa nadhani twende nalo kama Serikali ilivyopendekeza siku za usoni tuna nafasi, hili ndilo Bunge, lina nguvu sana hili Bunge siku mtakapoona hili neno linatuathiri basi ama Serikali yenyewe, ama sisi wenyewe kwa hoja binafsi tunaweza tukabadili. Lakini kwa sasa nadhani tuendelee nalo.

*(Sehemu iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Sehemu ya 5

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nimeomba, angalia ile Ibara ya 70 (1) ambayo inatoa *powers to make regulations.* Nikawa nimeshauri *AG* aone uwezekano wa kutumia neno *The Minister shall make regulations,* siyo *may.* Kwa sababu usimwachie *loop hole* atengeneze au asitengeneze. Sasa nilidhani ni kwamba *what is wrong* kaweka *shall make regulations.*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Paul Kimiti, kama ifuatavyo, neno *may* lilivyotumika hapa naona ni sahihi kwa sababu linampa madaraka Mheshimiwa Waziri kutengeneza hizi *by-laws* kama ataona kwamba kuna haja ya kufanya hivyo, ndiyo sababu tunatumia neno *may.* Hata ukitumia neno *shall* haimlazimishi kutunga *by-laws* zozote kama anaona hakuna haja ya kufanya hivyo. Kwa hiyo, lazima aone kwamba kuna haja ya kufanya hivyo na ndiyo maana neno *may* lilitumika.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, mimi nilikuwa na wasi wasi kidogo kwenye kifungu namba 65(2) kinachohusu *immunity.* Kwenye kifungu hiki kinazungumzia *official* na *employees* wa Benki na kwenye *interpretations* zilizoko kwenye kifungu cha tatu haija-*define* kwa uwazi kabisa *employees* na *officials* ni nani. Kwa hiyo, tafsiri ya moja kwa moja inayokuja inamjumlisha hata Gavana na Ma-*Deputy Governors* wake.

Sasa katika mazingira hayo napata wasiwasi kidogo kwamba kama Gavana anakuwa na *interest* ata-*declare interest* yake wapi? Kwa sababu tumesema awe *independent* sasa nikafikiri ni vizuri tukaweka kipengele ambacho kinafafanua *clearly employees* na *officials* wa Benki ni watu gani na pale ambapo inamjumuisha Gavana na *Deputy Governors* basi ieleze kwa uwazi zaidi kwamba kama wana *interest* katika kitu kinachotaka kufanyika, basi ni namna gani *controls* ziwe zimewekwa, badala ya mazingira ya sasa ambayo kidogo hapa naona kama kuna *vacuum.* Asante Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, katika kuendelea kujifunza hizi shughuli zetu, napenda kuwakumbusha kwamba katika Kanuni zetu mabadiliko ya Muswada yanaweza kuletwa lakini kwa taarifa ya maandishi.

Hili ni wazo zuri sana na ninasikitika sana, sijui labda Serikali inasemaje. Maana yake likitoka Serikalini ni kwamba wao wenyewe wanabadili. Lakini kwenye *floor* bahati mbaya hatuwezi kukubali kwa sababu utaratibu hauruhusu, lazima lije badiliko mahsusi na rasmi kwa maandiko na inabidi nilihoji Bunge kuhusu badiliko.

*(Sehemu iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Benki Kuu wa Mwaka 2006**
***(The Bank of Tanzania Bill, 2006)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imepitia Muswada wa Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania ya Mwaka 2006 *(The Bank of Tanzania Bill, 2006)* sehemu kwa sehemu na kuukubali pamoja na marekebisho yake. Kwa hiyo, naomba kutoa hoja kwamba taarifa hiyo sasa ikubaliwe rasmi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naafiki

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa mara ya tatu na Kupitishwa)*

**SPIKA:** Katibu! Muswada kusomwa mara ya tatu. Ndiyo umesha usoma! Basi hatua inayofuata Waheshimiwa Wabunge, shughuli tulizojipangia kwa leo hapa zimefikia mwisho, lakini ninayo matangazo machache.

Kwanza, tumepanga utaratibu wa Waheshimiwa Wabunge kulitembelea jengo lenye ukumbi mpya ili kuanza kuzoea. Kwa hiyo, siku mbili yaani kesho na keshokutwa, Wabunge kwa makundi ya watu hamsini hamsini, watakuwa na fursa ya kulitembelea jengo lile.

Kesho, kundi la A watatembelea saa 7.30 mchana. *Form* tumewaleteeni ili mchague wenyewe. Wanaopenda kutembelea kesho saa 7.30 mchana au kesho hiyo saa 9.00 alasiri na kesho kutwa hivyo hivyo. Kwa hiyo, tumepanga makundi A, B, C na D, kwa mujibu wa siku hizo yaani Jumanne na Jumatano. Tunaomba mzirejeshe *form* hizo kwa sekretarieti ili iwezekane kazi hiyo ifanyike kwa utaratibu mzuri.

La pili, taarifa kwamba Kamati ya Kanuni za Bunge itakutana Jumatano saa 7.30 mchana katika ukumbi wa Mikutano wa Spika pale ghorofa ya kwanza. Saa 7.30 mchana wajumbe wote wa Kamati ya Kanuni za Bunge ni kikao muhimu sana kwa sababu tunakwenda kuweka sawa majina ya Kamati kulingana na sekta na Wizara ili kusiwe na mkanganyiko huo wakati tunapokwenda kwenye *Budget Session.*

Mwisho, Tume ya Huduma za Bunge itakutana siku ya Alhamisi tarehe 6 Aprili, 2006 mara baada ya kuahirishwa Bunge. Hiki ndicho kikao chetu cha kwanza cha kipindi hiki. Wajumbe wa Tume ya Huduma za Bunge wote msiondoke mbio mbio kuna mambo muhimu ya kupashana habari. Kwa hiyo, ni siku ya Alhamisi tarehe 6 Aprili, 2006 mara baada ya kuahirisha Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hapo, sasa naliahirisha Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 01.03 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumanne tarehe 04 Aprili, 2006 saa tatu asubuhi)*